Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tisa - Tarehe 19 Juni, 2009**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU -SERA, URATIBU NA BUNGE:-**

Randama za Makadirio ya Mafungu na Kasma za Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake, kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**:-

Taarifa ya Mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa Mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 67

**Kuanzishwa kwa CDA Bila Idhini ya Bunge**

**MHE. MGANA I. MSINDI** aliuliza:-

Kwa kuwa *CDA* ilianzishwa chini ya Sheria inayosimamia Mashirika ya Umma *(Public Corporation Act No.17 ya Mwaka 1969)* na bado inaendeshwa chini ya *Subsidiary Legislation* na kwamba haina idhini ya Bunge; na kwa kuwa, *CDA* ilipewa

madaraka kwa kutumia Sheria Na. 378 Kifungu cha (35), (39) na kutangazwa kwenye *GN No. 260/1974* na kupewa Hati ya Kumiliki Ardhi ndani ya Halmashauri ya Dodoma; na kwa kuwa Manispaa ya Dodoma iliazishwa kisheria mwaka 1978 na kupewa *Instrument* kwamba ni *Legal Entity:-*

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni vyema kubadili utaratibu wa kuanzishwa kwa *CDA* kwa kuletwa Muswada mpya wa Sheria Bungeni?

(b) Je, kwa kuwa Manispaa ya Dodoma ilianzishwa kisheria na ina haki ya kukushitaki na kushitakiwa. Je, Serikali haioni kuwa kuna mgongano mkubwa kati ya *CDA* na Manispaa ambacho ni chombo cha wananchi?

(c) Je, Serikali haioni kwamba inainyima fursa Manispaa ya Dodoma ya kupata misaada ya kimaendeleo toka Mashirika ya nje kama ilivyo kwa Majiji na Halmashauri nyingine hapa nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango na inakusudia kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria unaolenga kuitambua Dodoma kuwa Makao Mkuu wa Nchi yetu ambao pia utaainisha bayana na kutambulisha shughuli za Ustawishaji Makao Makuu.

Hapa naomba nisisitize kwamba tunafanya hivyo, sio kwa vile kwa sasa hatuna Sheria inayoongoza Ustawishaji wa Makao Makuu. Kwa sasa Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 inayoelekeza kutungwa kwa Sheria hii baada ya Serikali kuwa imeratibu na kuendesha mjadala wa Kitaifa utakaolenga kukusanya maoni ya wananchi na wadau mbalimbali katika kuboresha mkakati huu.

Aidha, kuanzishwa kwa Mamalaka ya Ustawishaji Makao Makuu, kuliridhiwa na Bunge la Jamhuri la Muungano ya Tanzania kupitia Sheria ya Mashariki ya Umma Na.17 ya Mwaka 1969 iliyorekebishwa chini ya kifungu Na. 29 cha Sheria ya Mashirika ya Umma *(Public Corporation Act)* ya Mwaka 1992 iliyopitishwa pia na kuidhinishwa na Bunge hili.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka hizi mbili alizotaja Mheshimiwa Mbunge, hazina mgongano wa kimaslahi kwa vile zote zimeundwa kwa kuzingatia misingi ya Sheria ikiwa ni pamoja na kila moja kuainishiwa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ambayo imeianzisha. Aidha, Waraka wa Baraza la Mawaziri Na.7 wa Mwaka 1988 umeainisha bayana majukumu ya *CDA* na pia majukumu ya Manispaa ya Dodoma. Hivyo, iwapo kila Mamlaka itatekeleza majukumu yake ipasavyo, Serikali haioni sababu ya kuwepo kwa migongano wa kiutendaji baina ya Taasisi hizi mbili. Aidha, Mbunge wa

Dodoma Mjini pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma wote ni Wajumbe wa Bodi ya Mamalaka ya Ustawishaji Makao Makuu *CDA,* hatua ambayo inalenga kuhuisha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizi mbili.

(c) Mheshimiwa Spika, Wakati Serikali ilipokuwa inaazisha Programu ya Ustawishaji Makao Makuu, ilikuwa imejiwekea lengo la kutenga rasilimali za kutosha katika kutekeleza Programu hii. Wakati huo Mashirika ya Nje hayakuhusishwa sana katika kutoa misaada ya maendeleo kwa kuamini kuwa Serikali ingeweza kuuendeleza Mji wa Dodoma chini ya Programu hiyo. Lakini kutokana na matukio mbalimbali (kama vile ule ukame wa mwaka 1974, vita ya kumng'oa Idd Amin kule Kagera, kupanda kwa bei ya mafuta duniani na kadhalika. Yaliokumba dunia na pia nchi yetu; uwezo wa kutenga rasilimali kwa ajili ya kuendeleza Dodoma, ulipungua sana. Hata hivyo Serikali imeanza kuwashirikisha wafadhili na tayari Benki ya Dunia kupitia Mradi wake wa "*Tanzania Strategic Cities Project"* unaotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeahidi kutoa jumla ya Dola milioni 28, kwa ajili ya kuendeleza miundombinu.

Kati ya fedha hizo, Mamlaka ya Ustawishaji ya Makao Makuu, imeahidiwa kupewa dola za Kimarekani 14 na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imetengewa jumla ya Dola milioni 14 ambazo zitatumiwa kukarabati miradi iliyo chini ya Manispaa na pia kuimarisha mfumo wa maji machafu ambao sasa umeanza kuzeeka.

**MHE . MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa mpango wa kuhamia Dodoma umekuwa wa muda mrefu, na wananchi wanausubiri kwa hamu, kwani Makao Makuu yakiwa Dodoma, yatarahisisha wananchi kutoka pembe zote za Tanzania, kufika kumaliza matatizo yao kama ya pension na kadhalika. Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati ijitahidi kuharakisha uhamiaji huo?

Kwa kuwa, Waziri amesema, kuna wafadhili wameahidi. Na hatujui wataanza kutoa lini,Serikali haioni kwamba kuna umuhimu Bajeti hii iongezewe fedha *CDA,* ili kutengeneza Miundombinu ambayo mingi haiko kwenye hali nzuri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, maswala yake mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana naye kwamba hakuna mradi katika nchi yetu ambao umekubaliwa sana na wananchi kama mradi au mpango huu wa kuhamisha Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Dhamira ya dhati ilikuwepo muda hule na hadi sasa dhamira hiyo iko na ndio maana mradi huu mkubwa, umetajwa mara kwa mara katika Ilani ya uchaguzi ya chama tawala. Jitihada zinazofanyika, ni pamoja na zile

nilizotaja, lakini pia nimetaja na changamoto ambazo tumekuwa tukikabiliana nazo; kwa muda huu wote. Benki ya dunia, imeahidi kuchangia Dodoma, dola za marekani milioni 28 ambazo zitaanza kutolewa kuanzia mwaka huu wa fedha unaoanza Julai, 2009 Iwapo Serikali itakuwa na mapato zaidi. Tuna hakika kwamba, mradi huu utafanikiwa katika muda wa uhai wetu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa imekuwa sasa ni wimbo ulio bora wa kusema kwamba inahamia Makao Makuu na sasa hivi majengo Dar es Salaam yanaendelea kujengwa tu ya Serikali.

Sasa Serikali, ina nieleza nini sasa, mipango ya kuhakikisha kwamba, kwasbabu *CDA* ndio wanaopima maeneo Dodoma, ni eneo lipi ambalo limetayarishwa kwa ofisi za Serikali hapa Dodoma? Ili kweli tuhakikishe kwamba tumeamia hapa Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU - SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda nimjibu Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mwanza, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Unapoongea kuhamisha Makao Makuu, hatuongei kuhusu majengo tu. Tunaongea kuhusu Miundombinu kama vile maji, shule, afya, barabara na kadhalika.

Niliwahi kusema kwenye Bunge lako Tukufu mara kadhaa kwamba, miaka ile ya 1974 ambapo mpango kabambe unaandaliwa, ilitarajiwa kwamba, watu kama 120,000, kwa maana watumishi wa Umma na wafanyabiashara wangehamia Dodoma wakati ule, lakini katika mazingira ya sasa, Chuo Kikuu cha Dodoma pekee, kinatarajiwa kuvutia watu karibu 60,000 na Vyuo vingine, watu karibu 40,000.

Kwa hiyo, ni wazi kabisa waasisi wa mpango huu, hawakuwa wametabiri wingi wa watu ambao watahamia Dodoma, mara tu Makao Makuu yatakapo kamilika.

Kwa ajili hiyo basi, katika mazingira mapya, mpango kambambe utabidi uangalie upya ili kukidhi haja ya hali ya sasa ambapo kwa watu ni zaidi ya asilimia 200 ya ile iliyokadiriwa mwaka wa 1973. *(Makofi)*

Na. 68

**Matumizi ya Majani Matika Mufungia Matenga ya Nyanya na Magunia ya Lumbesa**

**MHE. MOHAMED H. MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna kero kubwa ya vipimo vya lumbesa na kwamba Serikali inaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya vipimona kwa kuwa ufungaji wa

lumbesa hizo hutumia majani ya ukoka na majani ya aina nyingine ambayo huchafua sana mazingira:-

Je, Serikali iko tayari kutoa elimu kwa wakulima na wafanya biashara kuacha kutumia majani katika matenga ya nyanya, magunia ya lumbesa ili kuepuka uchafuzi mkubwa wa mazingira?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua matatizo yanayotokana na matumizi ya vipimo visivyo rasmi na pia ufungashaji unaotumia majani katika kusafirisha mazao ambayo hukuchangia kwa kiasi kikubwa katika uchafuzi wa mazingira na imeshaanza kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya vipimo iliyopo, ikisomwa pamoja na *GN No. 16* ya tarehe 8/2/2008, inaruhusu mazao ya kilimo na bidhaa zake kuuzwa kwa uzito na ujazo unaotakiwa (*Tenth Schedle Part IV).*

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na matumizi ya vipimo visivyo rasmi ikiwemo lumbesa, Wizara yangu kupitia Wakala wa Vipimo, imeanzisha operesheni maalum ikihusisha Mikoa ya Tanzania Bara kwa kuweka: "*Check Points*" katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kudhibiti usafirishaji wa mazao usiozingatia vipimo vinavyokubalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mkakati huo, katika kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka 2008, jumla ya watuhumiwa 449 walikamatwa na kutozwa jumla ya sh. 30,053,000/= kama faini kwa kukiuka Sheria ya ufungashaji. Operesheni hiyo, inawashirikisha viongozi mbalimbali ambao hutoa msukumo mkubwa, wakiwemoWakuu wa Mikoa/Wiliaya, Wakurugenzi Watendaji, Maafisa Tarafa, Watendaji Kata/Vijiji, Madiwani na Makamanda wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wasafirishaji wengi wanapitisha mizigo yao ya "lumbesa" usiku na siku za mapumziko kukwepa kukamatwa mchana, ukaguzi huo sasa uwe unafanyika pia usiku pamoja na siku za mapumziko.

Mheshimiwa Spika, sambamba na zoezi la ukaguzi, Wakala wa Vipimo wanatoa elimu kwa wadau mbalimbali, wakiwemo wakulima, wafanyabiashara, viongozi mbalimbali wa Serikali na viongozi katika masoko. Elimu imekuwa ikitolewa vilevile juu ya umuhimu wa matumizi ya vifungashio visivyo haribu mazingira yetu. Elimu hii, imekuwa ikifikishwa kwa wadau kwa njia ya semina, radio na luninga.

Aidha, kumekuwa na utoaji wa elimu kwa kuweka mabango/vipeperushi/picha zenye ujumbe wa kukataza matumizi ya vipimo batili, katika magazeti, sehemu zenye masoko, magulio, mitaani na barabarani.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha hayo niliyoyaeleza hapo juu, naomba kutoa rai kwa wadau wote kuongeza ushirikiano ili kukabiliana na kero hii ya vipimo visivyo halali vinavyowaibia wananchi ikiwemo lumbesa.

**MHE. MOHAMED H. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kabla ya kuuliza maswali ya nyongeza, napenda kutoa taarifa kwamba, pamoja na juhudi zote hizo za Serikali, za kuwakamata hawa wanafaya hivyo, na takwimu zote alizotupa za kukamata na juhudi za kuwatafuta usiku, magunia ya lumbesa bado yanapatikana Bandarini Dar es Salaam. Mchana na yanapakiwa kupelekwa Zanzibar. Sasa baada ya utangulizo huo, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mbali na kuwaumiza wananchi kuhusu magunia haya ya lumbesa, na kwa kuwa teknolojia yetu leo ya upakiaji na upakuzi wa mizigo bado ni ndogo, kutegemea mwanaadamu kubeba na kwa kuwa gunia hili moja lina uzito wa kilo 150 hadi 200.

Je, athari gani Serikali imechunguza kwa wananchi hawa wa Tanzania, wanaobeba magunia haya Bandarini?

(b) Swali la pili, kwa kuwa swali hili ni mtambuka, na Mheshimiwa Waziri katika jibu lake anasema juhudi zinafanyikana kwa uchafuzi wa mazingira, katika ukoka unaovikwa katika magunia haya. Lakini kwa kuwa bado hatua hiyo inaendelea hadi hivi leo, na imesababisha Zanzibar kuingia vipanya vidogovidogo ambavyo visasumbua sana na vina athari kubwa tunaipata.

Je, Waziri atakuwa tayari hivi sasa kupiga marufuku sasa hivi, ufungaji wa lumbesa kwa kutumia ukoka na kutumia njia ya zamani ya kuweka magunia haya nyeti ya kusafirisha labda nyanya, au viazi kwa kutumia neti maalum kama wanavyofungasha wenzetu wa *South Africa*?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Habib Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana kunisaidia na kuisaidia nchi, katika kupiga vita lumbesa. Sasa nikijibu swala lake la kwanza. Ni dhahiri kabisa, mwanadamu anavobeba mzigo mzito, kwa hakika lazima atahathirika.

Athari hizo, zinaweza zikatolewa kwa huakika zaidi na madaktari pamoja na Mheshimiwa Mwakyusa pale, lakini kwa uhakika, lazima kuna athari. Na kwa hivyo, pengine nitaomba Wizara ya Afya na Mheshimiwa Waziri wa Afya akiwepo hapa,

kushirikiana naye, kujua kwa uhakika ni athari zipi ili wale wanaotumia lumbesa, wajue kwamba wanawaathiri wenzao Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, ugonjwa ukisha ingia mahali hautoki upesi. Ni rahisi sana kwangu mimi kutamka hapa napiga lumbesa marufuku na nilishafanya hivyo.

Lakini bado vita vinaendelea, lililo muhimu ni Watanzania kujua kwanza, kwamba ni makosa kuwaibia wenzao kwa kutumia vipimo vya lumbesa, na pili wana athiri afya za wale ambao wanabeba magunia hayo. Na kwa hivyo, nitajitahidi kuona Afrika Kusini wanafanya nini, ntawatuma wataalamu na sisi kuweza kuanza kutumia jinsi wanavyo fungasha mizigo Afrika ya Kusini kwa manufa ya nchi yetu. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri, katika majibu yake amesema kwamba, wanaopakia lumbesa, wanasafirisha mizigo hii usiku. Mimi hivi karibuni nilikuwa katika Jimbo langu, ambako tunalima sana mahindi na mpunga. Na nimeshuhudia mwenyewe kwamba lumbesa, inajazwa mchana, wala sio usiku. Je, huko vijijini katika ngazi ya Kata na Wilaya, hakuna watu wakuchukua hatua za Kiserikali? Ambako huko huko ndiko magunia yanapakiwa? Japo sisi Wabunge tunapiga kelele, lakini hatuwezi kuchukua hatua na kuwakamata watu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzindakaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninafurahishwa na jinsi Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, kutuunga mkono katika kuvipiga vita lumbesa. Ni kweli kabisa, watendaji wa Vijiji, wa Kata, Wakuu wa Wilaya na hata Makatibu Tarafa wapo na wao ndio wanapashwa kutusaidia kutekeleza hili ambalo tunalisema la kupiga vita lumbesa.

Kwa hiyo, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwakumbusha viongozi wenzangu kwamba wanajukumu la kuhakikisha kwamba lumbesa inapigwa vita, mpaka inapofutika. Na sisi tutafanya kila linalowezekana kutoka Wizarani, kuwasaidia kupiga vita lumbesa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile naomba wafanya biashara waelewe kwamba wanapaswa kutumia vipimo ambavyo vimekubalika. Na kwa hivyo, tutajitahidi kutekeleza Sheria ambazo zipo za vipimo, kuona wale wote ambao wanakiuka, wajue kwamba tutawachukulia hatua kali.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Tanzania tunacho kiwanda chetu ambacho kinatengeneza magunia, kwa nini Serikali haiagizi kiwanda hiki kutengeneza magunia

ambayo yana uzito usiozidi kilo 100 kama kilo 75; ili kuwapunguzia wananchi tatizo la ubebaji wa magunia ya lumbesa, ikiwa ni pamoja na kujali afya zao?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Riziki Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiwanda chetu cha magunia, kina zalisha magunia ambayo yana vipimo vinavyofanana. Lakini, ukipima kwa mfano maharage, uzito wake hautafanana na viazi, na hautafanana labda na pamba na kwa hiyo, swala si magunia. Hata hivyo, lumbesa mana yake ni kuweka mzigo zaidi ya gunia.

Kwa hivyo, ukweli ni kwamba kwa upande wa kiwanda cha magunia, halina matatizo. Isipokuwa ni pale ambapo wafanyabiashara, wanavyojitahidi kuongeza mazao zaidi ya lile gunia linavyoruhusu na ndio maana tunaita lumbesa.

Kwa hivyo, bado tutaendelea na vita na tutajaribu kutafuta njia nzuri zaidi ya kuweza kupambana na vita hivi, ili tumalize hili tatizo la kuwaibia wakulima.

Na. 69

**Mradi wa Maji Mkata kutokamilika**

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa fedha nyingi zimeishatumika katika mradi wa kuleta maji katika eneo la Mji mdogo wa Mkata na vitongoji vyake (Kwapala, Komnala na kadhalika), kupitia fedha za Benki ya Dunia, na mradi huo haujakamilika ambapo kuna mabomba mengi yapo *site* na matenki ya maji yametelekezwa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa , ipo haja ya kuendeleza mradi huu ili kuepuka hasara ya mamilioni ya fedha za wananchi na Serikali, zilizokwishatumika?

(b) Je, kwanini Serikali isitekeleze na kukamilisha mradi huu kwa kuchukua maji kutoka chanzo cha Kijiji cha Kitumbi, ambapo maji yake yamepimwa na kuonekana ni salama ili kuondoa tatizo la maji katika eneo la Mkata na Vitongoji vyake?

(c) Je, Serikali haioni kuwa,mkakati huu utaongeza uwezo wa mradi wa maji wa *Handeni Trunk Main (HTM),* mradi ulioanza mwaka 1974, ili kuwafanya wananchi wa Kitumbi, Kwenkale, Mkata na Manga wapate maji bila matatizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri ya Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, naomba kutoa maelezo mafupi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji katika mji mdogo wa Mkata na vitongoji vyake ni miongoni mwa miradi iliyotekelezwa chini ya Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, katika Wilaya 14. Uzoefu uliotokana na utekelezaji wa miradi hii, ndiyo uliotumika kuandaa programmu ya kuendeleza Sekta ya Maji *(WSPD).*

Kwa bahati mbaya, mradi huu ulisitishwa baada ya kukosa maji ya kutosha chini ya ardhi katika eneo la mradi. Kwa sababu hiyo, Mkandarasi wa ujenzi wa Miundombinu ya maji, hakuweza kuanza kazi yake.

Aidha, ulikuwepo mpango wa kujenga Bwawa katika kijiji jirani cha Mkata kwa Mnara, ambalo nalo halikujengwa baada ya Mkandarasi kutoroka pamoja na kwamba, sehemu ya miundombinu ya maji kama bomba na matanki, ilikuwa imejengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Kigoda lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia wananchi wa Mji mdogo wa Mkata, Vijiji vya Mkata, Kwa Mnala na Kwa Nyange ambavyo miradi yake haikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, vimeingizwa kwenye programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, vikiwa ni vijiji vya ziada kwa vile vijiji 10 ambavyo awali vilikwishachaguliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Hivyo basi vijiji vitakavyohusika chini ya Mpango huu ni Pozo, Misima , Kibaya, Kwamsangazi, Msilwa, Kwaluala, Msaje, Gole, Kilimang'ombe, Malezi, Kwandugwa, Manga, Hoza, Komkonga, Kwamnyange, Mkata na Mkata kwa Mnara.

Chini ya Mpango huu,Halmashauri ya Wilaya yaHandeni, inaendelea na mchakato wa kumwajiri Mhandisi Mshauri ambaye ataanisha vyanzo vya Maji vinavyofaa na kufanya usanifu wa mradi. Ili kuharakisha mchakato huu, Wizara yangu imepeleka kikosi kazi cha Wahandisi Wilayani Handeni, kuisaidia Halmashauri kukamilisha kazi hiyo. Matarajio yangu ni kwamba, Mhandisi Mshauri ataanza kazi yake mwezi Ogosti, 2009.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishapima wingi na ubora wa maji katika chanzo cha maji cha Kitumbi na kubaini kwamba, maji yake yanafaa kwa matumizi ya binadamu. Kwa sababu hiyo, Mhandisi Mshauri atakayepatikana ataelekezwa kujumuisha chanzo hicho katika usanifu wa mradi mzima kama Mheshimiwa Mbunge alivyoshauri.

(c)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba, baada ya mradi wa maji niliyo utaja kukamilika , baadhi ya Vijiji vilivyokuwa vinategemea chanzo cha mradi wa *HTM*, ambao kwa sasa umechakaa, vitaboresha upatikanaji wa maji.

Hata hivyo, mradi wa *HTM* unahitaji ukarabati mkubwa. Tayari Serikali imekwishafanya makubaliano na Serikali ya Ujerumani kuukarabati mradi huo kupitia shirika lake la *GTZ.*

**MHE. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza kwa kupitia Serikali napenda kushukuru kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kutembelea mradi huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na programu tajwa iliyotajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Maji alipokuwa Handeni alishuhudia na akakiri udharura wa ile programu ya kupata maji kutoka pale Kitumbi. Na kutokana na hali hiyo mapendekezo ya mradi tayari yameshapelekwa Wizara ya Maji, mapendekezo haya yatagharimu karibu shilingi milioni 154. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba mradi huo ukifanyika sasahivi utakuwa ni rahisi zaidi badala ya kungoja kwa muda mrefu na gharama zikipanda mradi ule kushindikana kufanyika? Hilo la kwanza, swali la pili.

Mheshimiwa Spika, pampu mbili za kituo cha maji cha Segera ambazo nazo zilishaombwa Wizarani. Je, zilishapatikana au bado, kwa gharama ya shilingi milioni 74?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu masali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa mambo mawili; kwanza kwa kufuatailia kwa karibu sana yale yote yanayohusu mradi wa *Handeni Trunk Mail* kwa niaba ya wananchi wa Handeni. La pili ni ninamshukuru yeye na viongozi wa Handeni kwa kuwa na mimi katika ziara niliyofanya ya ukaguzi wa mradi huu wa *Handeni Trunk Mail.* Ni kweli tulipotembelea nilimuahidi kwamba katika hicho chanzo cha maji ambacho kipo kimepatikana na si mbali na mradi wenyewe wa Handeni wa kupeleka maji sehemu aliyoitaja basi tungekuwa na mradi wa dharura. Namuhakikishia kwamba nimetoa changamoto kwa wahandisi kwamba pamoja na kungoja mradi huu unaoweza kuchukua miaka miwili au mitatu basi maji yapo na miundombinu ipo, basi tujaribu haraka sana na kwa dharura kuhakikisha kwamba tunautekeleza huo mradi. Na ninamuhakikishia kwamba tutafanya hivyo katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pampu alizozitaja, niseme tu kwamba sisi furaha yetu ni kuwapatia watu maji. Kwahiyo lolote lile linaloweza kuwapatia watu maji sasa badala ya kesho tutalifanya. Na pampu kwa shilingi milioni 70 si kitu kikubwa sana kuwapatia wananchi maji; kwahiyo tutalifuatilia hilo ili zipatikane kwa haraka. Ahsante. *(Makofi).*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nilikuwa napenda kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wq Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utekelezaji wa mradi wa mji mdogo wa Mkata, kuna utata umejitokeza pia katika Kata ya Msingi Ishinsi ambapo mradi wa umwagiliaji ulikuwa ujengwe katika kijiji cha Ndala, lakini sasahivi umehamishiwa katika Kata ya Mwanga ambako ni kilomita 30 kutoka Ishinsi Mkoani Singida. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba katika kuhamisha mradi huo kwa wananchi ambao tayari walishaahidiwa kutaleta utata na vurugu baina ya wananchi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo. Kwanza namshukuru kwa taarifa hii ambayo amenipa, nakiri kwamba sikuwa nayo. Lakini pia napenda nimwahidi kwamba nitalifuatilia kwamba kuna mabadiliko au hakuna. Lakini pili ningependa pia kumwarifu Mheshimiwa Mlata kwamba miradi yote utaratibu tulionao ni kwamba inapangwa katika maeneo husika.

Kwa hivyo sisi kama Wizara hatuwezi tukabadilisha vipaumbele vilivyowekwa na Halmashauri ya Wilaya husika mpaka pale tunapokuwa tumejiridhisha na tumewashauri. Kwa hiyo mimi nitalifuatilia hili lakini ninataka nimhakikishie kwamba mipango yote inaanzia katika ngazi ile ya vijiji na kwenda mpaka katika Halmashauri ya Wilaya kupitia mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya; lakini nitalifuatilia.

Na. 70

**Elimu Juu ya Uvunaji wa Maji**

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo mengi nchini hasa yale ya mjini yana shida kubwa ya maji kwa matumizi ya kila siku na kwamba Serikali bado haijawa na uwezo wa kuwapatia wananchi wote maji safi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya mikakati ya uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi yao ya kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu kwa ukamilifu kabisa swali la Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maji ya mvua ndio chimbuko la maji yote yaliyoko juu na chini ya ardhi, hususan katika chemchemi, mito, mabwawa na visima. Maji ya mvua yakivunwa yanaweza kusaidia wananchi mijini na vijijini kwa ajili ya matumizi ya

nyumbani, mifugo na bustani. Aidha maji yanaweza kuvunwa kwa kutumia paa za nyumba, majaluba, malambo na mabwawa.

Mheshimiwa Spika, jukumu moja la Wizara yangu ni kuendeleza tafiti zinazohusu teknolojia zinazotumika kutoa huduma ya maji na kilimo cha umwagiliaji. Aidha Wizara inatoa mafunzo kwa wataalamu na wananchi wengine katika ngazi mbalimbali na hatimaye kutoa miongozo ya matumizi ya teknolijia hizo. Utaratibu ulipo ni kujenga kwa njia shirikishi miundombinu ya mfano katika taasisi mbalimbali zikiwemo shule, zahanati na vijiji ili baadaye wananchi wajenge miradi kama hiyo wenyewe au waiibue na kuiweka katika mipango ya maendeleo katika ngazi za kijiji na wilaya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mifano michache tu inayoonesha juhudi za serikali katika kuendeleza teknolojia ya uvunaji maji kama ifuatavyo:-

(i)Mheshimiwa Spika, kila mwaka Wizara yangu inatoa elimu katika maonesho ya kilimo kupitia Kurugenzi ya Umwagiliaji na taasisi zisizo za kiserikali kwa kuhamasisha ujenzi wa matenki rahisi ya saruji na utumiaji wa matenki ya plastiki kama *Simtank* na matofali.

Mfano ni matanki ya saruji yaliyojengwa katika shule katika Wilaya ya Iramba. Jumla ya matanki 20 yenye ujazo wa lita 46,000 kila moja yamejengwa kwa kutumia *ferrocement.*

Matanki haya yamejengwa kwenye shule za Kaselya, Mbelekesye, Mwike, Tulya, Kidaru, mwangu, Nkitnto, Grace Msaki, Juma na Ibaga. Kwa kutumia teknolojia kama hii mashirika yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Dini na wananchi wenyewe kupitia *TASAF* wanaendelea kujenga miundombinu ya kuvuna maji.

(ii) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Kitengo cha Mabwawa na Uchimbaji wa Visima ilijenga matenki kwa kutumia *ferrocement* na miundombinu ya kuhifadhi maji katika viwanja vya maonesho ya Mwalimu Julius Nyerere, huko Kilwa *road* na kupitia maonesho hayo Wizara yangu huelimisha wananchi jinsi ya kupata huduma hiyo na faida zake. Kazi ya kuelimisha matumizi ya teknolojia ya uvunaji maji ya mvua inashirikisha sekta ya maji, kilimo, afya na hata Serikali za Mitaa.

(iii) Mheshimiwa Spika, teknolojia ya uvunaji maji kwa matumizi ya umwagiliaji imekuwa ikitumika katika maeneo kame yasiyopata mvua za kutosheleza, mazao kukua mpaka kukomaa. Mfano mmoja ni utekelezaji wa ujenzi wa *ndiva* inayotumika sana na Wapare katika Wilaya ya Same.

(iv) Kwa lengo la kuboresha hifadhi na matumizi ya maji ya mvua, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, *SUA*, tangu mwaka 1992 kilijihusisha na kufanya utafiti wa hifadhi na matumizi bora ya maji ardhini ambapo uendelezaji wa uvunaji wa maji ya mvua ni sehemu muhimu ya utafiti huo. Utafiti huo umeonesha mafanikio makubwa sana katika kijiji cha Makanya huko Same.

(v) Mheshimiwa Spika, teknolojia nyingine ni ya uvunaji maji kwa njia ya majaluba. Skimu ya umwagiliaji ya Bahi ni eneo mojawapo ambalo wananchi wanaweza kujifunza teknolojia hii. Aidha katika eneo hili wanaweza pia kujifunza jinsi ya kutumia visima vifupi, kuandaa vitalu vya zao la mpunga, na kutumia maji yanayovunwa kukuzia mazao hivyo kuongeza uhakika wa kuvuna mazao yao.

(vi) Mheshimiwa Spika, uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mabwawa madogo ulitekelezwa kwa mafanikio makubwa katika Mkoa wa Mara kwa kupitia mradi uliojulikana kama *Mara Farmers Initiative Project – MFIP* uliotekelezwa na Serikali kati ya mwaka 1996 mpaka mwaka 2002. Mradi huu umeonesha mafanikio makubwa sana na sasa ni mfano wa kuigwa.

(vii) Mheshimiwa Spika, uvunaji wa maji kwa kutumia *subsurface dykes* ni njia mojawapo ya kuvuna maji kwa kujenga kuta za kukinga maji na mchanga katika mto. Teknolojia hii imeanza kutumika katika kijiji cha Mkonze hapa hapa Dodoma, ambapo Kanisa la *Menonite* wameanza kuwajengea wananchi hao makinga maji. Juhudi za Kanisa zimeongezewa nguvu na Serikali kwa kuchangia shilingi milioni 60 kuendeleza ujenzi huo.

Wizara yangu kwa kupitia kituo cha umwagiliaji cha Kanda ya Kati Dodoma, imepanga katika mwaka wa 2009/2010 kuanzisha teknolojia mbalimbali zenye ufanisi katika matumizi ya maji kwenye eneo hilo kuongeza uzalishaji wa mboga, mifano mingi. *(Makofi).*

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Lakini kama alivyosema yeye katika majibu yake, sisi katika Manispaa ya Morogoro tunacho Chuo Kikuu cha Sokoine ambacho kina wataalamu wa fani hii ya maji.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwasaidia wataalamu hawa ili waweze kuendeleza teknolojia hii ya kuvuna maji katika Manispaa hasa katika mashule?

(b)Naishukuru sana Serikali katika Bajeti iliyopita kupitia mpango wa *MCC* tumepewa pesa kwa ajili kuboresha vyanzo vya maji ndani ya Manispaa ya Morogoro. Lakini zipo Kata za pembezoni ambazo katika mradi huu maji hayawezi kuzifikia. Je, Serikali ipo tayari kusaidia katika uchimbaji wa visima vifupi ili wananchi hawa waweze kupata maji bila matatizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Mzeru kama ifutavyo. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba Serikali imeonesha pia mfano katika mradi huu wa Mkonze kwa kuuchangia au kuuongezea nguvu. Mradi ambao unatekelezwa na Kanisa la *Menonite,* hata hawa wenzetu wa *SUA* ambao nao tayari wameonesha kama nilivyosema njia kwa kufanya utafiti. Wao ni Chuo Kikuu, basi Serikali hadi sasa inashirikiana nao. Kazi zote wanazozifanya wanashirikiana sana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Napenda kusema

kwamba tutaendelea kuwasiliana na wenzetu wa *SUA* na kuhakikisha kwamba tafiti zao zinapelekwa mpaka vijijini kusudi ziweze kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza maji katika mji wa Morogoro. Napenda tu niseme kwamba mji wa Morogoro umepata bahati kwamba wao katika miradi iliyotangulia kukubalika kupata fedha za *MCC* Morogoro ni mojawapo; hivi sasa tunachokifanya ni kwamba Mhandisi Mshauri anaendelea sasa kuainisha vyanzo vingine ambavyo vinaweza kutusaidia kuongeza maji katika vyanzo vilivyopo. Kubwa zaidi ni kwamba kuna vyanzo viwili vikubwa. Kuna chanzo cha Bwawa la Mindu lakini pia kuna chanzo kingine cha maji ya mtiririko. Sasa huyu Mhandisi anachokifanya ni kuangalia uwezekano wa kuongeza bwawa la mindu ili liweze kutoa maji mengi zaidi ya kiwango kinachotokea sasa hivi. Na yale yatakapoongezeka basi vijiji vingine tuna uhakika vitaweza kupata maji maana tutaongeza maji kutoka *cubic metre* 11,000,000 za sasa mpaka karibu 48.

Kwa hiyo tuna uhakika kabisa kwamba vijiji vingine vyote hata pamoja na Mji Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, tunataka nao ufanikiwe kupata maji kupitia njia hii.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu teknolojia mbalimbali zinavyoweza kutumika katika kuvuna maji ya mvua, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile, ufanisi wa uvunaji wa maji ya mvua unategemea sana uhifadhi wa vyanzo vya maji na vidaka maji, nadhani maana yake ni *catchment areas*. Na kwa vile, hapa nchini uharibifu wa vidaka maji unaendelea kwa fujo na kwa kasi sana, kila siku tunaona milima inanyolewa kila mahali kutokana na ongezeko kubwa la binadamu wanaohitaji maeneo ya kulima na makazi.

Wizara hii inafanya juhudi gani licha ya elimu inayozungumzwa ambayo haitoshi, tunataka kuona juhudi za vitendo sio nadharia. Vitendo vinavyoonesha kwamba kuna juhudi ya kuhifadhi vidaka maji pamoja na vyanzo vya maji. Wizara hii inasemaje kuhusu utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la nyongeza la Profesa Mwalyosi, kama ifutavyo.

Mheshimiwa Spika, Profesa mwalyosi ni mdau mkubwa sana wa mambo hayo na mimi ninamshukuru kwa hilo. Mimi napenda niseme kwamba uharibifu wa *catchment areas* si suala la Wizara moja ni suala mtambuka. Kwa sababu waharibifu ni sisi wenyewe pamoja na wananchi wanaokaa katika *catchment areas* hizo, mifugo, kilimo na shughuli za binadamu. Kwa hiyo, sio kweli kwamba Wizara moja inaweza ikashughulikia suala hili likaisha, ni lazima tushirikiane na Wizara mbalimbali na hasa hasa *TAMISEMI* katika kusimamia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nimkumbushe Mheshimiwa Mwalyosi kwamba katika Kikao kilichopita cha Bunge hili, tumepitisha sheria, ya *Water Resources Management.* Ukiisoma vizuri utaona kule ndani tumezungumzia jinsi ya kusimamia matunzo ya vyanzo vya maji, tunatumia kuwafundisha wananchi lakini pia ni lazima tutumie pia na nguvu kidogo, ndio maana tumetunga sheria hii na Bunge hili limeipitisha. Kwa hiyo ninataka nimhakikishie kwamba kama Wizara pamoja na elimu tunayoitumia tumetunga pia na sheria ambayo itatusadia kuhakikisha kwamba angalau tunasimamia utunzaji wa vyanzo hivi.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kumwuliza hivi:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mbali na uvunaji wa maji ya mvua, kwa kuondosha matatizo ya maji hapa nchini lakini tunavyofahamu kwamba nchi nyingi hapa duniani huwa wanatumia maji ya bahari kwa kuya-*treat* kisayansi kwa kuyatoa chumvi na kuyatumia kwa hali ya kawaida hata ya kunywa, ziko nchi nyingi hapa duniani.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa umefika wakati muafaka wa kutumia njia hizo zinazofanywa na nchi nyingine ili tuweze kutumia maji ya chumvi kwa matumizi ya kawaida ili kuondosha tatizo la maji hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, teknolojia anayoisema Mheshimiwa Faida ya kuchuja maji ya bahari ili yafae kwa kutumiwa na binadamu ni sahihi kabisa. Ni teknolojia inayotumika katika baadhi ya nchi.

Lakini ninataka nimwambie Mheshimiwa Faida kwamba sisi hapa Tanzania, kuchuja maji ya bahari kunahitaji gharama kubwa tena kubwa sana.

Kwa hiyo sisi tungependa kwanza tuangalie uwezekano wa kutumia maji yale ambayo hayahitaji gharama kubwa namna hiyo kabla hatujaingia katika teknolojia kubwa kama hiyo lakini pale ambapo itabidi kwamba kweli vyanzo vingine vyote tumeshindwa na hakuna njia nyingine mpaka tuanze kuchuja maji ya chumvi yafae kwa kutumika basi tutaingia katika teknolojia hiyo, hatutasita kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni pamoja pia na kutumia maji mengine ambayo tayari katika nchi nyingine wanatumia maji yanayotumika. Sijui nitumie neno hilo katika vyoo, lakini baadaye yanasafishwa yanatumika. Sisi hatujafika huko kwa sababu hata yale ambayo tunayo sasa hatujaweza kuyatumia kikamilifu. Lakini nasema nimepokea ushauri wake na sisi katika kuchunguza na utafiti wetu tutaendel kulifanyia kazi hilo.

Na. 71

**Ulipaji wa Fidia Kutokana na Upanusi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Julius K. Nyerere**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius K. Nyerere umepelekea matatizo katika ulipaji wa fidia kwa wakazi wa pembezoni mwa uwanja huo:-

Je, serikali imefikia hatua gani katika ulipaji wa fidia kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wakazi wa maeneo ya Kipawa, Kipunguni na Kigilagila ambao watatakiwa kuhama ili kupisha upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwalimu Julius Nyerere, lilianza kufanyiwa kazi tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000. Changamoto kubwa kwa serikali tangu wakati huo ni ukubwa wa gharama zinazotakiwa kama fidia kwa wakazi hao kwa mujibu wa sheria na uhaba wa fedha.

Kutokana na kuchelewa kulipa fidia hizo gharama zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Wakati gharama za fidia kwa mwaka 2004 zilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 22.9 mwaka 2007 zilifikia shilingi bilioni 27.8 na kwa sasa, yaani mwaka huu 2009 gharama za fidia zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Spika, gharama za ulipaji wa fidia kwa wakazi wa maeneo yote matatu zitajumuishwa katika mradi mzima wa upanuzi na uendelezaji wa kiwanja cha ndege cha Julius Nyerere, unaotarajiwa kufanyika kwa ubia kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini kwa niaba ya Serikali na Kampuni ya China *Sonangol International Limited* kutoka Jamhuri ya watu wa China.

Kimsingi kampuni ya China *Sonangol International Limited* imeonesha kuwa tayari kutoa shilingi bilioni 30 ambazo ni dola milioni 24 za Marekani kwa Serikali ya Tanzania kama mkopo ili zitumike kulipa fidia. Kwa sasa Serikali inakamilisha mazungumzo na Kampuni hiyo kuhusu masharti ya mkopo huo kabla ya fedha hizo kutolewa.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwa mtindo huu wa Serikali kupima maeneo ya wananchi hasa makazi, kunapelekea kuchelewa pia kulipwa fidia na vivyo hivyo kupelekea kwamba wananchi kuchukizwa na serikali yao ambayo wanaipenda. Je, Serikali haioni kwamba mtindo huu umeshapitwa na wakati?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suleiman Mossy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tu nataka niseme si nia ya Serikali kuwachukiza wananchi wake. Katika zoezi hili la kukadiria fidia lililofanywa na Serikali nia yake ilikuwa ni kuwalipa wananchi haraka iwezekanavyo, lakini kama nilivyosema katika jibu la msingi ni uhaba wa fedha mabo uliikumba Serikali.

Kwa hiyo, Serikali haina nia kabisa ya kuwachukiza wananchi wake lakini nataka tu nikubaliane au niafikiane na ushauri wake kwamba katika siku za usoni Serikali itazingatia kikamilifu kuhakikisha kwamba inapopima maeneo kwa ajili ya kuwahamisha wananchi na kuwapa fidia tuweze kuzingatia upatikanaji wa fedha kwanza kabla ya kuwahamisha wananchi. *(Makofi)*

Na. 72

**Ujenzi wa Bandari ya Mwambani - Tanga**

**MHE. NURU AWADHI BAFADHIL** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kujenga Bandari sehemu ya Mwambani – Tanga; na kwa kuwa, sehemu hiyo ina kina kirefu cha maji ambapo meli kubwa toka nje na ndani ya nchi zinaweza kutia nanga kupakua na kupakia mizigo:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa bandari hiyo ya Mwambani katika Jiji la Tanga?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali ina mpango wa muda mrefu wa kujenga bandari mpya sehemu ya Mwambani – Tanga. Umuhimu wa kujenga Bandari mpya unatokana na Bandari ya sasa kuwa na kina kifupi cha maji kwenye magati yake, takriban mita mbili. Meli kubwa hulazimika kufunga kwenye maji ya kina kirefu umbali wa takriban mita mia sita kutoka kwenye gati. Matishari hutumika kusafirisha shehena kati ya meli na gati na hivyo kuwepo kwa gharama kubwa za uendeshaji. Kulingana na Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Bandari nchini, *(Port Master Plan),* mradi wa ujenzi wa Bandari mpya ya mwambani umependekezwa kuanza kutekelezwa mwaka 2011/2012. kwa mujibu wa *Master Plan* hiyo ujenzi unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 165. hata hivyo, kwa kuwa, miradi ya ujenzi wa Bandari inakusudia kushirikisha Sekta Binafsi, *Public Private Partnership (PPP),* mradi huu unaweza kuanza kutekelezwa wakati wowote mara mwekezaji ama fedha za ujenzi zitakapopatikana.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali pia ina mpango wa kujenga bandari Bagamoyo. Je, ni ipi kati ya bandari hizi itatangulia kujengwa?

Mheshimiwa Spika, iwapo itatangulia kujengwa bandari ya Bagamoyo, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kujenga Bandari ya Tanga, pindi mizigo itakaposhushwa kutoka bandarini itapakiwa na treni kuelekea bara na kuweza kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wakazi wa Jiji la Tanga sambamba na wakazi wanaoishi katika maeneo inayopita hiyo treni?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili kwa pamoja ya Mheshimiwa Bafadhil, kama ifutavyo.

Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi hapa kwamba upo mpango kabambe, yaani *Master Plan* wa uendelezaji bandari nchini. Kwa hiyo bandari hizi ambazo zimeorodheshwa katika mpango mzima huo ikiwepo ya Tanga, Bagamoyo na nyinginezo kila mpango unajitegemea kwa aina yake.

Lakini pia nimeeleza ya kwamba mpango huu mzima unategemea utekelezaji kwa kushirikiana na Sekta Binafsi yaani *Private Public Partnership (PPP).* Na nikasema kwamba kwa kadiri fedha zitakavyopatikana au muwekezaji atakayejitokeza kuanza kujenga hizo bandari, kama atajitokeza wa Bagamoyo basi tutaanza kujenga Bagamoyo kwanza lakini kama atajitokeza huko Tanga basi itaendelea kujengwa huko Tanga. Lakini kimsingi tu niseme kwamba mpango huu umeziandaa hizi bandari kila moja kwa pekeyake.

Na. 73

**Serikali Kusimamia Kilimo cha Tumbaku**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kilimo cha tumbaku kimekuwa na matatizo makubwa ya pembejeo na soko kutokana na wanunuzi kuunda vikundi vyao na kuweka bei wanazotaka:-

(a)Je, ni lini Serikali itashughulikia kikamilifu tatizo la pembejeo kwa wakulima wa tumbaku badala ya kuwaachia wakulima kupata mikopo kutoka kwa wanunuzi?

(b)Je, Serikali haioni umuhimu wa kusimamia kikamilifu ununuzi wa tumbaku kama vile ilivyosimamia zao la korosho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2006 serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilikwishaagiza kufanyike mapitio ya mfumo wa uzalishaji na masoko ya tumbaku kwa lengo la kuwafanya wakulima wa tumbaku wabebe jukumu la kununua na kusambaza pembejeo wao wenyewe badala ya makampuni ya ununuzi wa tumbaku.

Utaratibu huu umeanza kutekelezwa kwa mara ya kwanza msimu wa kilimo wa 2008/2009 katika wilaya ya Chunya ambapo Vyama vya Ushirika vya Msingi 20 kupitia Chama Kikuu cha *CHUTCU* vimepata mikopo ya pembejeo yenye jumla ya thamani ya dola za Kimarekani milioni 5.8 kutoka Benki ya *CRDB.* Vyama hivi viliitikia wito wa Serikali wa kuvitaka vijitegemee kwa pembejeo.

Hata hivyo Vyama vinane kati ya vyote vilivyopewa mikopo Wilayani Chunya, viliendelea kurubuniwa, hali iliyosababisha vyama hivyo kuasi utaratibu huu na kuendelea kutegemea Kampuni ya ununuzi wa tumbaku. Serikali imeendelea kuwahamasisha wakulima kupitia vyama vyao vya Ushirika kwenye maeneo ya Tabora, Mpanda, Ruvuma, Manyoni, Kigoma, Biharamulo, Bukombe, na Kahama kukopa pembejeo kupitia mabenki na kuondokana na utegemezi wa makampuni ya wanunuzi. Ili kufikia azma hii, Vyama vya Ushirika vya maeneo haya vimeanza maandalizi ya kukopa fedha za kununulia pembejeo za msimu wa 2009/2010.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania, inasimamia kikamilifu masoko ya zao la tumbaku katika hatua zote muhimu yaani, usajili wa vituo vya kununulia tumbaku katika hatua zote muhimu yaani, usajili wa vituo vya kununulia tumbaku, uwekaji wa madaraja ya tumbaku wakati wa msimu wa masoko. Aidha Bodi ya Tumbaku hushiriki katika vikao vya Halmashauri ya Tumbaku na kushauri ipasavyo wakati wa majadiliano ya bei kati ya wakulima na wanunuzi. Kwa kuwa, zipo tofauti za msingi kati ya zao moja na zao jingine, Serikali inafanya tathmini ili kubaini namna sahihi ya kutekeleza mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani katika zao la tumbaku kwa kuzingatia mazingira ya zao husika. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize Swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa zao la tumbaku linachangia pato kubwa la taifa na ni zao ambalo ni tegemeo hata kimataifa.

Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kwamba zao hili linapatiwa ruzuku kunusuru wakulima kutangatanga na kurubuniwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa zao la Tumbaku linategemewa sana na wananchi wa Tanzania hasa linawapatia ajira watu zaidi ya laki tano na kaya 92,000 zimekuwa registered kulima zao hili na mapato ni makubwa katika zao hili. Aidha zao hili linaongoza katika kuipatia nchi fedha za kigeni.

Suala la kwanza kwa sasa hivi ni kuhakikisha kwamba mwaka huu tumeshatenga shilingi bilioni 2.2 kusudi kusaidia kuvilipia vyama vya ushirika ambavyo vinadaiwa na makampuni haya ili viweze kujinasua katika kutegemea makampuni kuwanunulia pembejeo.

Tukishatoka hapo ndiyo tutakapofikiria kwa sababu hata hii ni ruzuku kubwa tu ya kutosha kwa maana ya kusema kwamba tunawalipia bilioni 2.2 tukishatoka hapo tutaangalia utaratibu mzuri ambao unaweza ukawasaidia wakulima hawa ili waweze kuzalisha tumbaku zaidi.

Lakini pia niseme katika mazao ambayo yametikiswa na mtikisiko wa uchumi zao la tumbaku halikutikiswa. Kwa hiyo, tunaweza pia kama Watanzania kuongeza uzalishaji ili tuweze kutumia *opportunity* hii ya zao la Tumbaku halikutikiswa kama mazao mengine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa nadhani mnaelewa ningetamani sana liulizwe la nyongeza hapa lakini kwa kuwa nimekuwa siruhusu tunaendelea. *(Makofi)*

Na. 74

**Tatizo la Kuanguka kwa Nguzo za Umeme Igombe**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara nyingi huduma ya kusukuma maji toka Bwawa la Igombe Mjini Tabora, husimama kutokana na tatizo la kukatika kwa umeme kwa sababu ya kuanguka kwa nguzo za umeme mara kwa mara; na kwa kuwa, hali hiyo huathiri upatikanaji wa maji mjini Tabora:-

Je, kwa nini *TANESCO* imeshindwa kudhibiti tatizo la kuanguka kwa nguzo za umeme kila mara katika njia ya Igombe?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la kukatikatika kwa umeme mara kwa mara kwenye njia ya umeme Msongo wa kilovoti 11 iendayo Bwawa la Igombe, kutokea kituo cha umeme cha Tabora Mjini kilichopo eneo la Kiloleni. Tatizo hili limekuwa likiathiri huduma ya kusukuma maji kutoka Bwawa la Igombe kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza. Ukatikaji umeme wa mara kwa mara husababishwa na nguzo zinazoanguka kwenye njia hiyo ya umeme yenye urefu wa kilometa 16. Sababu kubwa zinazosababisha kuanguka kwa nguzo hizo ni uchakavu wa nguzo, upepo mkali unaombatana na mvua kubwa na njia ya umeme kupitia kwenye njia yenye unyevu nyevu hivyo kusababisha nguzo kuoza mapema.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa ni kwamba, laini ilikaguliwa mwaka jana na kugundulika kuwa nguzo zipatazo 120 zimeoza. Nguzo hizo zimepangwa kubadilishwa mwaka huu. Kati ya nguzo hizo, 62 tayari zimesababishwa kati ya Januari na Juni, 2009 wakati nguzo 58 zimeshasambazwa kwenye maeneo husika na zoezi la ubadilishaji wa nguzo linaendelea. Pia hatua za ziada zimechukuliwa za kuimarsiaha usimamishaji wa nguzo kwa kuziwekea zege kwa sehemu zilizo chepechepe. Nguzo nyingi zitakazobadilishwa zipo maeneo ya mabonde ambako kumejaa maji na wananchi wamelima mpunga.

Mheshimiwa Spika, uwezekano wa kujitokeza tatizo hili la kuweka nguzo kwenye sehemu zilizo chepechepe, lilikuwa jambo ambalo taaluma ilishabaini kama tatizo ambalo lingedhibitiwa kwa kujiwekea utaratibu wa ukaguzi na matengenezo ya nguzo ya mara kwa mara. Hata hivyo matatizo ya kifedha ya *TANESCO* yaliyopelekea shirika kushindwa kutekeleza ukaguzi na matengenezo kama ilivyokuwa imepangwa.

Hivyo pamoja na kuhimiza utaratibu wa ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara ili kubaini uharibifu wa nguzo mapema, kabla hazijafikia hatua ya kuanguka na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa umeme. Serikali imeiagiza *TANESCO* kuzingatia uwekaji wa zege wakati wa kusimika nguzo kwenye maeneo chepechepe au yenye unyevu nyevu, hatua ambayo itaongeza uhai na umadhubuti wa nguzo kwenye mazingira haya. *TANESCO* wameshahakikishiwa fungu kwa ajili ya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, wakati tathimini ya upana wa kazi hizi na gharama zake inafanywa hapo awali mwaka 2007, ilikadiriwa kazi hizi zingegharimu shilingi 51.7 milioni. Hata hivyo baada ya kufanya mapitio ya kazi na gharama za sasa, kazi hii inakadiriwa kugharimu shilingi milioni 78.

**SPIKA:** Waheshimiwa mtaona tunaendelea kidogo kuvuta muda kufidia yale matangazo ya awali.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wakazi wa mjini Tabora niishukuru Serikali kwa kubaini tatizo hili na kuanza kulishughulikia kama alivyosema Naibu Waziri, lakini napenda niulize maswali mawili ya nyongeza.

Hivi kwa nini Serikali na kwa maana hiyo *TANESCO* inachukua muda mrefu sana kulikabili tatizo hili wakati wakijua kwamba TUWASA ndiyo wateja wakubwa mjini Tabora anayelipa shilingi zisizopungua milioni 20 kwa mwezi.

Je, kwa nini *TANESCO* isifanye utafiti wa njia mbadala wa kufika Igombe, ikiwa njia ya sasa ina hayo matatizo ya unyevu nyevu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwamba *TANESCO* wakati wanapitisha nyaya kwenye njia hii ya kutoka Kiloleni kwenda Igombe walishajiwekea taratibu uliopangwa kwamba kila mwaka watakuwa wanaangalia uharibifu unaotokea kwenye nguzo na kuzifanyia mabadiliko ya mara kwa mara. Lakini kama nilivyosema hali na matatizo ya *TANESCO* sisi wote tunayafahamu, utekelezaji wa azma ile ulikuwa na matatizo. Kwa hiyo, kama azma ile na mpango ule ungetekelezwa kama ulivyokadiriwa, kusema kweli tusingekuwa na tatizo hili haswa ikizingatiwa kwamba TUWASA ni miungoni mwa wateja wakubwa sana. Sasa hili la kuchukua njia mbadala, kwa sasa hivi *TANESCO* wamesema kwamba kila nguzo watakapoweka watakuwa wanaisimika na zege ndani yake ili kuondoa uwezekano wa kuoza mapema. Nadhani ni utaratibu ambao utaongeza umadhubuni na utakuwa kwanza umebakia kwenye njia fupi lakini inawezekana kwamba tutaokoa gharama na ule uwezekano wa kuoza mapema. Lakini pamoja na hayo naomba nichukue ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuangalia kama kuna njia mbadala inaweza ikakidhi mahitaji tunayokusudia, kuliko hiyo njia ya kusimika kwa kuweka *cement.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali mawili ya Wizara ya Fedha nimetazama maudhui yake ni mazito na nikienda kwa haraka haraka itakuwa haina maana kabisa. Kwa hiyo, naagiza kwamba yawekwe Jumatatu yajibiwe siku ya Jumatatu ijayo. Kwa sasa muda wa maswali umekwisha sasa tunaingia kwenye matangazo. Tunaanza na wageni, wako wageni wa Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Ludewa, nao ni Mheshimiwa Diwani Meja Mstaafu Mtima Valie wa Kata ya Malangali, na Mheshimiwa A. Haule, Diwani wa Kata ya Koma Ng’ombe pale Mchuchuma. Ahsanteni sana karibuni sana tunafurahi kuwakaribisha wageni kutoka Ludewa, moja ya Wilaya tunazozipenda sana hapa nchini msiniulize sababu yake. *(Makofi)*

Pili, mgeni wa Mheshimiwa Felister Bura, ni Mwenyekiti wa Chipukizi Kata ya Zuguni, Ndugu Edson Chipadali, karibu sana. Mgeni wa Pindi Chana, ni Mwijilisti Damian Ndelwa, karibu sana Mwinjilisti, mgeni wa Mheshimiwa Michael Lekule Laizer ni Charles Msangi, Mkuu wa shule ya Longido yaani *Longido High School.* Wapo wageni 40 wa Mheshimiwa Lucy Mayenga ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Bwana Anthony Mavunde, Mwenyekiti wa UVCC mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Wapo wageni saba wa Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa George Mkuchika, nao ni viongozi wa *Tanzania Olympic Committee,* ambao madhumuni yao ni kutayarisha siku ya *Olympic* Duniani itakayofanyika kitaifa mjini Dodoma, siku ya Jumamosi tarehe 20 Juni, 2009 saa kumi na mbili asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa katika mbio za taratibu yaani *Jogging,* itakayofanyika saa kumi na mbili asubuhi kesho nadhani kwenye uwanja wa Jamhuri kesho watakaoshiriki viongozi wa *TOC* ni Bwana Gulam Rashid Rais wa Chama hicho cha *Olympic Tanzania,* Bwana Filbert Bayi - Katibu Mkuu wa *TOC,* Ahsante sana Bwana Filbert Bayi, tunafurahi kukuona hapa, ulileta heshima kubwa sana kwa nchi yetu, heshima ambayo haiwezi kusahaulika. (*Makofi*)

Bahati mbaya sasa mbinu ulizotumia inaelekea hujazirisisha. Siku hizi hatufanikiwi sana, lakini kwa kuwa wewe ni Katibu Mkuu wa *TOC* basi endelea na juhudi zako ili tuweze kupata wanariadha bora na wazuri kjama ulivyokuwa wewe. Bwana Juma Adi Katibu Msaidizi na Juma Zaidi Muhazini Mkuu, Bi. Mwinga Mwanjala - mjumbe. Huyu naye hatuwezi kumsahau nadhani vijana waige mfano wako tutafika mbali. Ndugu Peter Mwita Mjumbe ahsante sana na Bwana Salum Khamis mjumbe, karibuni sana. *(Makofi)*

Nawatabiria kwamba Wabunge wasiopungua 60 wanaume na wanawake watakuwa nanyi kesho saa kumi na mbili asubuhi. Wageni wa Mheshimiwa James Lembeli, ni Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Nyandekwa, Ndugu Hassan Mponya, ahsante sana. Bwana Robert Mdula, mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Kata ya Ulowa, yule pale rasmi kabisa.

Wageni saba wa Mheshimiwa Kidawa Salehe na Mheshimiwa Balozi Seilf Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ni Madiwani wanawake kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja, nikiwataja msimame. Mheshimiwa Mariam Haji Zubeir, Mheshimiwa Mwanaidi Fidia, Mheshimiwa Asha Hassan, Mheshimiwa Kyembe Vuai, Mheshimiwa Nali Makame Ngwali, Mheshimiwa Sonzi Juma Sigireti na Mheshimiwa Tatu Mustafa. (*Makofi*)

Nyakati zote tunafuraha sana sisi hapa Dodoma kuwaona Ndugu zetu kutoka Zanzibar, karibuni sana. Wanafunzi kutoka Sangiti *Secondary School,* Moshi wanaosoma Kidato cha Tatu wamekuja kufanya utafiti kuhusu Elimu ya Uraia, ofisi itawapa kila ushirikiano, Ofisi ya Katibu wa Bunge ili muweze kufanya utafiti mzuri.

Waheshimiwa wapo pia wanafunzi 57 na mlezi wao wa wanafunzi wa Kiswali Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki kama tawi la chuo kikuu cha Mtakatifu Yohana, *(St. John's University),* wale 57 ahsante sana. Tunafurahia sana mko katika harakati ya kuiboresha lugha yetu ya taifa Kiswahili. Wako wageni wa *World Vision,* walezi wawezeshaji wa mradi wa *World Vision* kanda ya Kati.

Mwisho wageni wa 24 wa Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mwenyekiti wa Bunge, wanafunzi wa chuo cha uandishi wa habari wa Royal wakiongozwa na Mwalimu Bwana Haruna Taratibu na Rais wa Chuo Aloyce Nchimbi. Nadhani tuna ukumbi mwingine bila shaka wako kule wanaangalia kwenye *TV.* Hakuna matangazo ya mikutano leo. Kwa hiyo, huo ndiyo mwisho wa matangazo. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mwongozo wa Spika, Kanuni ya 68.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, endelea Mheshimiwa Kimaro.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida vikao vya Bunge kuonyeshwa moja kwa moja kupitia televisheni ya taifa na *Star TV*. Na naamini Ofisi ya Bunge inalipa, kwa kufanya hivyo Bunge lako limekuwa la viwango kabisa katika Afrika. Kwa siku za hivi karibuni televisheni ya Taifa imekuwa haionyeshi vikao vya Bajeti jioni na badala yake imekuwa inaonyesha mpira.

Mheshimiwa Spika, Watanzania hasa walioko vijijini na hata walioko nchi za nje na kwenye balozi zetu mbalimbali walipenda kuona vikao vya Bajeti. Kutokana na utaratibu huo wamenyimwa haki na fursa ya kufuatilia vikao hivyo vya Bajeti. Naomba ufafanuzi na mwongozo wako kuhusu hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Kimaro, tuna mkataba na *TBC* ambao tunaulipia wa kuonyesha vipindi vya Bunge. Bahati mbaya ulitokea mgongano na ilipotokea tu mara ya kwanza mapema wiki hii Katibu wa Bunge alimwandikia Ndugu Tido Mhando, atupe maelezo. Maelezo yake ni kwamba walikuwa na mkataba wa kibiashara na Kampuni *DSTV* kurusha matangazo ya mpira, *Confederation Cup.*

Sasa katika siku zile ambazo mambo haya mawili yaligongana, yaani Bunge na mechi ya mpira kutokana na mkataba ule mwingine kuwa na masharti magumu sana walilazimika kuonyesha mpira. Lakini hali hiyo sasa imerekebishwa, na wale mliokuwa mnaangalia ni kwamba kuanzia jana nadhani kipindi cha Bunge na leo kitaendelea kuonyeshwa. (*Makofi*)

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009
### (The Finance Bill, 2009)

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri nimeomba nataka nitoe maelezo kwa nini tumeanzisha utaratibu wa kuwa na *Finance Bill* mara baada ya hotuba ya Bajeti na Bajeti kupitishwa, kuliko kusubiri hadi mwisho. Ni kweli kabisa Mabunge mengi ya *Commonwealth* yana utaratibu wa kupitisha *Finance Bill* pamoja na *Appropriation Bill* mwisho kabisa wa mjadala wa Bajeti. Lakini tumefuatilia tukakuta kwamba mabunge hayo yana utaratibu wa mkutano wa Bajeti wote unakwisha kabla ya mwaka wa fedha mpya. Mathalan, sisi ingepaswa tuwe tunakutana mwezi wa Aprili, ndiyo tupitishe Bajeti. Kwa hiyo, kufikia Juni, 30 tungekuwa tumemaliza mkutano wa Bajeti na 1Julai, ukishapitisha hata ile *Finance Bill* ikawa ni sheria basi mambo yanaendelea.

Badiliko hilo hatujalifanya, badala yake tumekuwa na *Provisional Collection Tax.* Sheria ya mwaka 1993 iliyokuwa inaruhusu chombo cha kukusanya mapato hata kama sheria ya fedha haijapita. Baada ya kujadiliana na wakati tunaendelea kufanya mabadiliko napengine katika Bunge lijalo, Bunge la kumi linaloanza 2010, kunaweza kuwe na mabadiliko, kwa sababu katika *Hand Over Note* tutayaeleza haya, tukaona pengine kuzingatia kwamba hata mjadala wa *Finance Bill* kwa historia ukipima kwenye *hansard* haujaleta mabadiliko makubwa sana ya hatua za kodi, karibu kila mwaka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hata ile jambo kubwa linalozungumzwa kwa wakati huo kuanzia *Vote* za Wizara. Kwa kweli huwa ni matumizi, kuliko hata *Finance Bill* yenyewe. Sasa kwa kuzingatia ingekuwa vema zaidi kutokana na sababu hizo kuwa na sheria ya fedha rasmi kabisa ambayo haigongani na ile *intentions* ya *Provisional Collection Tax* kwa sababu ile nayo ilikuwa inataka kisheria tukusanye mapato. Lakini hii inaboresha zaidi kwamba unakuwa sasa na sheria rasmi na hapo hakuna mgongano, mgongano ingekuwa ni kwamba tunazuia, lakini tunaruhusu sasa kuanzia tarehe 1 Julai, fedha za mapato ya Serikali, kodi, ushuru ziweze kukusanywa. Kwa hiyo, ndiyo sababu kubwa iliyotufanya tujaribu utaratibu huu na mwaka 1963 kidogo ni mbali sasa imepita muda mrefu, sasa tuujaribu utaratibu mpya na tuone unakwendaje, nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI - MHE. OMAR YUSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2009 yaani *The Finance Act,* 2009 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya Kamati na pia tutaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo mengine yaliyowasilishwa**.** Aidha**,** kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya Bajeti ya Serikali niliyowasilisha wiki iliyopita na kupitishwa na Bunge lako Tukufu jana. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake, wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara na sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti walitoa ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni utekelezaji wa hatua kadhaa za mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya ushuru, ada na tozo mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Muswada huu ni utekelezaji kisheria wa hatua kadhaa za mfumo wa kodi, ushuru na ada mbalimbali zilizobainishwa katika hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2009/2010 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 11 Juni, 2009 na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jana tarehe 18 Juni, 2009. *(Makofi)*

Aidha, Muswada huu unakusudia kuzifanyia Marekebisho Sheria Nane zinazohusu masuala ya fedha, kodi na ushuru, kwa lengo la kuweka, kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali na kuweka mazingira mazuri zaidi ya uzalishaji hapa nchini ili kupunguza makali ya msukosuko wa uchumi duniani na kurahisisha ukusanyaji kodi. *(Makofi)*

Baadhi ya Sheria zinafanyiwa marekebisho madogo madogo yasiyo ya kisera ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Sheria hizo ni:-

1. Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura 365;

2. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;

3. Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332;

4. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290

5. Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura 189;

6. Sheria ya Tozo za Huduma za Bandari, Sura 264;

7. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, Sura 148;

8. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu muhimu tisa**.**

Sehemu ya Kwanza, inahusu masuala ya Utangulizi**,** kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura 365 kwa kuongeza kifungu kipya cha 10A ili kutambua ndani ya Sheria hii, matumizi ya nyaraka za eletroniki na kuruhusu nyaraka hizi kutumika kama ushahidi na kukubalika mahakamani.

Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka 3 wa mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* unaosisitiza utumiaji nyaraka za eletroniki ili kurahisisha ulipaji kodi wa hiari (*Self Compliance*).

Aidha, kama nilivyobainisha katika Hotuba ya Bajeti, baadhi ya marekebisho yaliyopendekezwa na Serikali yanahusu marekebisho madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho niliyowasilisha hivi punde ni sehemu ya marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya Tatu kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 katika vifungu Namba 2, 71,124, na Jedwali la Nne kama ifuatavyo:-

(a) Kurekebisha Kifungu cha 2 ili kuongeza tafsiri mpya ya neno "*Document*" ili kutambua matumizi ya nyaraka za eletroniki katika utekelezaji wa Sheria hii.

(b) Kurekebisha Kifungu cha 71 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 6 ili kutambua ndani ya Sheria hii, matumizi ya nyaraka za eletroniki na kuruhusu nyaraka hizi kutumika na kukubalika kama ushahidi mahakamani.

(c) Kurekebisha Kifungu cha 112 kwa kuongeza vifungu vidogo vya 2 na 3 ili kwanza, kubainisha utaratibu utakaotumiwa na Taasisi au mtu binafsi katika kuwasilisha nyaraka za eletroniki kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Pili, kuweka taratibu za utambuzi wa namna nyaraka za eletroniki zitakavyowasilishwa na Kamishna Mkuu wa *TRA* kwa taasisi au mtu binafsi pamoja na upokeaji wa nyaraka husika.

- Kurekebisha Kifungu cha 124 kwa kufuta kifungu kidogo cha 4 na kuweka kifungu kipya ili kuwezesha, Ushuru wa Bidhaa katika huduma za simu za mkononi kutozwa pale vocha au muda wa maongezi unapouzwa badala ya kusubiri hadi muda wa maongezi utumike kama ilivyo hivi sasa.

- Kurekebisha Jedwali la Nne ili kurekebisha kwa asilimia 7.5 viwango maalum vya Ushuru wa Bidhaa kwenye bidhaa zinazotozwa ushuru huu, isipokuwa bidhaa za petroli (*petroleum products*). Marekebisho haya yamezingatia kiasi cha wastani wa mfumuko wa bei. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

Moja, Vinywaji baridi kutoka shilingi 54 kwa lita hadi shilingi 58 kwa lita;

Mbili, bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 194 kwa lita hadi shilingi 209 kwa lita;

Tatu, bia nyingine zote, kutoka shilingi 329 kwa lita hadi shilingi 354 kwa lita;

Nne, mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,053 kwa lita hadi shilingi 1,132 kwa lita;

Tano, Vinywaji vikali, kutoka shilingi 1,561 kwa lita hadi shilingi 1,678 kwa lita; na

Sita, kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 5,348 hadi shilingi 5,749 kwa sigara elfu moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 12,618 hadi shilingi 13,564 kwa sigara elfu moja;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 22,915 hadi shilingi 24,633 kwa sigara elfu moja;

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara (*cut filler*) kutoka Shilingi 11,573 hadi shilingi 12,441 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa (*Cigar*) unabaki asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, katika Jedwali la Marekebisho, aya namba A, yamefanyika marekebisho madogo katika sehemu hii ya tatu ya Muswada hususan, ukurasa wa 7 ili kurekebisha makosa ya kiuchapaji.

Sehemu ya Nne, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kifungu kipya cha 136A ili kwanza, kubainisha utaratibu utakaotumiwa na taasisi au mtu binafsi katika kuwasilisha nyaraka za eletroniki kwa Kamishna Mkuu wa *TRA* na upokeaji wa nyaraka husika.

Pili, kuweka taratibu za utambuzi wa namna nyaraka za eletroniki zitakavyowasilishwa na Kamishna Mkuu wa TRA kwa taasisi au mtu binafsi pamoja na taratibu za upokeaji wa nyaraka husika.

(b) Kuongeza kifungu kipya cha 139A ili kutambua ndani ya Sheria hii, matumizi ya nyaraka za eletroniki na kuruhusu nyaraka hizi kutumika kama ushahidi Mahakamani.

(c) Kurekebisha aya ya 3 (2) ili kuruhusu unafuu wa kulipa kiwango cha Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 ya faida hadi asilimia 25 kwa kampuni zinazoorodheshwa katika soko la mitaji utumike kwa kampuni ambazo zitauza angalau asilimia 30 ya hisa zake kwa wananchi. Hivi sasa unafuu huu ni kwa ajili ya kampuni zinazouza angalau

asilimia 35 ya hisa zake kwa wananchi. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha kampuni kujiorodhesha katika soko la mitaji na kuongeza umiliki wa wananchi kwenye hisa za kampuni binafsi. Hatua hii inazingatia maamuzi ya Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Sehemu ya Tano, inapendekeza kurekebisha aya ya 1 ya Jedwali la Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kupunguza kiwango cha ukomo cha kutoza ushuru wa mazao kutoka asilimia 5 ya bei ya kuuza mazao shambani hadi asilimia 3 ili kupunguza makali ya athari za msukosuko wa uchumi duniani kwa wakulima nchini. Hata hivyo, kama nilivyobainisha katika Hotuba ya Bajeti, marekebisho haya yataanza kutumika katika mwaka wa fedha 2010/2011, ili kutoa nafasi kwa Serikali za Mitaa kujiandaa kupata vyanzo mbadala vya mapato.

Sehemu ya Sita, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 2 cha Sheria ya Ushuru wa Stempu kwa kuongeza maneno ”*in a paper or electronic form*” katika tafsiri ya neno ”*instrument*” ili kutambua ndani ya sheria hii, matumizi ya nyaraka za eletroniki.

Sehemu ya Saba, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Tozo za Huduma za Bandari, Sura Na. 264; ili kutambua ndani ya Sheria hii, matumizi ya nyaraka za eletroniki na kuruhusu nyaraka hizi kutumika kama ushahidi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane, kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kama ifuatavyo:-

- Kurekebisha kifungu cha pili kwa kuingiza tafsiri ya maneno ”*document” na* ”*lodge*” ili kutambua ndani ya Sheria hii, matumizi ya nyaraka za eletroniki;

- Kurekebisha kifungu cha 8, ili kupunguza kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani kutoka asimilia 20 ya mauzo hadi asilimia 18 ya mauzo. Lengo la hatua hii ni kupunguza makali ya athari za msukosuko wa uchumi duniani. Aidha, hatua hii inatarajiwa kujenga mazingira ya kuongeza kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari;

- Kurekebisha kifungu cha 13 kwa kuongeza kifungu kidogo cha 4, ili kuwezesha Kodi ya Ongezeko la Thamani kutozwa kwenye muda wa maongezi kwenye simu kwa kuzingatia bei halisi inayoonyeshwa kwenye vocha badala ya bei nafuu anayotozwa muuzaji wa jumla. Lengo la hatua hii ni kuhuisha mapato yatokanayo na chanzo hiki cha kodi na kuziba mwanya wa ukwepaji kodi;

- Kurekebisha kifungu cha 26, kwa kuongeza vifungu vidogo vipya vya 4 na 5 ili kwanza, kubainisha utaratibu utakaotumiwa na taasisi au mtu binafsi katika kuwasilisha nyaraka za eletroniki kwa Kamishna Mkuu wa TRA na upokeaji wa nyaraka husika. Pili, kuweka taratibu za utambuzi wa namna nyaraka za eletroniki zitakavyowasilishwa na Kamishna Mkuu wa TRA kwa taasisi au mtu binafsi pamoja na taratibu za upokeaji wa nyaraka husika; na

- Kurekebisha kifungu cha 37 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha 9, ili kuruhusu ndani ya Sheria hii matumizi ya nyaraka za eletroniki kwenye ushahidi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, jedwali la pili, (linalohusu bidhaa na huduma zilizosamehewa kodi ”*exempt supplies and imports*) Kwanza, katika aya ya 1, kufuta aya ndogo za (6) na (7) ili kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye chai na kahawa iliyozalishwa na kusindikwa hapa nchini ili kuleta usawa na mazao mengine yaliyosindikwa ambayo hutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hivi sasa, mazao yote ambayo hayajasindikwa, hayatozwi kodi hii. Pili, Kufuta aya ya 7 na kuiandika upya ili:-

Moja, kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kukodi ndege (*air charter services*) kwa kuwa huduma hizi hutolewa kibiashara kama huduma za kukodi vyombo vingine vya usafiri ambazo kisheria hulipiwa kodi.

Pili, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za upakiaji na upakuaji mizigo kwenye meli za hapa nchini kwa mizigo inayotoka nje ya nchi na ambayo huduma ya kupakua mizigo kutoka kwenye meli iliyoleta mizigo kutoka nje ya nchi ilishatozwa kodi hii. Hatua hii inalenga kuhamasisha wafanyabiashara kushusha mizigo katika bandari zetu za Tanga na Mtwara na hivyo kupunguza msongamano wa meli na mizigo katika bandari ya Dar es Salaam. Aidha, katika jedwali la marekebisho, aya namba B yamefanyika marekebisho madogo ya kiuandishi ili kifungu hiki kisomeke vizuri.

Tatu, Kufuta aya ya 8 na kuiandika upya ili kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za upangishaji na ukodishaji wa nyumba na majengo (*leased buildings and serviced apartments*) isipokuwa zile zinazotolewa na Shirika la Nyumba la Taifa na Msajili wa Majengo. Hatua hii haitahusisha upangishaji wa nyumba na makazi ya kawaida ya wananchi kwa vile mapato wanayopata wapangishaji kutoka kwenye ada ya pango hayafikii kiwango cha usajili cha Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Registration Threshold*).

Nne, kurekebisha aya ya 19, kwa kuondoa maneno “*and specified cash register*” ili kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine za elektroniki za kutunza kumbukumbu za mauzo (*electronic cash register*) kwa kuwa mashine hizi hazitumiki tena kwa kazi hiyo na badala yake Mamlaka ya Mapato Tanzania wataanzisha, kwa awamu, matumizi ya mashine mpya za elektroniki za kutunza kumbukumbu za kodi (*electronic tax register).*

Tano, kufuta aya ya 27 na kuiandika upya ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kilimo za kutayarisha mashamba, kulima, kupanda na kuvuna ili kupunguza gharama za uzalishaji kwenye kilimo. Hivi sasa pembejeo za kilimo na mbolea zinasamehewa kodi hii.

Sita, kuongeza aya mpya ya 28 ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye matanki maalum ya kuhifadhi maziwa (*heat insulated milk cooling tanks*) na

vipipa vya alumini (*alminium jerry cans*) vya kukusanya maziwa ili kuhamasisha matumizi ya vyombo hivi kwa ajili ya kukusanya na kuhifadhi maziwa na hivyo kuongeza ubora wa maziwa na kipato kwa wananchi.

Saba, kuongeza aya namba 29 ili kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma ya uuzaji wa vocha za simu pale huduma hii inapotolewa na mawakala. Msamaha huu hautahusisha huduma za aina hii pale zinapotolewa na kampuni za simu. Lengo la hatua hii ni kuzuia utozaji kodi mara mbili kwa kuwa kwa utaratibu uliopo chini ya sheria hii, kampuni za simu (*service providers*) wanapaswa kulipa kodi ya *VAT* pale wanapotoa huduma ya uuzaji vocha kwa mawakala (*dealers*).

Mheshimiwa Spika, jedwali la tatu, kwanza, kufuta aya namba 8 na 8A na kuiandika upya ili kupunguza wigo wa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief*) kwa kampuni za madini, mafuta ya petroli na gesi ili msamaha huo uhusishe shughuli za utafiti na utafutaji pekee ambazo hufanywa na mwekezaji kabla ya kuanza uzalishaji.

Pili, kufuta aya namba 9 na kuiandika upya ili kupanua wigo wa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief*), unaotolewa kwenye maduka yasiyotoza kodi ya Jeshi la Ulinzi (*Defence Forces Duty Free Shops*), ili kujumuisha Majeshi yote ya Ulinzi na Usalama (*Armed Forces*).

Aidha, utawekwa utaratibu maalum wa kusimamia msamaha huu ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutangaza katika Gazeti la Serikali orodha ya bidhaa zitakazohusika na msamaha ili kuzuia matumizi mabaya ya msamaha husika kwa vyombo hivi.

Tatu, kupitia jedwali la marekebisho, yamefanyika marekebisho kwa kufuta kifungu cha 28(d) cha Muswada, ili kurejesha msamaha maalumu wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief*) kwa mashirika ya dini na mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGO).* Kama nilivyoelekeza jana wakati wa kuhitimisha mjadala wa bajeti, Serikali kwa kushirikiana na taasisi za dini, itaunda Kamati ya pamoja itakayojumuisha wawakilishi wa madhehebu ya dini, *TRA* na Serikali ili kuandaa utaratibu wa wazi utakaoweza kuziba mianya yote ya matumizi mabaya ya misamaha hii.

Nne, kufuta aya ya 15 na kuandika upya ili kupunguza wigo wa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief*) kwa asasi na mamlaka za maji safi na taka nchini ili msamaha huo uhusishe vifaa na huduma zitakazohusika katika ujenzi wa miundombinu ya maji safi na taka pekee. Hatua hii inalenga kuziba mwanya wa matumizi mabaya ya msamaha huu ambapo hivi sasa unahusisha bidhaa za aina yoyote. Aidha, kupitia jedwali la marekebisho, yamefanyika marekebisho ya kiuandishi ili kifungu hiki kisomeke vizuri.

Tano, inapendekezwa kurekebisha aya ya 18 kwa kufuta maneno "*pharmaceutical products and"* ili kuondoa msamaha maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT Special Relief)* kwenye mali ghafi na vifungashio kwa wazalishaji wa ndani wa madawa ya binadamu kwa kuwa wazalishaji wa ndani wa madawa tayari wanapata unafuu wa

kodi kupitia Jedwali la Kwanza ambapo wanawajibika kulipa kodi na baadaye kurejeshewa ili kutoa muda wa kutosha kwa wazalishaji kujiandaa bila kuathiri uzalishaji. Aidha, kama nilivyobainisha katika hotuba ya bajeti, hatua hii itaanza kutekelezwa rasmi tarehe 1 Januari, 2010.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa na ya mwisho iliyoainishwa kupitia aya namba D ya Jedwali la marekebisho inapendekeza kurekebisha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197 kama ifuatavyo:-

- Kurekebisha kifungu cha 20 kwa kuongeza kifungu kipya cha 7 ili kubainisha kwamba Benki Kuu ya Tanzania itawasilisha taarifa ya hesabu zake za mwaka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ndani ya kipindi cha miezi 3 baada ya kufunga mwaka. Hivi sasa Sheria ya Benki Kuu haitamki bayana matakwa haya. Lengo la marekebisho haya ni kuhuisha Sheria hii na matakwa ya Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma ya mwaka 2008 inayoelekeza Wizara na Taasisi za Umma kuwasilisha taarifa ya hesabu zake za mwaka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ndani ya kipindi cha miezi 3 baada ya kufunga mwaka.

- Kurekebisha kifungu cha 21, kifungu kidogo cha 1, ili kubainisha kwamba Benki Kuu itawasilisha taarifa ya hesabu zake za mwaka kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kufunga mwaka. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Benki Kuu ya Tanzania kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha taarifa yake ya mwaka ambayo itajumuisha taarifa ya hesabu zake za mwaka zilizofanyiwa ukaguzi na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zilizobainishwa katika hotuba ya bajeti, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Matangazo ya Serikali (*Government Notices)* kwa mujibu wa matakwa ya sheria husika. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Kufuta Matangazo ya Serikali 405 yalitolewa katika kipindi cha mwaka 1964 hadi 2005 ambayo yanatoa misamaha ya kodi kwa kampuni binafsi; asasi zisizo za kiserikali; taasisi za kidini; mashirika ya kimataifa na miradi ya mbalimbali iliyokwishakamilika ili kuziba mwanya wa kuvujisha mapato ya Serikali;

- Kuondoa msamaha wa Ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli na dizeli kwa makampuni ya madini unaotolewa kupitia Tangazo la Serikali namba 480 la mwaka 2002;

- Kuondoa msamaha wa Ushuru wa Mafuta ya Petroli na dizeli kwa mafuta yanayotumiwa na kampuni za madini kwa kufuta Tangazo la Serikali Namba 99 la mwaka 2005.

Marekebisho haya yatahusu kampuni za madini zitakazoingia mkataba na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2009 kwa kuzingatia kwamba, mikataba baina ya Serikali na Kampuni za madini (MDA’S) iliyopo hivi sasa inatambua misamaha hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza jana wakati wa majumuisho ya hotuba ya bajeti, kwa kuwa suala la msamaha wa ushuru wa mafuta kwa makampuni haya limebainishwa kwenye mikataba ya madini, suala hili litapelekwa kwa Wanasheria wetu kwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya viwango vya ada ya *VISA* ili kutoza kiwango kimoja kisichozidi dola hamsini kwa nchi zote. Kuanzia mwezi Oktoba, 2007, Tanzania imekuwa ikitoza ada ya *VISA* ya kiasi cha dola 50 kwa mataifa yote isipokuwa kwa nchi chache ambazo Tanzania imeingia nazo makubaliano maalumu ya kutoza viwango sawa (*reciprocal arrangement*); Mfano wa nchi hizi na viwango vya ada ya VISA ni kama Pakistani dola 200, Marekani na Ireland Dola 100 na Burundi dola 20. Serikali itafanya majadiliano na nchi ambazo zinatoza ada ya *VISA* ya zaidi ya dola 50 kwa raia wa Tanzania ili nazo zitoze kiwango cha dola 50.

Marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara na Idara zinazojitegemea.

Marekebisho ya kuongeza kima cha chini cha penshenii kutoka kiwango cha sasa cha Sh. 21,601.05 kwa mwezi na kuwa Sh.50,114/= kwa mwezi kuanzia Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza, ni utekelezaji kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 ambayo tayari yameridhiwa na Bunge hili wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Kwa hiyo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuhalalisha kisheria bajeti iliyokwishapitishwa jana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iIlitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi baada ya Kuchambua na Kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009 (*The Finance Act*, 2009), unaokusudia kupendekeza marekebisho katika Mfumo wa Kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya ushuru, ada na tozo mbalimbali.

Kimsingi Kamati imekubaliana na mapendekezo ya marekebisho yote ya Muswada huu ambayo ni utekelezaji Kisheria wa mapendekezo ya Serikali ambayo

yameridhiwa na Bunge lako Tukufu jana tarehe 18 Juni, 2009 wakati tulipohitimisha hotuba ya bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakupongeza kwa kubainisha kasoro iliyojitokeza katika Kanuni ya 106, Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2007 ambapo Muswada huu ulitakiwa kuwasilishwa hapa Bungeni mara baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kupitisha Muswada wa Fedha. Kimsingi utaratibu huu ulikuwa unaiweka Serikali mahali pagumu kisheria katika mchakato wa kutoza kodi unaotakiwa kuanza tarehe 01 Julai, 2009. Hii inadhihirisha lengo lako la kulifanya Bunge hili kuwa la Viwango na Kasi (*Standard and Speed*).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati ilikubaliana kimsingi na maeneo yote ya marekebisho ya Sheria ya Muswada yaliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Pamoja na hivyo, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo katika baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri alikubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa msamaha wa ushuru wa mafuta ya *petrol* yanayotumiwa na Kampuni za Madini kwa kufuta Tangazo la Serikali Namba 99 la Mwaka 2005. Marekebisho haya yatahusu Kampuni za Madini zitakazoingia Mkataba na Serikali kuanzia tarehe 01 Julai, 2009. Eneo hili lilileta utata kutokana na Tangazo hilo kutolewa na Serikali baada ya baadhi ya mikataba ya makampuni makubwa kusainiwa (2004 kurudi nyuma). Aidha, kuna maoni kwamba Serikali iondoe msamaha huo moja kwa moja. Kamati ilibaini kuwa kuondoa msamaha huo moja kwa moja kwa kuyahusisha makampuni ya zamani kutaleta mgongano wa kimaslahi baina ya Serikali na makampuni hayo. Kwa sababu hiyo, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali na kuisisitiza iendelee kufanya mazungumzo na kampuni za madini zenye mikataba, ili kuondoa kipengele kinachohusu msamaha huo kwenye mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati imeridhika na marekebisho yote ya viwango vya ushuru wa pamoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Kamati imetoa tahadhari juu ya kuondoa Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 unatozwa kwenye mafuta ghafi ya kula ya Mawese (*Crude Palm Oil)* na kutoza asilimia sifuri; kwamba eneo hili litazamwe upya na kuzingatia ipasavyo kauli mbiu ya bajeti ya mwaka huu kwamba Kilimo Kwanza, ambayo inataka tuwahimize wakulima wazalishe kwa wingi mbegu za mafuta na kukidhi mahitaji ya viwanda vyetu vya ndani kwa sababu vinginevyo tutaviua hasa ikizingatiwa kuwa viwanda vya ndani vitalipa *VAT* asilimia 18. Hata hivyo, ili kuleta ushindani ulio sawa baina ya viwanda vyetu na vile vya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inapendekeza Viwanda hivyo visamehewe *VAT*.

Aidha, Kamati inapendekeza Wizara ya Viwanda na Biashara, ifanye utafiti kujua mahitaji halisi ya mbegu za mafuta katika Viwanda vya Kusindika Mafuta ya kula na uwezo wa uzalishaji ili kubainisha uhalali wa kuendelea na asilimia sifuri au kurejesha ushuru huo wa asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye Chai na Kahawa. Kamati ilibaini kuwa katika mwaka 2004, Serikali ilifuta *VAT* kwenye Chai inayozalishwa hapa nchini kwa lengo la kukuza viwanda vya Chai na kuepuka kuletwa kwa chai isiyofaa hapa nchini na kuleta ushindani ulio sawa. Kutokana na maamuzi hayo, uzalishaji wa Chai uliongezeka toka tani 30,000 Mwaka 2003/2004 hadi tani 37,000 Mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kurejeshwa kwa Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) kwenye Chai na Kahawa, ni kudhoofisha makusudio au maamuzi ya awali, jambo ambalo Kamati imeshindwa kuelewa ni kwa maslahi ya nani. Kamati inaamini kuwa ili kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, Serikali haina budi kutoa *incentives* katika sekta ya kilimo, hivyo Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya uamuzi wake wa kuondoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye Chai.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kutekeleza ushauri wa Kamati tulioutoa wakati tulipowasilisha maoni ya Kamati kuhusu bajeti ya Serikali kwa mwaka 2009/2010, kuhusu Serikali kukaa na Mashirika ya Dini na kutoa mwongozo na ufafanuzi mzuri wa namna ya kuziba mianya yote ya ukwepaji kodi ili kurejesha msamaha maalum wa *VAT* kwa Asasi zisizokuwa za Kiserikali *(NGOs)* na Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuona umuhimu wa hoja hii na kuitisha kikao baina ya Serikali na Viongozi wa Mashirika ya Dini tarehe 17 Juni, 2009, kikao ambacho kimezaa suluhisho kwa Serikali kukubali kurejesha msamaha huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu, kwa michango yao makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia kuboresha Muswada huu. Kama ilivyo ada ingefaa niwatambue hapa lakini kwa sababu itakuwa kwenye *Hansard* na tulikwishawatambua kwenye hotuba yetu iliyopita, nadhani itabakia kwenye *Hansard*. Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhab Fereji, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Athuman Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence B. Liamba, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Hamad R. Mohamed, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Mossy Mussa, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omary N. Mzeru, Mheshimiwa Murad Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, naomba kukushukuru wewe binafsi kwanza kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na pia kukushukuru wewe, Naibu Spika na Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii, kufanya kazi ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii, nimshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Mbunge na Manaibu wake, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee. Pia niwashukuru Gavana wa Benki Kuu, Profesa Ben Ndulu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Katibu Mkuu, Ndugu Alhaji Kija, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato, Ndugu Kitilia; kwa kuisaidia Kamati kufanikisha kujadili na kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Lawrence Robert Makigi, kwa kazi nzuri katika kuihudumia Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Sasa ni zamu ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2009 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru Wabunge wote na hasa wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wao katika kipindi hiki kigumu cha matayarisho na mawasilisho ya hotuba zetu. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutoa salamu za pole kwa familia za Mheshimiwa Ania Said Chaurembo (Mb), Mhe.shimiwa Paschal Degera (Mb), kwa kuondokewa na wazazi wao wapendwa. Mwenyezi Mungu awape roho ya ustahimilivu katika kipindi hiki cha majonzi. Amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba sasa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2009 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Kambi ya Upinzani ilivyosema wakati ikiwasilisha maoni ya bajeti kuhusiana na fedha zilizotengwa za *"stimulus package"* kuwa itungwe jedwali maalum kwenye marekebisho ya Muswada huu wa fedha, ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi nzuri ya kutoa mawazo yao wakati wanapitisha

Muswada kuhusiana na fedha za kunusuru makampuni mbalimbali, bado tunashikilia msimamo huo kwa kuwa fedha za mpango huo nyingi hazionekani kwenye bajeti ya Serikali kama tulivyosema katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Spika**,** Kambi ya Upinzani baada ya kupitia kwa harakaharaka kwenye vifungu vilivyotengwa kwa ajili ya safari za ndani na nje ya nchi kwa Wizara mbalimbali ambazo ni Tshs. 34,637,638,460/= (Tshs.34.64billion). Kati ya hizo, safari za ndani ni Tshs. 22,979,125,660/=. Mfano mwingine mdogo, ni Fungu 20 na 30 posho tu zinafikia Tshs.1,049,770,000/= ( Tshs. 1.0478 billion), wakati "*Allowance In Kind*" Tshs.19 billion zaidi ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa fedha zilizotengwa kwa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli nchi ambayo iko kwenye kipindi kigumu cha msukosuko wa uchumi, kutumia fedha hizo kwa matumizi hayo ni sahihi? Kambi ya Upinzani inaona hapa kwa kweli ni kuwadhihaki walipa kodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004**.** Katika Muswada huu, viwango mbalimbali vya kodi vinaongezwa na kupunguzwa, ni jambo zuri kwani vile vinavyoongezwa, vinakusudia kuongeza kiwango cha mapato na vile vinavyopunguzwa vinakusudia kuwasaidia wananchi katika kuyafikia maendeleo yao. Lakini pamoja na hayo, ukusanyaji mkubwa wa kiwango kikubwa cha kodi kutoka kwa wananchi unatakiwa uende sambamba na upatikanaji wa huduma muhimu kama vile huduma za maji, umeme, barabara na nyinginezo. Tanzania hili ni tofauti, kodi kubwa inayokusanywa inakwenda kwenye matumizi ya kawaida, ambayo hayawezi kuleta maendeleo ya uchumi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kilio kingine cha Kambi ya Upinzani ni uwepo wa misamaha mingi ya kodi isiyo ya lazima katika sekta mbalimbali za uchumi inayotolewa kupitia sheria hii na sheria nyingine zinazokwenda sambamba na sheria hii. Mfano, sekta ya madini na uwekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hizi ni sekta za msingi ambazo zingeweza kuliingizia Taifa hili fedha ya kutosha kujiendesha, lakini misamaha mingi ya kodi kwa kisingizio cha kuwavutia wawekezaji ni tatizo. Kwa mujibu wa taarifa kutoka chapisho la " *THE DEMYSTIFICATION OF MINING CONTRACTS IN TANZANIA*" Tanzania ni mzalishaji mkubwa wa tatu wa dhahabu kwa Afrika, ukitoa Ghana na Afrika ya Kusini, lakini sekta hiyo ya madini inachangia kwa asilimia 3.2% ya *GDP* na asilimia 3.6% tu ya mapato ya Serikali yatokanayo na kodi.

Hali hii inatokana na kutunga Sheria na kuingia katika mikataba na wawekezaji yenye masharti ya kutobadilisha viwango vya kodi mbalimbali vinavyostahili kulipwa na makampuni hayo hata kama viwango hivyo vitabadilika katika hali ya kawaida ya mabadiliko ya sheria.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kushuhudia Serikali inavyoyaogopa na kuyakumbatia makampuni yanayochimba madini. Serikali imependekezwa kuondoa

msamaha wa Ushuru wa Mafuta ya Petroli, kwa mafuta yanayotumiwa na kampuni za madini, kwa kufuta Tangazo la Serikali namba 99 la mwaka 2005. Marekebisho haya yanahusu kampuni za madini zitakazoingia mkataba na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2009. Kwa nini ufutaji wa misamaha hii usiyaguse makampuni yaliyopo hivi sasa?. Serikali inaendelea kulinda mikataba ya kifisadi kwa manufaa ya nani?

Mheshimiwa Spika, Bunge lako litakumbuka, Mheshimiwa Rais alipokuja kulihutubia Bunge tarehe 30,12 2005, aliahidi kuwa, katika kipindi hiki atapitia mikataba ya madini, katika kutekeleza hilo, Raisi aliunda Tume ya Jaji Bomani. Bunge lako Tukufu lilijadili na kupitisha Azimio la kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Jaji Bomani, katika mambo yaliyoazimiwa na Bunge lako Tukufu ni pamoja na kufutwa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa badiliko alilolitoa Waziri wa Fedha la kufuta utekelezaji wa GN.99, kuanzia Julai 2009, kwa makampuni yatakayo sajiliwa sasa, ndio kutekeleza azimio la Bunge lililotokana na taarifa ya Jaji Bomani?

Mheshimiwa Spika**,** Bunge hili liazimie na liitake Serikali katika bajeti hii kuyatekeleza mapendekezo ya Jaji Bomani ya kuiongezea Serikali mapato ikiwa ni pamoja na kufuta misamaha ya kodi. Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa, haikubaliani na hatua hii ya Serikali ya kuendelea kuyasamehe makampuni ya madini ambayo yanaendelea kusamehewa ushuru wa mafuta, hasa ukizingatia kuwa, makampuni ya nje yananufaika zaidi kuliko ya ndani (ya nje yanalipa US$ 200,000 kwa mwaka yale ya ndani yanalipa kwa lita, hivyo kulipa mara tatu ya haya ya nje).

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa**.** Ni ukweli kuwa, njia ya kuendesha Serikali, ni kutoza ushuru na kodi katika bidhaa, lakini kwa kuangalia hali halisi ya matumizi kwa siku, kwa mujibu kigezo katika taarifa ya utafiti bajeti ya kaya UBK ya mwaka 2007, cha mtu mzima kutumia shilingi 641/- au zaidi kwa siku ukiwa Dar es Salaam, shilingi 532/- au zaidi kwa siku, ukiwa katika miji mingine, bidhaa ambazo kwa asilimia kubwa zinatumiwa na watu wengi ambao kipato chao kwa siku ni chini ya dolla 1 ya Kimarekani kwa mujibu wa kipimo cha Kimataifa. Mwaka jana (2008) ushuru kwa maji na vinywaji baridi uliongezwa kwa Tshs. 54 kwa lita moja. Mwaka huu (2009) ushuru umepanda hadi Tshs. 58 kwa lita. Vinywaji hivi ndio vya watu wa chini na watoto. Ni vyema Serikali ikatafuta eneo lingine kama tulivyopendekeza kwenye bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa. Ushuru wa mazao, ni kero kubwa kwa wakulima, inawapunguzia motisha wakulima, inachochea rushwa ya watendaji wa Vijiji, Kata na Halmashauri. Waziri anapendekeza kupunguza kiwango cha ukomo cha kutoza ushuru wa mazao kutoka asilimia 5 ya bei ya kuuza mazao shambani, hadi asilimia 3 ili kupunguza makali ya athari za msukosuko wa uchumi duniani kwa wakulima nchini. Hata hivyo, inapendekeza hatua hii ianze kutekelezwa mwaka wa fedha 2010/2011, ili kutoa nafasi kwa Serikali za Mitaa kujiandaa kupata vyanzo mbadala vya mapato.

Mheshimiwa Spika**,** Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ifute kabisa ushuru wa mazao hivi sasa na itumie misaada ya mtikisiko wa uchumi, kufidia Halmashauri kwa mwaka mmoja wakati Halmashauri zinajiandaa kutafuta vianzio vingine vya mapato badala yake inafidia madeni ya mabenki na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, tumesikia maelezo ya Serikali juu ya wakulima, ambao "*stimulus package*" haikuwangalia kwa namna ya kuwasaidia. Nchi nyingi Duniani, zimeangalia maeneo yote yaliyoathirika na mtikisiko wa uchumi wakiwemo wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Serikali inaondoa Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula ya mawese (*Crude Palm Oil*) hadi kuwa asilimia 0. Punguzo hili litasababisha wakulima wetu wa alizeti, wakulima wa pamba (mbegu za pamba kwa ajili ya mafuta) na wakulima wa mawese kushindwa kunufaika na kilimo cha mazao hayo. Kambi ya Upinzani inaona, punguzo hili badala ya kuimarisha uchumi binafsi na uchumi wa nchi, litazidi kuharibu uchumi huo na kwenda kinyume na malengo ya MKUKUTA (*Cluster I-Growth and Reduction of Income Poverty*- Ukuaji na kupunguza umaskini wa Kipato). Ni vyema Serikali ikajua uwezo wa viwanda vyetu vinavyozalisha mafuta ya kula na idadi ya mbegu zinazohitajika ili itoe maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika**,** Serikali imekuwa ikikwepa majukumu yake ya msingi kwa wananchi wake, ni jukumu la msingi la Serikali kuhakikisha viwanda vya nguo vinazalisha kwa kiwango kilichokusudiwa. Kitendo cha kupunguza ushuru kwenye nguo za mitumba maana yake ni kuwa Watanzania tuendelee kuvaa nguzo za mitumba wakati pamba tunalima sisi. Hivyo ni kwanini Watanzania wasivae nguo mpya kutokana na Pamba wanayolima? Kambi ya Upinzani inasema kuwa, uamuzi huu si kwa manufaa ya Watanzania, bali ni kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Ni wazi kuwa, Serikali imekubali kutekeleza ushauri wetu wa kupunguza kiwango cha Kodi ya Ongezeko la Thamani, toka 20% hadi 18%, ili kuwa sawa na viwango vinavyotozwa na nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kama inavyosomeka katika kifungu cha 23 cha muswada.

Mheshimiwa spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba, kuweka sheria ambazo ni pana sana sio sababu ya kukusanya pato kubwa, bali upembuzi yakinifu katika kubuni vyanzo vya mapato na utendaji bora wa mamlaka za kukusanya mapato, ndio misingi pekee ya kukusanya mapato stahili na makubwa ya taifa.

Mheshimiwa Spika**,** kuhusu msamaha wa *VAT* kwa wafanyabiashara wakubwa chini ya Sheria ya *Hotels Act, Cap 105, RE. 2002*. Kifungu cha 73A cha Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli, kinatoa msamaha kwa wafanyabiashara wakubwa kwa kusema kuwa Sheria hiyo inatoa msamaha wa kutolipa kodi ya ushuru wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mtu yeyote au Jumuia yoyote ya watu ambao wamesajiliwa chini ya sehemu ya (iv) ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, kuanzia siku ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, msamaha huu ni sawa na kuwapa nafasi wafanyabiashara hawa kutolipa kodi ambayo, kimsingi kila mtu anayeuza bidhaa na kutoa huduma zinazopaswa kulipwa kodi hii, analazimika kuilipa kwa mujibu wa kifungu cha 3(1) na 4(1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, kodi ya ushuru wa hoteli ya asilimia 20%, inayotakiwa kulipwa chini ya kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Ushuru wa Hotel na marekebisho yake ya 1st August,1972, imekuwa kero kubwa hasa kwa wafanyabiashara wadogowadogo katika sehemu tofauti za Miji, Majiji, Manispaa na nyinginezo. Hii ni kwa sababu kiwango cha asilimia 20%, ni kikubwa na hakizingatii gharama za uendeshaji kwa biashara hiyo. Mfano, tarehe 10/01/2008, Umoja wa Wafanyabiashara wa Nyumba za Kulala Wageni Mwanza, (UWANZA), ulimuandikia barua yenye kumbukumbu namba UW/MZ/06, Waziri wa Fedha, wakilalamikia kodi hii na manyanyaso wanayoyapata kwa sababu ya kodi hii. Malalamiko haya, yalijibiwa kwa barua yenye kumbukumbu namba TYC/R/160/32 ya Waziri wa Fedha kwamba, atalishughulikia jambo hili lakini hadi leo hii halijashughulilikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia jambo hili kwa makini na kuchukua hatua zinazofaa, ili kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara hawa. Aidha kifungu hiki cha sheria, kinawaondoka Watanzania wenye mitaji midogo katika biashara na kuwapa fursa wafanyabiashara wakubwa, kuendelea kwenye biashara hii (dhana ya ushindani iko wapi?).

Mheshimiwa Spika, kuhusu Marekebisho ya ada na tozo mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea. Serikali imeamua kupunguza viwango vya ada ya *Visa* na kuwa na kiwango kimoja cha Dola 50, bila ya kuangalia kuwa, wageni wanatoka nchi zipi. Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa, viwango vya *Visa* kwa nchi mbalimbali, ni makubaliano baina ya nchi hizo. Mfano, kama Watanzania wanalipia Euro 100 hadi Euro 150, kwenda nchi mwanachama wa *European Union*, inatakiwa iwe sawasawa na wananchi wao wanaokuja kwetu walipe kiasi hicho hicho. Kinyume na hapo, ni kutokuwatendea haki Watanzania na nchi kwa ujumla.

Aidha, mapato hayo ya *Visa* hutumiwa na Balozi zetu nje ya nchi, Kambi ya Upinzani inahitaji kuambiwa kuwa, badiliko hili litaipunguzia Serikali mapato kiasi gani na Balozi zitafidiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuruni Waheshimiwa wote kwa kunisikiliza, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWANGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA**: Mheshimiwa Spika, najua hivi karibuni, tutaingia katika majadiliano lakini sasa, mabadiliko yaliyomo katika hii *Finance Bill*, ina maana kila Mbunge atafute sheria zaidi ya tano, sita ili kuweza kufuatilia vizuri, hivi haiwezekani kuwekwa pamoja kama ilivyo *Volume II* na *Volume IV* ili wakati wa

kupitisha tuweze kufuatilia kifungu hadi kifungu ili kuweza kuhojiwa vizuri na rekodi ya nyuma ikoje? Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli Muswaada wa Fedha huwa mgumu kwa sababu unahitaji kuangalia sehemu mbalimbali pamoja na Sheria na ndiyo maana tumeweka Makatibu hapa kama unahitaji rejea ya haraka, basi unaweza kusogea kupata msaada. Vinginevyo haiwezekani katika muda mfupi kuchapisha au kuleta vitabu vyote kwa idadi tulivyo kwa ajili ya rejea. Niwakumbushe tu kwamba, hata wanapoweka Mezani kwa mfano, yale yanayoitwa randama, tumeomba ziwekwe nakala 10 ili kuokoa gharama. Kwa mfano, hii ndiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, shughuli ya Jumatatu, wamekwishaleta randama tano hapa, zitawekwa Maktaba na tano zitakuwa kwa Makatibu kwa ajili ya rejea. Yote ni kujaribu tu kuokoa gharama. Kwa hiyo, yeyote ambaye anataka undani zaidi anaweza kuwaona Makatibu Mezani pale na kuweza kupata msaada. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata idadi ya wachangiaji watano, nitawataja majina ili wajiandae. Anaanza Mheshimiwa Dk. Zainab Gama, anafuatiwa Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, halafu Mheshimiwa Pindi Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga, tutahitimisha na Mheshimiwa William Shellukindo. Kwa mpangilio huo, basi sasa namwita Mheshimiwa Dr.Zainab Gama na Mheshimiwa Raphael Chegeni ajiandae.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nami naungana na wenzangu kwanza kabisa, kutoa pole kwa ndugu yetu Mheshimiwa Pascal Degera na Ania Chaurembo, kwa kupoteza wazazi wao. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kabisa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ilijiwekea majukumu na majukumu iliyojiwekea yalikuwa mawili. Jukumu la Kwanza, kujenga misingi ya uchumi ya kisasa ya Taifa linalojitegemea (yaani *modernization* ya uchumi) na la pili, kutekeleza sera za kuwawezesha wananchi kiuchumi. Ninaposema kuwawezesha kiuchumi, leo nataka nizungumzie, asilimia karibu 70 ya wananchi wetu wanategemea Kilimo. Kwa hiyo, hili jukumu la pili, lazima tujitahidi sana sana kuwasaidia wananchi wetu kwenye suala la kilimo.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa ukweli kabisa, kwa mikakati mingi inayofanya, haya majukumu mawili yatekelezeke. Hasa ninapozungumzia jukumu la uchumi kwa wakulima, ukitizama MKUKUTA, ukitazama MKURABITA ambao ni mpango wa kurasimisha mali na hasa ardhi, ili wakulima wetu waweze kupata mikopo ingawa, kwa bahati mbaya sera kama hizi utekelezaji wake unasuasua lakini nia ipo pale. Tumekuwa na kauli mbalimbali za kukionyesha Kilimo ni kitu muhimu sana. Tumesema, Kilimo ni Uti wa Mgongo, tumezungumzia Kilimo juzi tu, tumetoa kauli mbio Kilimo Kwanza, Serikali imeweka mikakati ya kulipa fidia kwa hasara itakayotokea kwa mazao kwa sababu ya suala zima la kuyumba kwa uchumi. Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wetu ametoa msisitizo mkubwa katika suala zima la kilimo kwa kuagiza kwamba, yale Mabilioni ya kifisadi yaliyotoka kwenye *EPA*, yapelekwe kwenye Benki

ya Raslimali (*TIB)* ili lianzishwe dirisha la mikopo la kilimo na pembejeo. Pia tumesimama na tumeng'ang'ana kwamba, hata kama tumeingia kwenye *East African Community,* ardhi yetu itabaki mali ya Serikali kwa faida ya wananchi wa Tanzania na tumekataa kabisa wananchi wa nchi zingine kuchukua ardhi yetu. Hii yote inaonyesha jinsi tunavyowathamini wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, pia imeweka kipaumbele katika matumizi mazima ya pembejeo na hii imefanya msisitizo kwa vitendo kwa kuweka matrekta, siku hizi kuna matrekta madogo, kusudio la kuanzisha benki ya kilimo na mengi mengineyo. Kwa kweli mipango hii na mikakati hii ni mizuri, lakini nina wasiwasi mmoja. Inawezekana kuna baadhi ya Watendaji hawana nia njema na Serikali, wanasema kwa mdomo lakini wanatushawishi tufanye matendo ambayo yatakwenda kinyume na nia hii.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nilipokuwa Bungeni hapa, pamoja na kuwa Mbunge mzoefu na kuona matatizo mbalimbali ya Wabunge wakati tunapitisha sheria, niliomba sana sana, hakuna shule au *profession* ambayo inaitwa Ubunge. Wabunge tunaingia ndani ya Bunge tukiwa na *professions* mbalimbali, ili kuendesha mambo yetu na hoja zinazopita hapa, niliomba tuwe na wataalamu, tupate mchanganuo wa kitaalam, halafu sisi wenyewe tutoe maamuzi, lakini kila nikiinuka nikisema hivyo, wa kwanza, anayepinga hilo ni Serikali. Lakini ukienda Serikalini, Mawaziri wote wana watalaam wa kuwashauri, Marais wetu wana Wataalam wa kuwashauri, lakini sisi hatuna wataalam wa kutushauri. Matokeo yake nini? Matokeo yake, tunapitisha sheria ambazo badala ya kusaidia Mtanzania, zinamkandamiza Mtanzania na si kwa makusudi, ni kwa sababu hatuna wataalam.

Mheshimiwa Spika, mtu unapoumwa homa, unasema jamani nipimwe damu, inaombwa *microscope* itizame damu yangu sio jicho lako, *microscope* itatizama wadudu waliokuwepo pale. Lakini ukikuta mtu anaku-*deny*, usitumie *microscope* kuona wadudu waliokuwepo pale unaambiwa hiyo homa uliyokuwa nayo tibia *Aspirin*, ujue huyo mtu hana nia nzuri na wewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pale inapotokea mara nyingi, tunapoomba na sisi tuwe na watalaamu, tutoe shauri kutokana na ushauri wa kitaalam, wanaweza kutu-*mislead* lakini angalau wao ni watalaam, kuliko hivihivi tu, Dokta amekuja kama Daktari, Engineer amekuja kama *Engineer* , unless suala la *engineering*, *unless* suala la udaktari, mtu anaweza kusahau, lakini kuna masuala mengine magumu.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano, ndugu zangu wote tulisimama hapa na namshukuru Mwenyekiti wa Kamati husika amelitaja, tumelalamika sana kwenye kuweka *zero percent* kwenye suala zima la *crude oil* ya mafuta ya kupikia, na-*underline*, mafuta ya kupikia, tumelalamika, tumesema, lakini wakati tuna-*wind up*, Waziri hakusikiliza, aliweka *deaf ear.*

Mheshimiwa Spika, wakulima kwa sababu hawana *mandate* kama walivyo Mapadre na Mashehe, wameshindwa kutekelezewa matakwa yao. Mapdre na Mashehe

kwa sababu ni viongozi wetu, waliweza kumwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, njoo wewe muumini wetu wewe, kwa nini unataka kufanya hivi? Kweli kuogopa laana ya hawa waumini wetu, tulibadilisha lakini kwa bahati mbaya, hatujui kama tuna laana ya wakulima. (*Makofi*/*Vicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme mfano huu, inaonekana jinsi nilivyokuwa sifuatilii sheria na naomba huu uwe ni mfano kwa Wabunge. Jana nimetoka hapa, nikamfuata Waziri Mkuu, nikamwambia, Waziri, mbona sikusikia umerudisha ile kodi ya asilimia 10? Akaniambia, bwana hii ni miezi sita tu, aah, lakini namjua Mkulo, sikutaka kugombana naye, nikawafuata Manaibu Waziri, nikasema Naibu Waziri, mimi bwana nimeamua kabisa nafanya *amendment*, Mawaziri hawa wazuri sana. Manaibu Waziri naomba niwashukuru sana, Manaibu Waziri wa Fedha wakanijibu *politely* na sisi tunakwenda kwenye kikao chetu kuonyesha *our concern* kuhusu suala hili, namimi nikaona vizuri nikatoka. Sasa tafuta ile Sheria ya *Finance Bill*, tafuta hicho kipengele, hakuna. Nikasema, kama kipengele hiki hakuna, Waziri anakuwa na *mandate* gani kuondoa? Lakini, nikaja kugundua kitu kimoja na ndio nasema jamani, tusikubali kukaa kupitisha jambo ndani ya Bunge, bila watalaam.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya *East African Community Custom Management Act* ya 2004, kipengele Namba 140, sisi wenyewe Wabunge, tumempa *power* an *individual person*, kufanya mabadiliko hata kama yanaathiri nchi. Kipengele hicho, pamoja na kipengele Na. 19 na Na.71, ku-*ammend Schedule*, yaani *the Power* of *the Council to amend schedules, schedule no. 2, schedule no.3* na kuondoa *duties* kwa faida ya *East Africa*. Mtu mmoja anakaa na Mawaziri wenzie huko anatoa maamuzi hata kama yanaathari ndani ya nchi yetu, lakini tumempa *power, go.*

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza mimi, *power* hiyo amepewa na kwa sababu tulinyimwa kuwa na *microscopic eyes*, lakini Mawaziri wenzie walikuweko na malalamiko haya tuliyatoa tukasema inavyoathiri wakulima wetu wanaolima mazao haya ya mbegu za mafuta, Mawaziri wenzie wakaendelea kukataa kuweka *zero percent*, waliendelea, Waziri wa mwisho namjua, Dada yangu Zakia Meghji, aliendelea kukataa. Yeye mwenyewe mwaka jana alikutana na wakulima, wakati akiandaa bajeti ya mwaka 2008/2009, wakamlalamikia, walipinga suala la ushuru wa malighafi ya mafuta kuwekwa *zero percent*, alikubaliana, lakini leo alikaa na Mawaziri wenzie wa *East Africa* eti kwa sababu *East Africa* isivunjike, amesahau kwamba, sehemu kubwa ya wakulima wa Alizeti, wa Ufuta na mbegu zingine za mafuta, sisi ndio tunazalisha sana kuliko wenzetu! Alisahau kwamba, wenzetu wanatumia hayo mafuta anayoita malighafi sana kuliko sisi, alisahau, akatumia nafasi hiyo, samahani sana Kaka yangu Mkulo, kachukua nafasi hiyo kwa kutumia udhaifu wetu wa kutokuwa na *microscopic eyes*, kuwa na watalaamu wa kutizama sheria zetu akapitisha.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bahati mbaya, wakulima hawa hawana nguvu kama Mashehe na Mapadre na Maaskofu, kuweza kubadilisha, imebaki palepale. Inasikitisha sana nia yote nzuri, sera yote nzuri ya Chama cha Mapinduzi, inafanyiwa hujuma na baadhi ya watendaji na mimi sina hujuma na baadhi ya watendaji kwa sababu nikisema Mbunge, Mkulo ni sawasawa na mimi, anapoletewa sheria, hatokuwa na macho

kama walivyokuwa nayo watendaji, kwa hiyo walipotuletea sheria hii na wakatuondelea tusiwe na watalaam, kwa hiyo na Mkulo naye akaingia kwenye *line*. Inanisikitisha sana, je, itapofikia sasa wakulima wetu hawa bei zao zitashuka kutokana na suala hili, ule utaratibu tulioambiwa na Rais JK, watafidiwa au ni viwanda tu?  Naomba niulize swali hilo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wabunge katika kubishana katika suala hili, walipata nafasi kwenda Malaysia na Indonesia, walichokigundua ni nini? Malaysia na Indonesia, wanasema hivi, mfanyabiashara yeyote anayetaka kupeleka malighafi nje, wanamtoza ushuru mkubwa kwa sababu ya kulinda viwanda vyao vya ndani, ili wawe na *Value Added* lakini sisi tunasema hapana.  Kama sisi tunaondoa kodi kwenye malighafi ya mafuta ya kupikia, kwa nini tusitoe na ile ya viwanda vya sabuni? Viwanda vya sabuni sasa hivi vyote vimekufa, kwa nini tusiondoe ushuru katika viwanda vyetu vinavyotengeneza mafuta? Vinakufa, jamani mnajua Wabunge wengi tuna *Cholesterol* nyingi? Mafuta haya yanayotoka nje ni *Choleserol* tupu, mafuta mazuri ni yetu ya Alizeti na mengine. Tunashindwa kununua kwa sababu ni gharama, kwa sababu ya kutokusamehewa kodi. Kwa kufanya hivyo, mmewatendea haki Watanzania wakulima?

Mheshimiwa Spika, nazungumza kwa uchungu sana, utanisamehi kaka yangu Mkulo na kwa bahati mbaya nimeshindwa kufanya *amendment* kwa sababu tumemruhusu Mkulo *as individual* asiweze kwenda *East Africa*, asiweze kuingia ndani ya Bunge la Taifa letu tukaamua mazuri na mabaya tukamwambia *go ahead*.  Kwa hiyo, hata siku anaweza kusema kwa sababu ya uzuri wa *East Africa* kwa hiyo hii nchi tunaiuza, inawezekana!  Tumempa *power*, tunauza mambo yote haya apeleke *Custom Union.*  Kwa kweli najilaumu mim lakinii tujilaumu na Wabunge wote *seniors* tukiwaacha wale wageni, tulikuwa tunalalamika tupewe macho lakini kila tukisema tunanyimwa macho matokeo nimeshindwa kufanya *amendment*, ndugu zangu inasikitisha sana. Tunataka tuwasaidie wakulima wetu lakini tunaweka sheria *which is contradicting* ya kufanya wakulima waendelee kuathirika kwa kulinda viwanda viwili vitatu. Viwanda vingi vya sabuni vimeshindwa kupewa na wao hiyo inayozungumziwa malighafi, inasikitishwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema nimesikitishwa sana sana na tumeshindwa kufanya *amendment* lakini nataka kumwambia kaka yangu Mkulo, kauli hii naitoa, wakulima wa Tanzania wanaisikia, wakulima wa Jimboni kwa Mheshimiwa Mkulo wanasikia kwamba Mawaziri wenzie walikataa yeye peke yake ndiyo alikubali. Wanamsikia kama kuna wakulima wa alizeti huko kwenye Jimbo lake basi ajue wamesalitika.  Kama wakulima wengine wajue Wabunge tumeshindwa kutazama na *microscope* kuona *the invisible organism* ambayo huwezi kuona kwa macho ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba nikae chini lakini naomba kuzungumza kwa uchungu sana. Kila siku nasema *APNAC* inang'ang'aniza, ndani ya sheria nyingi hapa kuna *loop hole* ya rushwa.  Suala hili kama Mawaziri wengine walikataa ni sababu zipi zilizomfanya Waziri huyu akubali.  Hii ni *loop hole* na sio kwa ajili ya yeye kwa sababu ya watalaam wake wamempangia kitu, kwa sababu yeye si mtaalamu wa kila kitu.  Tuwe waangalifu ndugu zangu, *APNAC* iling'ang'ania *Public Hearing*, ilikataliwa na wengine

tulinyanyaswa lakini mwisho wa siku sasa hivi tuna-*enjoy Public Hearing* kupitia *APNAC*, naomba niwaarifu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna mambo mengine ndugu zangu kwa *interest* ya wapiga kura wetu na ukikuta mtu anasema *three line whip* kwa ajili ya kumnyanyasa mpiga kura, ujue huyo ndiyo adui wa mpiga kura na ndio adui wa chama husika. Chama cha Mapinduzi, Rais wetu ana moyo mzuri anawapenda, kwanza si rahisi anayetaka mihelahela sijui ya kununulia nini, *no, no,* ni Rais ambaye anapenda wananchi wake lakini wataalam wake wanamsaliti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ninakaa chini lakini kwa masikitiko kabisa leo nilitakiwa kufanya *amendment* na nilifanya *lobbing* kubwa kwa Wabunge wote kama hiki kifungu kingekuwepo leo wote wangeinuka kupiga kura kukataa. Lakini kwa kutokuwa na *microscopic eye* na kukubali ushauri wao sisi tusiwe na *microscopic eye* hili ndilo limetokea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Muswada huu wa Fedha.

Kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na timu yake yote kwa kuweza kuandaa bajeti ambayo kwa kweli niseme tu kwamba kwa kiwango kikubwa imejaribu kukidhi yale ambayo tunapaswa kupambana nayo katika kipindi hiki na hasa cha mtikisiko wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, pengine si rahisi kwa haraka haraka mtu kuweza kuyaona haya yote kwa jicho moja yahitaji kidogo kuwa na macho kama ya chandarua ili uweze kuona kwa upana zaidi.

Napenda nirejee katika sehemu ya 5 ya Muswada huu, aya ya 5 ambayo narejea vile vile kitu ambacho Mheshimiwa Rais wetu alikigusia kwa upana mkubwa sana wakati akitoa hotuba yake juu ya *Rescue Package* pamoja na *Stimulus Package* ambayo alituhutubia hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alisema kwamba zaidi ya shilingi bilioni 21.9 zitatumika kwa ajili ya kukwamua na hasa wafanyabiashara wa pamba ambao wamepata hasara kwa sababu ya kushuka kwa bei ya pamba katika soko la dunia. Ebu tujiridhishe kidogo, tumekuwa na mazoea sana ya kuuza pamba yetu ikiwa pamba ghafi. Kwa mfano, mwaka jana tuliuza zaidi ya marobota 600,000 ambapo kati yake ni marobota 120,000 peke yake yaliyosindikwa katika kiwango cha kuweza kuuzwa kama malighafi iliyoongezwa thamani (*Value Added*) na hii ni kama asilimia 20 tu ya kilimo au ya pamba ambayo ilipatikana sehemu kubwa tukauza kama malighafi. Sasa hii ukiizungumzia mkakati wa kilimo kwanza, ni *theory* ambayo huwezi ukai-*match* kwa sababu leo hii soko la dunia kila wakati linabadilika na bei za mazao yetu na hasa haya asilia inazidi kupanda na kushuka, inapanda inashuka, inapanda inashuka. Sasa kuna

wakati mkulima inapokuwa imeshuka na yeye itafika mahali anashindwa kuhimili kulima mazao haya.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivyo kwa sababu gani, kwa sababu Wizara ya Kilimo tumeipa jukumu kubwa sana inahitaji tuipe *support* kubwa sana kwa maana ya kwamba *support* ya kimatendo sisi kama wanasiasa, sisi kama viongozi na iwe *support* ya kuwaimarisha wakulima wetu ili waweze kulima kilimo bora zaidi. Lengo la Serikali yetu daima ni kujaribu kumuondolea umaskini Mtanzania na hasa mkulima. Sasa tunapokuwa tunasema mkulima anapolima zao la pamba anauza pamba ghafi ile pamba inapaswa kuchambuliwa na kupata pamba ambayo inakuwa imekuwa *ginned* kwenye maroboto na baadaye inasokotwa kupata nyuzi, nyuzi ukiuza inakuwa na thamani kubwa zaidi kuliko inavyouza pamba ambayo ni ghafi, sasa itabidi tuangalie katika mchakato wote huu ni kwa namna gani itamsaidia mkulima aondokane na kuuza pamba yake ikiwa ghafi. Mimi nimeona hapa katika Muswada huu kuna lile suala la kuruhusu zile nyuzi za aina *ya polyester* kwamba ziingie hapa nchini bila ya kuwa na kodi au kwa kodi ndogo. Hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba sasa tunasema kwamba nyuzi zetu za pamba hazitaweza kupatikana kwa urahisi zaidi na hakutakuwa na *value* kubwa zaidi. Sasa tukienda kwa mtazamo huu hatumsaidii mkulima.

Mimi ningeshauri ili tuweze kumsaidia mkulima wa pamba ambaye akilima pamba atapata mashudu, atapata pamba yenyewe, atapata nguo watu watavaa nguo badala ya kuvaa mitumba, dada yangu hapa Mheshimiwa Sakaya amesema kwamba Watanzania tumezoea kuvaa mitumba tuvae nguo ambayo inatokana na pamba yetu hapa. Sasa hatuwezi kuvaa nguo inayotokana na pamba kama hatuwezi ku-*add value* na kupunguza kodi au kuzuia vitu ambavyo vinachangia kupunguza bei ya pamba yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa haraka haraka namna gani nchi hii tunaweza kuondokana na hadithi, kwa sababu sisi Watanzania wazuri sana kwa kupanga, kila wakati tunapenda kupanga lakini tunashindwa kutekeleza. Ninaomba kupitia bajeti hii, tuite bajeti ya Kimapinduzi kwamba sasa impindue Mtanzania ili atokane na kilimo chake duni iwe ni kilimo ambacho inaweza kuzalisha zaidi na kuweza kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, leo hii Serikali yetu inasema kwamba tunasamehe ushuru wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye pembejeo za kilimo. Mimi nashukuru kabisa na naomba huu mkakati uendelee vizuri kwa sababu utaongeza tija kwa uzalishaji wa mazao yetu, mazao ambayo tunahitaji tuyauze na tupate fedha, lakini tujichochee zaidi katika kuongeza thamani kwa mazao yetu. Tuondokane na kuuza mazao ghafi nje ya nchi. Kwa sababu leo hii unapouza mazao ghafi inakubidi sasa wewe utumie tena fedha zako za nje kuagiza malighafi zingine. Lakini tunapo-*add value,* tunaongeza ajira kwa wananchi wetu lakini pili tunaongeza pato la mwananchi vile vile hii ni njia ambayo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* Muswada huu, afikirie sana hili suala la kuruhusu *polyester*, ukiruhusu *polyester* ikiingia hapa nchini itaua zaidi zao la pamba, haitamsaidia mkulima. Lakini pili wafanyabiashara ambao wanafanya kazi hizi wenye viwanda na vinu vya kusindika pamba, watashindwa

kufanya kazi vizuri zaidi. Leo hizi bilioni 21.9 tungekuwa tume-*add value* pengine tusingefikia kuweza kufidia kwa kiwango hiki kwa sababu tulikuwa tunauza bidhaa ambayo imekuwa *added value* badala ya kuuza bidhaa ambayo ghafi ambayo haina thamani kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili ukirejea kwamba Tanzania ni nchi ya pili katika Afrika kwa uzalishaji wa pamba ni sifa moja kubwa sana. Tanzania tuna kila kitu ambapo, ni watu wa pili. Madini ni watu wa pili kwa Afrika, sasa tunajaliwa vitu ambavyo tunahitaji kweli tuvitumie kwa ajili ya kuongeza uchumi wa nchi hii na nina imani kwamba hata bajeti ya mwaka kesho Mheshimiwa Waziri angejiandaa kwamba tuondokane na suala la kuwa tegemezi. Ebu tutafute namna ya kuweza kutumia mapato yetu ya ndani na vyanzo mbalimbali vya ndani kuweza kuchochea bajeti yetu ijitegemee zaidi badala ya kuwa tegemezi kwa sababu siku zote ombaomba ni mtu ambaye unakuwa huna uhuru. Uhuru wa kuombaomba unakufanya ushindwe kufanya maamuzi mengine kwa maslahi ambayo unadhani ni muhimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze katika suala zima la kilimo cha pamba na hasa kwa wakulima wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mashariki. Leo hii bei ya pamba inashuka, mwaka jana ilikuwa shilingi 400/= mpaka 500/= kwa kilo moja, mwaka huu hatujajua bei itakuwa shilingi ngapi, lakini ni namna gani itamsaidia mkulima huyu kumhakikishia kwamba walau aweze kupata bei ambayo itampa tija ili mwaka kesho aweze kulima tena? Kwa sababu naogopa kwamba itafika mahali wakulima watashindwa kulima pamba na hili ni tatizo kubwa sana na ukizingatia hoja kubwa katika nchi yetu ni kwamba hivi tukiruhusu bidhaa ambazo zinaua mali zetu hapa sisi wenyewe tunajenga uchumi kweli au tunabomoa uchumi? Lengo la Serikali yetu ni maisha bora kwa kila Mtanzania. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ajikite pale tu kwamba ni namna gani tutaweza kupitia Muswada huu kudhibiti bidhaa ambazo zitakuwa ni *competitor* wa zao letu la muhimu sana pamba ili liweze kustahimili na kustawi zaidi kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja ambalo nadhani Mheshimiwa hajaligusia katika bajeti yake nalo ni suala la hizi *Bureau De Change*. Ni Tanzania peke yake ukiacha nchi nyingi mtu anaweza kuingia na aka-*transact* kwa fedha yoyote ya kigeni bila ya kuwa na *restriction* yoyote ile. Lakini jamani ukienda nchi zingine huwezi ukaruhusiwa ku-*transact* kwa fedha nyingine zaidi ya fedha ya nchi ile. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie namna gani tuta-*control Bureau De Change*, haya maduka ya kubadilishia fedha za kigeni kwa sababu ni moja ya njia ambayo inasababisha fedha nyingi inatoka nje ya nchi bila kujua, lakini pili vile vile hatuwezi hata ku-*monitor* fedha zote ambazo zimeingia nchini kwa sababu fedha zinaingia na kutoka kama ambavyo watu wanavyotaka. Ninaomba hii sheria vile vile ijaribu kugusia sana kwa sababu ni moja ya vyanzo ambavyo hata fedha nyingi ya *EPA* ukiangalia ilitoroshwa kwa njia ya maduka kama haya. Watu walikuwa wanachukua fedha za madafu wanakwenda kwenye *Bureau* wanapata fedha za kigeni wanatorosha nje ya nchi, lakini tukiwa na *proper system* itatusaidia sana kuweza kuwa na *control*.

Mheshimiwa Spika, siku hizi unakwenda kwenye maduka ya *Bureau* hawakuulizi kwamba wewe una kitambulisho gani, wala sijui kama una Pasipoti, hata kama kuna *control* yoyote hakuna na sijui Benki Kuu wanafanya kazi gani katika suala hili. Kwa sababu suala zima lazima tulikazanie, tusipoweka msisitizo, kwa kweli tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe ni msikivu, ni kaka yangu na bahati nzuri ni mjukuu wa Wasukuma, Wasukuma wakulima wa pamba kule wamekusikia sijui kama utawaangusha, ukiwaangusha sasa sijui maana wakiamua kukuita nyumbani watakwenda kukuhoji kidogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda nikushukuru sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono Muswada huu.

Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri na timu yake ya Manaibu wawili na nimpongeze pia Kiongozi wa Serikali kwa bajeti nzuri ambayo kimsingi imepita jana kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya ya kuipeleka ile meli yetu kwenye ile nchi ya ahadi yenye wingi wa asali na maziwa.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye Muswada, pale kifungu cha 5 ukurasa wa 10, nichukue nafasi hii kupongeza sana maboresho mengi ambayo yamekuwa yakifanyika ya kuboresha vyanzo vya mapato maeneo mbalimbali. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa na Wilaya zake zote 7 kitendo cha kupunguza ushuru wa mazao kutoka asilimia 5 mpaka asilimia 3, kwa kweli tunawapongeza sana Serikali. Ninakubaliana kabisa kwamba ipo haja ya kupunguza na kama wananchi kwa kweli wanapaswa kuchangia na suala la kuchangia lipo maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hawa wa mazao wakati mwingine wanatokea nchi za jirani. Kwa kule Iringa wengine wanakuja Ludewa kwetu kununua mahindi wanatokea Malawi, Zambia na kadhalika, wanatumia magari, miundombinu ya kwetu barabara, kwa hiyo wanapolipa ushuru wa asilimia 3 kwenye mazao ni sahihi kabisa. Ila tu naomba ombi kwa Serikali kutafsiri neno ambalo limetumika pale wamesema ni asilimia 3 ya neno *farm get price*. Sasa hivi ni wakati wa soko huria, hasa hii *farm get price*, tutaitambuaje wakati huu wa soko huria? Kwa hiyo, hili nilidhani ni la msingi sana tuone tunalitafakari vipi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo wakati mwingine wananchi wananunua mazao kwa ajili ya lengo la chakula si kwa ajili ya biashara. Basi wanaponunua mazao kwa ajili ya kula kama mahindi gunia moja kiroba basi wanapopita katika maeneo ya makusanyo kama kwenye mageti mbalimbali katika Mikoa mbalimbali basi watu kama hawa si vyema sana kuwatoza. Ni vyema tukiwatoza wale ambao wanajaza Ma-*fuso, Scania* kwa lengo la biashara, lakini kwa wananchi wetu wanaponunua mazao kwa lengo la chakula au kwenye gulio, ni bora kabisa tukajaribu kutafakari ni jinsi gani tunawasaidia kwa sababu ni kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chakula.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Mkoa Iringa licha ya kwamba tumesema "kilimo kwanza" sisi Iringa tunasema "Siasa ni Kilimo" na mwaka huu tunaishukuru sana Serikali kwa kutusaidia pembejeo ikiwa ni pamoja na mbolea za vocha na tumeahidiwa kwamba kipindi kijacho vocha zile zitaongezeka na tunawaahidi kabisa kwamba tutakapopata vocha hizo za kilimo cha mbolea, hakika watu wa Iringa tutalima sana na Mikoa mingine ambayo itakuwa ina njaa tuseme karibuni sana Mkoa wa Iringa mahindi yapo.

Mheshimiwa Spika, jambo dogo tu ambalo ninapenda ku-*share* uzoefu ni pale katika Muswada huu lilipotumika neno "*Electronic Document*, hili jambo jema sana. Katika sheria nyingi ambazo tumezifanyia maboresho hapa tumesema zitatumia *Electronic Document*, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sheria ya Tozo za Huduma zote hizo tutaanza kutambua *Electronic Document*. Ombi langu katika Muswada huu, hizo *Document* za *Electronic* tutoe tafsiri, tunamaanisha ni *document* gani? Kwa mfano, mtu ukitumia *document* ambayo imetokana na kuwa *scanned,* umetumia *document* ambayo ume-*print* kwenye *e-mail* na mambo kama hayo, je, hizo nazo ni *document* za ki-electroniki. Lakini niipongeze sana kwa sababu wanasema "muda ni fedha" kwa lugha ya Kiingereza wanasema "*Time is money*". Sasa kama huko nyuma ilikuwa unatafuta *document original* tusafiri kutoka Ludewa, Njombe tuje tulete, muda wa usafiri ni gharama kubwa sana. Kwa kuwa Serikali imesema kwamba itaanza kuleta utaratibu wa *E-government document*, hizi zitaokoa sana na uchumi wetu utapanda sana. Kwa hiyo, niwapongeze sana kwa utaratibu huu. Utaratibu huu wa *electronic document* siku za huko nyuma ulikuwa unatumika katika *International Trade Law*. Sasa kwa kuwa tumekubaliana kwamba wakati mwingine hata katika maeneo ya vyombo vya kisheria kama Mahakamani tutambua hizi *electronic document* kama ni sehemu ya ushahidi, hapo ndipo ninapenda kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mawazo hayo mazuri, kwanza ipo haja ya kurekebisha ile Sheria ya masuala ya Ushahidi ya Mahakamani ili iweze kukidhi azma hii kwamba *document* zile, kunapokuwa na migogoro, zinaweza zikatumika Mahakamani ambazo zimetokana na electroniki. Kwa hiyo, ile Sheria ya *The Law of Evidence,* ni lazima irekebishwe kukidhi haja ya *electronic document*.

Mheshimiwa Spika, lakini zile *document* ambazo ni *electronic,* ipo haja ya kuzipa vigezo zaidi kwa sababu tunalinda vipi *corruption of computer*? Ni rahisi sana mtu ku-*forge* sehemu ilipoandikwa namba mbili anaandika namba 8 ana-*print.* Sasa mambo kama haya sisi kama Taifa ni lazima tuwe makini sana. Nchi ya Uingereza wameleta masuala haya ya *electronic document* si muda mrefu sana mwaka 1995 katika sheria zao za nyuma kwa mfano *Law of Evidence* yao ya mwaka 1968 walikuwa hawana masuala haya ni mpaka hivi karibuni wameboresha na imewasaidia. Lakini ipo haja ya kuweka *security* katika utaratibu huu wa kutumia *document* hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunaweza tukasema tutumie *document* ambayo ni *electronic* lakini labda iwe imethibitishwa na Afisa anayetambulika katika Idara inayohusika kwamba hiyo ni *document* halali labda kwa kuweka saini ya Mkurugenzi. Kwa hiyo, si tu kila *electronic document* itumike katika kufanya mabadilishano ya

kibiashara. Sasa hivi kuna masuala ya utandawazi, kuna makontena yanakuja, sasa hizi *document* lazima ziwe *classified* ili kuweza kutunza na kuhakikisha usalama, kwa sababu maendeleo sasa hivi yanakwenda kwa kasi sana. Kwa hiyo, masuala haya lazima tuyawekee vigezo kuwalinda watu wetu na masuala kama ya *forgery* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati mwingine inawezekana mtu aka-*mis-use computer*. Katika baadhi ya nchi hizo, *electronic document* wanasema kabisa ni zile ambazo zimetokana na *computer* fulani au na *program* fulani sio *document* yoyote inaweza ikatumika katika kufanya mabadilishano ya shughuli mbalimbali. Huo ndio ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaweza tukaangalia *Convention on Sober Crime* kama nchi ili tuweze kujiunga na mikataba hiyo ya Kimataifa kwa sababu unapokubali kutumia *electronic document* kwa mfano unaingiza magari kutoka Dubai basi wewe Tanzania na nchi ya Dubai lazima muwe na mahusiano ya karibu sana ili kuhoji je, hiyo *document* ya *electronic* ni halali? Kama kuna tatizo, wale wanaweza wakawapa *support* kuwadhihirishia kwamba *document* zetu zipo namna hii. Kwa hiyo, nilidhani maeneo hayo ni muhimu sana yakazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ninaomba pia kushauri Sheria yetu ya Makosa ya Jinai (*Tanzania Civil Procedure Code)*, bado haijatambua makosa yanayotokana na ku-*forge* hizi *electronic document*. Kwa hiyo, sambamba na hiyo pamoja na marekebisho ambayo nimeshauri ya *The Law of Evidence Act*, ni vyema basi wataalam wakaangalia sheria hizi ili kuweza kukidhi matumizi haya ya *document* hizi na pale mtu anapokuwa ana-*forge* ijulikane kwamba ni kosa na kwa kuwa itakuwa ni kosa basi atawajibika kisheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, kwa kweli kwa mara nyingine, ninaipongeza sana Serikali hususan Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa maboresho haya na Muswada huu, ninauunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada wa Fedha ulio mbele yetu.

Baada ya shukrani hizo, niseme tu kwamba na mimi ni mjumbe katika Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, kwa hiyo baadhi ya maoni yangu yamo katika maoni yaliyotolewa na Mwenyekiti wangu. Nimesimama hapa kuongezea tu yale ambayo kwa bahati mbaya, hayakuonekana kwenye hotuba ya Mwenyekiti wangu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa maelekezo yako uliyoyatoa kabla ya mjadala huu kwamba ulikubali kabisa kwamba ipo sheria inayoiruhusu Serikali kuanza kukusanya mapato yake hata kabla ya Muswada huu kupita. Kwa hiyo, tungeweza tukauacha huu Muswada tukauzungumza mwisho kama ilivyokuwa huko zamani, lakini kwa sababu ambazo Mheshimiwa Spika umesema, ni vizuri tukafanya mabadiliko ya utaratibu. Kwa hiyo, tumefanya mabadiliko haya lakini niliomba tu kwamba ili tusije tukawa tunazigonganisha sheria zetu na taratibu zetu basi hii Sheria ya

*Provisional Revenue Collection Act* ya mwaka 1963 iweze kufanyiwa mapitio ya haraka ili iendane na wakati. Kwa sababu sasa hivi tunafanya kitu kimoja na sheria ipo lakini kwa mantiki ambayo umekwishaielezea na mimi nakubaliana nayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, niende moja kwa moja kwenye suala zima la kwa nini kodi na ushuru, ziko sababu nyingi lakini nitajikita kwenye sababu mbili kubwa. Ya kwanza, ni kuiwezesha Serikali kupata mapato yake lakini ya pili, Serikali inatumia masuala ya ushuru na kodi kuweza kujenga mazingira ya kuendeleza uchumi wake kwa njia ya kulinda viwanda vyake.

Hapa nataka kusisitiza yale ambayo baadhi ya wenzangu wamekwishayasema, nichukulie tu viwanda vya nguo. Viwanda vya nguo usipoviwekea utaratibu wa kuvilinda kwa kutumia njia ya ushuru hususan wa nguo au vinavyotengeneza nguo kama nyuzi vinavyotoka nje, utaviua. Kwa hiyo, huu ushuru wa *synthetic* ambao unaondolewa, nasisitiza hasara yake ni kuua viwanda vyetu vya pamba.

Mheshimiwa Spika, tayari kule Tabora tuna kiwanda na ndio kiwanda pekee mjini Tabora cha Kusokota Nyuzi kutokana na pamba, kimekwishaanza kuonja joto la jiwe kabla ya huu ushuru haujaondolewa kwenye *synthetic yarn* sasa kuondoa ushuru kwenye *synthetic yarn* ni kama tunaongeza msumari mwingine kwenye jeneza la kile kiwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nilikuwa nimezungumzia jambo hili katika mchango wangu kwenye bajeti. Matarajio yangu ni kwamba wenzangu au wenzetu katika Wizara ya Fedha na Uchumi, wangelielewa na katika mapendekezo haya wangeliweka kwamba tumeafiki kuondoa ushuru kwenye *synthetic yarn* kwa sababu ni kitendo kitachoua viwanda vyetu, kwa hiyo, tunaondokana na hili pendekezo, lakini badala yake wamezidi tu kulileta. Kwa hiyo, liko mbele yetu ili tulipitishe maana yake tupitishe, tuhalalishe, kuwa viwanda vyetu vinavyosokota nyuzi za pamba vife, inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, la pili, jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipokua anajibu kuhusu namna Serikali iatakavyopata fedha zake, katika ufafanuzi uliotolewa ni pamoja na kwamba ipo sehemu ya takriban shilingi 300 bilioni zitakopwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Katika lugha ya kawaida mtu akisikia mkopo anaona kama ni mkopo ni kama vile mtu unavyokwenda *NBC, CRDB* ukakopa lakini mkopo wa Benki wa Kuu ni tofauti. Serikali kukopa Benki Kuu kwa lugha sahihi ni Serikali kuiruhusu Benki Kuu ichapishe noti mpya iingeze kwenye uchumi, hiyo ndiyo lugha sahihi, tutairuhusu Benku Kuu ichapishe fedha iziingize kwenye mzunguko. Lakini kukopa si vibaya, Serikali ingeweza kukopa kutokana na pesa ambazo tayari ziko ndani ya mzunguko, hizo hazina athari kwa kutumia taratibu zake za dhamana za Serikali za muda mfupi na za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini nalizungumzia suala hili? Nalizungumzia hili ili nilite suala la kodi katika sekta ya madini. Kama tungeweza kupashika pale vizuri, tusingekwenda kukopa ndiyo hoja yangu. Kwa hiyo, tungeunusuru uchumi huu kutokana na kasi ya kupanda kwa mfumuko wa bei kwa kuchapisha pesa mpya wakati pesa ambazo tungeweza kuzipata kihalali kutoka kwenye makampuni ya madini tunaziacha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, nizungumzie suala la ushuru katika mafuta ghafi. Mimi nilipata maelezo na niliridhia kwa shingo upande kwamba tatizo letu kubwa ni kuwa ndani ya soko la Afrika ya Mashariki kwamba wenzetu wa Kenya na Uganda wao ni *zero rate* na kwa sababu chini ya utaratibu wa Ushuru wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, mkishakua kwenye *Customs Union*, biashara zenu za ndani ni *zero rated.* Kwa hiyo, sisi tukiendelea kukataa kwetu kutakua *defeated on that ground*, nakubali.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nisisitize suala zima la kulinda viwanda vyetu na hapa suala la kulinda viwanda vyetu, ni suala la kufa na kupona. Ndiyo sera nzuri ya uchumi. Uchumi mzuri ni uchumi ambao una maingiliano ya mbele ambayo tunasema *forward and backward linkages*. Uchumi mzuri ni ule ambao ndani yake kuna *forward na backward linkages*. Sasa leo sisi *forward linkages* za zao letu la pamba ni nje badala ya kulifanya hapa ndani. Halafu *backward linkage* yake badala ya kuwa ni wakulima wetu inakua ni wakulima wa Malaysia yaani wakulima wa Malaysia walime zile mbegu halafu watuletee sisi ndiyo tu-*process* badala ya kutumia mbegu za wakulima wetu ku-*process*. Ni aina gani ya uchumi hii?

Mheshimiwa Spika, sasa suala ni kwamba kama mbegu hazitoshi, mimi nilitarajia hao wenye viwanda vya mafuta wangepewa nafasi ya kwanza ya kuwa na ardhi kubwa ya kulima mbegu zao wenyewe kama mbegu za Watanzania wenzetu hazitoshi walime wao wenyewe. Kama watu wa Malaysia wanaweza kulima mbegu mpaka wakatuletea sisi kwanini sisi tusilime tukawapelekea watu wa Malaysia? Ni kitendawili, ardhi tunayo, maji tunayo, watu tunao kwa nini tusifanye hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la hizi nyuzi bandia halitoua halitaleta matatizo au madhara kwenye viwanda vya pamba peke yake bali vitaathiri na sekta yetu ya katani. Hizi nyuzi za bandia ndizo hutumika kufungia mitumba ya majani ambayo yanalishwa ng'ombe. Utafiti umeonesha na imethibitishwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ananitazama, ng'ombe akila ile kamba, anakufa lakini ng'ombe akila kamba ya katani iliyofunga mtumba wa majani inakua haina madhara. *Product* za nylon ni *unfriendly* kwenye mazingira. Sisi tunazileta tena tunazipunguzia na ushuru kwa maana kwamba tunaziona ni *friendly* kwenye mazingira? Sasa ninachotaka kusisitiza hapa kama utaratibu wetu wa kuzungumza humu ndani ya Bunge, tukatoa hoja Serikali ikasikia, hili si lilikwishazungumzwa, sasa mbona tena linarudi? *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, *Air Charter Services*, limeondolewa msamaha wa kodi, tatizo hapa ni kwamba *Air Charter Services* ni akina nani wanao-*charter*? Hii ni sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo tunapoondoa hizi *incentive* tujitazame na jirani zetu wanasema nini. Tukifanya *service* hii kuwa ghali Tanzania watakwenda kukodi Kenya na watakuja tu Tanzania na hizo ndege ambazo wata-*charter* Kenya. Kwa hiyo na hili nalo tulitazame wenzetu wa Kenya wanafanyaje maana tusifanye mambo kana kwamba tupo kisiwani. *We are part of the East Africa* kama ni *charter services* ziko zaidi Kenya kuliko Tanzania. Kwa nini tunaondoa ule msamaha wa ushuru na katika hali ambayo tuna mtikisiko wa uchumi na sekta moja iliyoathirika ni sekta ya utalii. Sasa tunaisaidiaje

sekta ya utalii kwa kuondoa *incentive* ambayo ingefanya *services* za *air charter* ziwe *cheaper and therefore competitive*?

Mheshimiwa Spika, hili suala la soko la Afrika Mashariki, suala la msingi la kujiuliza tuko tayari kweli kuwa katika soko la Afrika Mashariki? Tunapokwenda kwenye mazungumzo tuelewe tunakwenda kule kama Watanzania milioni 44 bila Watanzania milioni 44 soko la Afrika Mashariki halipo. Kwa hiyo, sisi ndiyo wenye nguvu, lakini tatizo letu tunafanya nini? Tumeacha kiwanda cha matairi, siku zote nazungumzia kiwanda hiki kwa sababu nakijua, toka nikiwa kijana…

*(Hapa kengele ya kuashiria kumalizika*
*kwa muda wa mzungumzaji ililia)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hii hoja hii.

**SPIKA:** Nadhani kwa kutumia Kanuni Na.2 na mchango wako ni wa kitaalam nakuongezea dakika tano.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa dakika tano za ziada. Nilikuwa kwenye kiwanda cha matairi cha Arusha. *General Tyre East Africa*, ilikuwa ni jina la nyumbani kwa Kiswahili *House hold name*. Katika utaratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipoanzishwa mwaka 1967, tuligawana sisi Afrika Mashariki Viwanda. Tanzania katika viwanda ilichopewa ni kiwanda cha matairi, kwa hiyo kilikua kinatengeneza matairi ya Afrika ya Mashariki, sasa leo iweje Tanzania imebadilika imekuwa soko la matairi yanayotoka nchi jirani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa moja ya kuanzisha kiwanda ni soko la nyumbani. Hivi sisi hapa nyumbani hatuna soko la matairi? Tuna sababu gani ya matairi yote ya Tanzania kutoka nje? Ndiyo ile niliyosema tunapeleka ajira zetu nje badala ya watu wetu kaijiriwa wakatengeneza matairi kwa soko la Tanzania, tunatumia watu wengine kututengenezea matairi sisi tunakua soko tu. Kwa hiyo, nilitarajia katika hizi *proposal* ambazo zinaletwa hapa na Serikali kwenye mambo ya ushuru na nini kusema kweli zingezingatia zaidi haja ya kusaidia viwanda vyetu na kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi pale kwenye nyuzi bandia, kama haiwezi kubadilishwa, kwa sababu ndiyo utaratibu wetu kama kitu kikishapita, kimeshapita hicho, kama haiwezi kubadilishwa basi tuondoe ile Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa viwanda vyetu vya ndani vinavyotengeneza bidhaa zinazoshindana na hizi zinazotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mbunge aliyemaliza kusema sasa hivi anatoka Mkoa ninaotoka. Sasa nataka niwasomee Kanuni Na.2 niliyoitumia kwa sababu wengine

mlianza kuona labda kuna mambo ya *undugunization* hapana. Kanuni ya 2 ya Kanuni za Bunge inasema hivi:-

"Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Spika ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika pamoja na mila na desturi za uendeshaji bora wa shughuli za Bunge..."

Sasa Kanuni zetu hazikuweka uratibu pale ambapo Mbunge mtaalam anatoa mchango mzito wenye manufaa kwa nchi, kwa hiyo, Spika ametumia Kanuni hii kumwezesha Mbunge mhusika ambaye wote mnafahamu ni mtaalam wa masuala haya ili amalize hoja yake na si upendeleo. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye Muswada huu wa Kurekebisha Sheria mbalimbali za Fedha pamoja na Kodi. Mimi nitakwenda kwenye Muswada wenyewe. Nimeupitia vizuri sana na nimetazama Jedwali la Marekebisho. Kuna mambo ambayo hayajafanyiwa marekebisho, naomba niyazungumzie.

Mheshimiwa Spika, moja, kuna neno hapa ambalo limetumika karibu mara tano ambalo ningeomba liandikwe sawasawa. Neno hilo liko katika kifungu cha nne, kifungu kipya cha 10A, ukurasa wa nne, ni neno linaitwa *quasi judicial body*. Naomba sasa ile (-) iwekwe pale na hiyo pia ihusike vifungu vifatavyo, hicho chenyewe cha 4 Kifungu kipya cha 10A katika Muswada wenyewe, halafu Kifungu cha 7(6), Kifungu 13, kifungu kipya cha 39A, Kifungu 20 na Kifungu 26(6). Wale vijana nadhani wanayo *dictionary*, ile *quasi-.judicial body* kale kamstari kakuunganisha mngeicheki ili twende na uhakika. Mimi nimecheki *dictionary* nimekuta kwamba ni sawa hivyo hilo lirekebishwe katika hivyo Vifungu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ninataka kuchangia, ni hili suala la ongezeko la thamani kwenye mazao ya chai na kahawa. Haya yamezungumzwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake katika Kifungu 72(vi) na katika mchango wangu wa maandishi nimemwandikia nikasema hili ukiliondoa tutawakatisha tamaa wakulima. Hebu tuache kwa muda tuendelee na huo msamaha wa Kodi ya Ongezeko kwenye haya mazao mawili chai na kahawa. Kwa mfano, sasa hivi kwa upande wa chai kwenye Jimbo la Bumbuli watu waliacha kulima chai kwa sababu kwanza bei waliokuwa wanalipa ilikuwa ni ndogo sana lakini jinsi bei inavyoongezeka wanahamasika. Sasa nadhani la kufanya hapa ni kujitahidi chai chache sana kwenda kwenye mnada wa Mombasa na chai nyingi iongezwe thamani hapahapa nchini ili mauzo ya nje yawe ni kwenye chai tuliyoiwekea thamani. Mimi naungana kabisa na Mheshimiwa Kaboyonga, kwamba imefika wakati sasa tusiwe nchi inayojenga ajira kwa ajili ya watu wa nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivyo kwa nini? Chai ambayo tunazalisha sisi, bahati nzuri mimi ni mkulima wa chai ni mkulima sio wa nadharia hapana nina kishamba kidogo cha chai sasa ile chai pale mimi ningefurahi kama asilimia 100 tungeipa thamani hapa hapa nchini na tukauza iliyowekewa thamani, tutaongeza ajira na mapato vilevile

hapa nchini. Lakini ilivyo sasa hivi ni asilimia 50 ya chai tunayolima sisi wakulima wadogo wa Jimbo la Bumbuli ndiyo ambayo inabaki hapa kwa kuwekwa thamani na pengine inanunuliwa na watu wengine ambao wanakwenda kuiuza katika nchi hizi ambazo zimetuzunguka lakini asilimia 50 inakwenda kwenye mnada wa Mombasa, tunabishana pale kwenda kujenga ajira za watu wengine. Mimi naungana asilimia mia moja na Mheshimiwa Kaboyonga. Kwa hiyo, naomba hii chai inayosindikwa hapa, hii kodi tungeiacha kwa muda hata kwa miaka mitano tufike mahali pazuri. Sasa hivi tujitahidi zaidi kuhimiza ujenzi wa viwanda vya kuitengeneza hapa hapa na kuipa thamani na tuuze chai ambayo imepewa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Kamati ya Fedha na Uchumi, imeliona jambo hili na mimi nimezungumza na Waziri nikamwandika vilevile mchango wangu wa maandishi ni jambo muhimu sana. Ninapozungumza hapa ninaamini kabisa Wabunge wa Mkoa wa Iringa, Mbeya, Kagera na kule Mara ambako wanaingia sasa kwenye kilimo cha chai wanaunga mkono. Hii kwa kweli ni hoja kubwa sana kwa upande wetu katika zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka kuchangia liko katika Jedwali la Marekebisho la Mheshimiwa Waziri. Mimi napenda kumpongeza sana kwa kuongeza ile sehemu ya (ix) ambayo inazungumzia marekebisho kwenye Sheria ya Benki Kuu Sura ya 195, kwa kuweka vipengele ambavyo vimeweka wazi kabisa *"checks and balances"* kwamba hesabu za Benki Kuu zipelekwe kwa *"Controller and Auditor General"* na kwa wakati ambao unastahili. Hili ni muhimu na kama hili likifanyika mambo ya *EPA* na vitu vingine vya aina hii haviwezi kurudiwa tena maana hapa tayari *"checks and balances"* zimefanya kazi yake. Kwa hiyo, naunga mkono rekebisho hili. Haipo katika mapendekezo ambayo yamekwishaletwa katika ile *Finance Bill,* hayakuwemo hivyo napenda kusema kwamba yaingizwe katika *Finance Bill* na ni mambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba mniwie radhi kidogo. Nilikua Mtumishi wa Serikali tena mwaminifu, nimefanya kazi kama Katibu Mkuu kwa miaka 18, kwa hiyo sikwenda kwenye Chuo cha Sheria lakini *I picked the pieces of knowlegde as I stayed in the government*. Kwa hiyo, Sheria inayotungwa mimi siwezi kui-*draft* lakini nina uelewa kwamba hapa lazima kiwe kitu hiki. Katika Bunge la Kumi na Tatu, nilizungumzia kuhusu matumizi ya alama, lakini nikaambiwa kuna muongozo wa kutunga Sheria. Nikasema sawa tuupate, sasa naomba tuupate ili tusifanye mambo ambayo yanaonekana kama tunakwenda nje ya taratibu za kutunga Sheria. Lakini kuna alama ambazo utake usitake katika maandishi yoyote yale utazikuta, ndiyo niliyokuwa nazungumzia. Utakuta *full stop, comma, colon, semi-colon, hyphen* na utakuta *apostrophy,* hayo yapo. Sasa haya mengine ya kuongezea mimi nasema tuelezwe ili tusionekane kama ni watu wanokonoko tunaingia kwenye vitu vya wataalam vya ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa katika Sheria ya leo nilivyoitazama, haya hayahusu watu wa Wizara ya Fedha, ni watu wa Wizara ya Fedha, sina tatizo nao ni wale ambao hu-*draft* Sheria. Ukiangalia kwenye Sheria hii wametumia *interchangeably* alama mbili *hyphen* kuonyesha vitu vinavyofuata pale ambako *hyphen* inaunganisha maneno lakini wakati huo huo mmetumia *colon* ambayo ndiyo sahihi inatangulia mambo ambayo

yanaorodheshwa. Nilitaka hili niliweke wazi maana yake siku ile nilionekana kama mtu mpumbavu hivi ambaye sielewi mambo, hapana. Uzoefu umetufanya tuweze kuelewa haya mambo mengine, sasa tusaidiwe tu Kisheria kwamba Sheria ipo ya ku-*draft* Sheria na hatutakiwi kutumia alama hii za kimataifa (*international signs in any script*).

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nitachukua kwenye huu Muswada, kifungu kile cha tisa, ambacho kina kifungu kidogo cha nne na hicho kinafuatana na orodha chini yake ukurasa wa tano. Sasa nataka kuuliza hii sentensi inayoanzia kifungu kidogo cha nne cha kifungu cha tisa "*For the purpose of subsection (2) "dutiable value" means, in relation to,* kameweka kamstari (-) *what is the name of that line?* Kale kamstari kanaitwa nini katika alama? Kama ipo ya kisheria basi tupewe lakini haka ni *hyphen* ambayo inaunganisha maneno mawili. Lakini ukiendelea kule chini utakuta mmetumia ile alama yenyewe ya *colon* kuonyesha kuna mambo yanafuatana.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wenzetu walioko nje, utungaji wa Sheria ndiyo huu wenyewe hapa. Tunatunga Sheria kwa hiyo tuwe na uhakika kuwa Sheria inayotoka hapa kwa kweli imetungwa vizuri na imezingatia mambo mengine ya kijumla vinginevyo itakua kama tunalipua tu.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono kabisa marekebisho haya lakini hoja ambazo nimezitoa hasa ile ya kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye chai na kahawa, ni suala ambalo litatusaidia kuimarisha uchumi wetu na hasa tukijitahidi kujenga viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao hayo ili tuyauze nje kwa bei nzuri maana mazao ambayo yameongezwa thamani. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja hii tena. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shellukindo.

Waheshimiwa Wabunge, nimeshauriana na Serikali na kufuatia mchango mzuri sana ambao Waheshimiwa Wabunge mmeutoa, wanahitaji muda kuweza kuangalia mambo gani ambayo pengine yanaweza yakaleta tija zaidi. Kwa sababu hiyo na ukizingatia muda umebaki dakika thelathini, haututoshi hata kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima na kupitia kifungu kwa kifungu, kwa hiyo, uamuzi ni kwamba tutaendelea hapo saa kumi na moja jioni.

Lakini kabla ya kuhitimisha hoja kwa asubuhi hii, kupitia Kiti hiki, nataka kutoa tahadhari kwa wenzetu Waandishi wa Habari kwa baadhi ya mambo ambayo yanaweza kuleta sura ya Bunge kuonekana ni tatizo tatizo hivi.

Hapa ninalo gazeti la jana la Mwananchi, kuna picha katika ukurasa wa 12, inaonesha kama vile Mbunge Richard Ndassa anakaribia kumbusu Mbunge Lucy Owenya na mbaya zaidi ni kwamba karibu yao kabisa, anaonekana baba yake Mheshimiwa Lucy Owenya ambaye naye ni Mheshimiwa Mbunge. Ukizitazama zinaonesha kama vile yametumika maarifa tu ya kamera kuwafikisha katika hali hii, sasa

sijui nia yake nini? Lakini naomba wenzetu, tumevumilia sana sisi Wabunge, leo asubuhi nimemuagiza Katibu wa Bunge, Sheria ya *Powers and Privileges* ya Bunge sasa ianze kutumika. *(Makofi)*

Kuna magazeti yanaonesha kabisa yanaendesha *Jihad* kamili dhidi ya Bunge. Moja ya magazeti hayo ni gazeti linaitwa RAI. Jana Rai imesema hili ni Bunge la Marehemu. Sasa tunafika mahali ambapo; ni kwa sababu tunamaliza muda wetu lakini inawekwa katika hali ya chuki tu na mengi mengine wamepotosha sana kuhusu maslahi na mishahara ya Wabunge kwa makusudi kabisa kwa kujumlisha vitu ambavyo wala si mshahara. Mishahara ya wasaidizi, matengenezo ya magari yote imeitwa mshahara ili tu kuchochea chuki ya wananchi dhidi ya Bunge.

Kwa hiyo, nimemwagiza leo kwa maandishi Katibu wa Bunge wakusanye haya magazeti mbalimbali waone yale yenye nia mbaya basi. Mihimili hii imepangiwa kwa umuhimu wake Mahakama, Serikali na Bunge kila mmoja amepangiwa ndani ya Katiba na Sheria vipengele vya kumlinda. Kwa sababu mmoja wapo ukitetereka kabisa mambo hayaendi. Sasa Bunge nalo ndiyo lina sheria hiyo ambayo inatulinda, hatusemi tusikosolewe, Wabunge ni baadhi ya watu katika jamii wanafurahi sana kukosolewa ili wajirekebishe lakini ukosoaji uwe ni kwa mambo ya haki, sio kujaribu kuchochea chuki ya wananchi dhidi ya Bunge hata kama unamchukia Mbunge fulani basi isiwe tena jukumu lako kutumia magazeti ili kulichafua Bunge zima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Katibu kama nilivyokuandikia leo asubuhi, yafuatilieni sio magazeti tu na vyombo vingine ili sasa tuanze kuchukua hatua. Tumevumilia sana nadhani sasa mtajua tumefika pagumu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.27 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

*(Hapa Wabunge fulani walishangilia baada ya Mwenyekiti kuingia Ukumbini)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwashukuru sana kwa makofi mazito. Nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Waheshimiwa Wenyeviti wote, tumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyoonesha utendaji wake kazi kwa viwango vikubwa sana. Leo tunaweka historia mpya katika Bunge letu, kwa miaka mingi Wenyeviti tulikuwa tukiingia huku katika Kiti tukiwa katika mtazamo tofauti, lakini leo nadhani Bunge limechukua sura mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ninaomba niwathibitishie tu, joho langu linanitosha; la Mheshimiwa Zubeir linamtosha; na la Mheshimiwa Job pia linamtosha sawa sawa. Nashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu, naomba tuendele na hatua inayofuata.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wengine wote, kwa kazi nzuri na za kutukuka mnazozifanya Wizara ya Fedha. Pia nawapongeza sana kwa kuiwezesha Bajeti ya Serikali ya 2009/10 kupita bila zengwe; hongereni sana. Nawapongeza pia kusikia mmefuatilia, mmefanya utafiti na kukubaliana na ushauri wa Wabunge, Viongozi wa Dini, Wasomi, Wataalamu na Wananchi kwa ujumla, juu ya kurudisha misamaha ya kodi kwa vifaa vya kiroho, afya, elimu na kadhalika, kwa Mashirika yetu ya Dini. Pia nakupongezeni sana kurudisha asilimia kumi ya kodi kwa mafuta ya kula yanayoagizwa toka nje. Wananchi wameridhishwa sana na uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, sina wasiwasi na kupita kwa Muswada wa Sheria hii ya Fedha ya 2009. Bunge litaipitisha bila tabu, ninachoomba wewe na Wasaidizi wako; wakiwepo TRA na wengine wote wanaofanya kazi chini yako, wafanye kazi kwa makini na uadilifu mkubwa ili kuleta mafanikio kwenye ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha mianya yote ya kukwepa kodi inazibwa, kuhakikisha bandari yetu na reli zinafanya kazi nzuri ili kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote wana imani kubwa na Serikali ya Awamu ya Nne na wanategemea ahadi nyingi zilizotolewa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2005, zitatekelezwa na mwezeshaji mkubwa wa kutekeleza ahadi hizo zote ni wewe na Wasaidizi wako. Inawezekana, tekelezeni wajibu wenu.

Mheshimiwa Spika, tunatarajia mabadiliko makubwa, pamoja na kuyumba kwa Uchumi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aisaidie Bodi ya Mazao Mchanganyiko, ianzishwe mapema, nayo itasaidia sana kuinua uchumi wa nchi yetu.

Naitakia Wizara na Serikali kwa ujumla, utekelezaji mwema wa kazi zote kwa mwaka 2009.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu, unaokusudia kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali zinazohusu fedha na kodi. Kufuaatia kuwasilishwa kwa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupendekeza matumizi ya nyaraka za kielektroniki *(Electronic Document)* na kuruhusu matumizi yake Mahakamani. Hilo ni jambo jema, hasa ukuzingatia kwamba, sasa tupo kwenye karne ya sayansi na teknolojia. Hatua hii itarahisisha sana utendaji wa kazi hasa katika suala zima la makusanyo ya kodi na kuisimamia Sheria yenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda nitoe tahadhali kwa Serikali na Wizara ya Fedha na Uchumi kwamba, itabidi iwe makini sana katika matumizi ya nyaraka za kielektroniki *(Electronic Documents).*

Kwa kuzingatia hatua kubwa ya maendeleo ya sayansi na teknolojia hasa katika eneo la Kompyuta; ni rahsi sana watu kucheza na nyaraka hizo na hivyo kupotosha ukweli na kuharibu ushahidi pale zitakapotumika kama ushahidi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza ada ya mazao *(Produce Cess),* kutoka asilimia tano hadi asilimia tatu kuanzia mwaka ujao wa fedha 2010/11. Hata hivyo, lingekuwa jambo zuri zaidi iwapo Serikali ingeanza kutekeleza hatua hiyo mwaka wa fedha wa 2009/2010. Hatua hiyo ingewapa wananchi wetu, hasa wakulima, unafuu zaidi na hivyo kupata bei nzuri kwa mazao. Serikali ingeweza kabisa kuficha pengo ambalo lingesababishwa na hatua hiyo ya kupunguza ada za mazao. Aidha, nashauri kupunguzwa kwa ada hiyo, iwe ni hatua ya kudumu wala lisiwe suala la muda tu. Hilo likifanyika, itaonekana Serikali inawajali sana wananchi wake hususan wakulima. Nashauri pia ukusanyaji wa kodi hiyo usimamiwe vizuri, kwani wafanyabiashara wengi, hasa wanaonunua mazao kwa mkulima, hukwepa sana kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuondoa ushuru wa kushusha na kupakia mizigo kutoka melini *(Steve Doaring).* Hata hivyo, bado kuna tatizo la meli zenyewe (kutoka nje), kuendelea kutozwa ushuru wa asilimia 18, tofauti na Bandari za nchi jirani kama vile Mombasa na Beira, ambazo hazitozi ushuru huo.

Mheshimiwa Spika, hatua hiyo huzifanya meli au wenye meli, kuamua kutotumia bandari zetu hususan Dar es Salaam na hivyo kupoteza mapato mengi.

Nashauri kwamba, kodi hiyo ya Ongezeko la Thamani (asilimia 18), kwa meli kutoka nje, ifutwe kabisa ili kuvutia wafanyabiashara wengi wenye meli watumie bandari zetu na hivyo kuinua pato la bandari au Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali isiondoe msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye chai na kahawa inayozalishwa na kusindikwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hili litaathiri Wananchi wa Tanzania, ambao ni wakulima wadogo. Mwaka jana ndio tumeanza kuongeza uzalishaji wa chai. Chai yetu bado ni kidogo tu. Litaathiri uzalishaji na kufumua soko kwa chai ya wageni!

Mheshimiwa Spika, kahawa pia ni zao linaloendelea kudhoofika kiuzalishaji, kwa sababu ya soko kuwa baya. Naomba izingatiwe kwamba, Tanzania tunavyo viwanda vichache vya kusindika kahawa kama vile TANICA cha Bukoba. Hebu, Serikali itafute kianzio kingine.

Mheshimiwa Spika, chai na kahawa ni maeneo yanayotoa ajira na kipato kwa watu wetu; tuwalinde. Isitoshe, watu waliojisajili kulipa VAT ni wachache, kwa hiyo naomba wafikiriwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha kilio hiki na kuomba chai na kahawa isitozwe VAT. Ahsante sana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Waziri kutueleza kwamba, *Visa* walikuwa wanatoza kutokana na nchi wageni wanapotoka, lakini tukumbuke watalii wengi wanaotembelea Tanzania, nchi inayoongoza ni Amerika ikifuatiwa na Britain, German na kadhalika. Wageni hawa wanalipa US$ 50 kwa mtu kwa *single entry,* lakini *multiple* wanalipa US$ 100 kwa mtu.

Je, punguzo la ada ya *Visa* liko wapi? Wageni wote hulipa *Visa* au *arrival* na wanalipa US$ 50 kwa mtu.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, *Section 10A;* nashauri *electonic evidence* kabla haijatumwa au kukabidhiwa iwe *certified true copy of the origin.*

*Electronic Document* na *Electronic Evidence,* ningependa kujua na kuhakikishiwa jinsi ya kuzuya kughushi.

*Part IV, Section* 139A - *Electonic evidence;* naomba kuhakikishiwa kuzuia kughushi hizi *Electonic Document and Electronic Evidence*. Ni kweli *Bill* inasema *unless the contrary is proved*; *What if it is not proved*? Kwa nini tusikubaliane *to certify as a true copy of the origin*?

Mheshimiwa Spika, kwa shughuli za *forwading and clearing*, wana utaalamu wao kwa mfano, *Persons Authentication Code.*

Mheshimiwa Spika, *Part V; Amendment of Local Government Act.* Ushuru wa mazao kwa wanunuzi:-

(a) Ushuru wa Mazao – 3% ya bei ya *gate:* Sasa hivi kuna soko huria, *how do you determine Farm Gate Price?* Naomba kuwepo na *Definition* ya *Farm*

*Gate Price.* Neno liwe *classified – Farm gate Price.* Ni lazima kuwepo na *Security Devices* na *Computer Misuse.*

(3) We need adequate mechanisms in the available law or new laws are enacted at both National and International level that would deter the would be – hacker a fraudster.

(4) There is greater co-operation between Countries to exchange information about cross-border data flow and access to evidence.

Security Device using digital cryptology that makes computer break is near impossible, thereby reducing chances of forgery or alterations of data.

Electronic hutumika katika International Trade Law.

Tuwe na Computer Misuse Act; some traditional Criminal Law could not cope with certain kinds of Computer related crime due to intangible nature of the information held on Computers.

This legislation will carry criminal sanctions in event of Computer misuse.

Zipo Internal Convention on Cyber Crime. The success of the above Convention depend on countries willingness to participate. In England, there is hear say rule in civil proceedings. The Civil Evidence Act was passed in 1995 which allows the admissibility of Computer generated evidence.

Guarantee of Non Corruptibility of Computer System; litatumika katika Electronic Document; Airport Service Charge Act; Sheria ya Kodi ya Mapato; Excise (Management and Tariff Act); Sheria ya Ushuru wa Stempu; Income Tax Act; Sheria ya Tozo ya Huduma za Bandari; Stamp Duty Act; Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani; Port Service Charge Act; Value Added Tax Act; Evidence Act; na The Evidence Act.

Definition of Electronic Document means Fax; Scanned; and Printed kwenye Computer Email.

**MHE. GEORGE M. LUBEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2009.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Naipongeza sana TRA kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato; hata hivyo, nashauri Serikali iendelee kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili mapato yapatikane ya kutosha kwa ajili ya kuboresha huduma za Kiuchumi na Kijamii. Misamaha ya kodi idhibitiwe

kikamilifu kwa vile inapunguza mapato ya Serikali. Ipo haja kubwa ya kuziachia Serikali za Mitaa vyanzo zaidi ili kuzijengea uwezo kimapato na kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu.

Kwa kuwa hivi sasa Serikali za Mitaa zinategemea ruzuku ya Serikali kwa asilimia 90 – 95, kwa hiyo, ipo haja ya kuziachia baadhi ya vyanzo Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilima 100.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hatua inayofuata sasa ni kuanza kupokea taarifa ya maelekezo na maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, kama walivyoyatoa kwenye Muswada wenyewe. Mheshimiwa Naibu Waziri tuanze una dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Fedha wa mwaka 2009. Nitachangia mambo mawili; moja, lililotamkwa na Mheshimiwa Chegeni, kuhusu maduka yetu ya fedha za kigeni na aliloona kuwa ni tatizo la kutumia fedha za kigeni badala ya kutumia sarafu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, tunakubaliana naye kwamba, ndio kumekuwa na matatizo katika uendeshaji wa maduka haya toka yalipoanza mwaka 1992. Lakini mwaka hadi mwaka, usimamizi wa maduka haya umeboreka na hivi sasa Benki yetu Kuu, ambayo ndiyo msimamizi wa maduka haya, imechukua hatua ambazo nazo zinalenga kwenye kuboresha zaidi na kuongeza udhibiti wa biashara zao na moja ya mambo ambayo Benki Kuu imefanya hivi karibuni na tayari imeshaanza ni kutunga Kanuni Mpya za Usimamizi wa maduka haya. Vilevile kuweka sharti la kiwango cha chini cha mtaji, ambao utahitajika kama unataka kufungua duka la fedha za kigeni; kwamba, utahitajika uwe na mtaji wa shilingi milioni 40. Utatakiwa pia ujiandikishe kama kampuni ambayo imesajiliwa ili uweze kuingia kwenye usimamizi kamili wa Benki Kuu. Tunatarajia kwamba, Benki Kuu wakishirikiana na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, wataongeza nguvu kwenye usimamizi wa maduka haya na kwamba, kwa kufanya hivyo, tutaweza hatimaye kuwa na maduka tu ambayo kweli yanafuata taratibu, sheria na kanuni ambazo zimewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuhusu hatari zinazotokana na kutumia kwa wingi, kiasi kikubwa cha fedha za kigeni kwenye uchumi wetu. Hii ndio sababu Serikali kupitia matamko hapa Bungeni, Mawaziri wa Fedha wametoa matamko mbalimbali kuhusu matumizi ya fedha hizo na kuwahamasisha na kuwahimiza Watanzania, kuienzi Shilingi ya Tanzania ambayo ndiyo sarafu kwa malipo halali nchini chini ya Sheria, lakini pia kuelewa athari ambazo zinaweza kutokea kutokana na matumizi makubwa nchini ya fedha za kigeni ambayo ni pamoja na mfumko wa bei na vile vile kupunguza uwezo wa usimamizi wa uchumi wetu. Serikali itaendelea kutazama jambo hili na tunajua athari zake. Kuna nchi ambazo zimeachia, zikafika mahali ambako zimepoteza uhai kama Taifa, kwa mfano, ukitazama historia ya Equador -

nchi moja kule Amerika ya Kusini, walifanya mzaha na jambo hili, wakajikuta hawana nchi na nchi yenyewe imekuwa kama Jimbo la Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili utakuwa kujibu aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge, ndugu yangu na *colleague really,* Mheshimiwa Juma Kaboyonga, siyo kwa sababu ya kubishana, lakini kwa sababu ya ufafanuzi na inatokana na tuliyosema jana yaliyoko kwenye Kitabu cha Bajeti ya azma ya Serikali kukopa shilingi bilioni 300 kutoka Benki Kuu kwenye Mwaka wa Fedha 2009/2010. Kwanza, niseme kwamba, kukopa kutoka Benki Kuu si jambo la ajabu. Tuko kwenye hali ambayo siyo ya kawaida kiuchumi, kwa hiyo, tunatakiwa tuchukue hatua ambazo *ordinarily* tusingechukua.

Hakuna nchi hata moja, ambayo inataka kwa sasa hivi kurekebisha uchumi wake na kuendeleza kukuza uchumi wake duniani, ambayo haichapishi pesa. Marekani imechapisha, Japan imechapisha, China imechapisha, kwa hiyo, sio ajabu. Sisi si kwamba, tunafuata mkumbo tu; kwa nini iwe shilingi bilioni 300 na sio bilioni 900 kwa mfano? Shilingi bilioni 300 inatokana na tathmini iliyofanyika na kuoenekana kwamba, tukikopa na kuchapisha kweli shilingi bilioni 300 na kuzitumia kwenye uzalishaji, basi hizo fedha hazitapelekea kuwa na mfumko wa bei ambao tutashindwa kuudhibiti.

Niseme hapa kwamba, shilingi bilioni 300 hizi tumezikokotoa na tukaona kwamba, ongezeko la deni ni asilimia 1.6 ya Pato la Tafa. Sasa hivi Deni la Taifa kwa Pato la Taifa ni asilimia 33. Kama nilivyosema jana, bado tuko chini sana; wastani wa nchi ambazo zinataka kupiga hatua kiuchumi, deni lao la taifa kwa Pato la Taifa ni kati ya asilimia 40 na asilimia 70. Kwa hiyo, bado tuna nafasi kubwa sana ya kuendelea kukopa ama ndani ya Benki Kuu au nje ya Benki Kuu na bado tutakuwa na uwezo wa kudhibiti mfumko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema jana, sera za fedha zinasimamia asilimia 25.9 tu ya mfumko wa bei. Iliyobakia asilimia 74.1 inatokana na gharama za chakula na ndio sababu kwa wakati huu, Serikali kwa kuamua kwamba, tutakuwa na ajenda ya Kilimo Kwanza. *We couldn’t have done better, that is the right thing to do.*

La pili la kufanya ni kuweka mkazo kwenye miundombinu, kwa mfano, China imeamua kwamba, wao wataongeza juhudi kwenye miundombinu kiasi kwamba, wanavunja madaraja ambayo ni mazima *so that they create employment, and to that they have to print money*. Kwa hiyo, tusiogope hata kidogo. Tunatakiwa tu-*print money, we shouldn’t be afraid of printing money, we need that*. La muhumu ni kiasi cha fedha, ambacho tuna-*inject* kwenye uchumi, kinaweza ku-*sustain*, kinaweza kudhibitiwa na kinaweza kusimamiwa vizuri kisipeleke mfumko wa bei *out of control; that is the main thing*. La pili ni kukopa kupekeleka kwenye uzalishaji. Tusiogope mfumko wa bei; *it is necessary,* siyo mnyama huyu, haumi.

La msingi ni kwamba, unakopa, unazipeleka kwenye uzalishaji. Mkopo wa *short term* unaupeleka kwenye uzalishaji wa *long term and therefore* kama umezalisha

*inflation* kwenye *short term*, matokeo ya uzalishaji ambao utakuwa umetumia zile fedha *will counter your inflation pressure*, ambayo mtakuwa mmepata kushoto. Kwa hiyo, ndugu yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Siraju, nafikiri kwa kicheko kile, hapo tunakubaliana. Nafikiri tumekwenda vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo nataka kusema kwa upesi upesi tu ni kuhusu utegemezi. Si kweli kwamba, utegemezi wetu unatisha. Toka mwaka jana tumekwenda vizuri sana na ukitazama kwenye Kitabu cha Bajeti, ambacho Mheshimwa Waziri wa Fedha alikichapisha, ukitazama sura ya bajeti na zile takwimu, *if you look them closely* na ukafanya zile hesabu; utaona kwamba, bado kwenye *revenue expenditure* tuna *surplus* ya shilingi bilioni 84. *We don't have a deficit in that*. *Issue* hapa ni lile deni la taifa; unalifanyaje? Unaliweka wapi; kwenye *revenue* ama kwenye *capital expenditure*?

Nasema kwamba, ukiliweka kwenye *recurrent expenditure*, hiyo sio sahihi kwa sababu hili deni sio la *short term* ni deni ambalo nchi inalipa *over a long period*. Mara nyingine kwenye ile orodha ya madeni yale, tuna madeni ambayo yana *span* ya *over 40 years or 50 years*. Kwa hiyo, hii ina maana kwamba, lile deni huwezi kulichukua ukalitumia kwenye ukokotoaji wakati unapotaka kujua hali halisi ya matumizi ya Serikali. *However*, ninakubali kwamba, hata shilingi bilioni 84 ambazo tunasema ni *surplus*, hazitoshi kuwa ndio *contribution* yetu kwenye ile *portion* ya bajeti kwenye *development*, hiyo nakiri. Hiyo ni changamoto na niseme hapa, sio changamoto ya Serikali ni changamoto ya sisi sote, Wabunge na Watanzania kwamba, tutaongezaje ile *portion* ya mapato ya ndani. Ile siyo kazi ya TRA tu (Mamlaka ya Mapato) ni wajibu wa Watanzania.

Ukisoma Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, utaona anachosema kule, kwa kiasi kikubwa amethibitisha kwamba, bado tuna uwezo mkubwa sana Watanzania kuchangia kwenye mapato ya ndani na si kwamba Serikali haikusanyi kodi au haisimamii kodi. Tunasimamia sana, kiasi ambacho mara nyingi vijana wetu kwenye Mamlaka ya Mapato wanaambiwa ni wakali sana. Huo ndio usimamizi wa mapato na hiyo ndiyo *collection*. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba, tusaidiane na Serikali kuijenga nchi hii, *it is our country, we have to fix it ourselves*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja hii ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2009. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Sumari, nilitaka kushangaa kama ungeondoka hapo bila kuunga mkono hoja, ambayo umeitoa wewe mwenyewe kupitia Wizara yako. Naomba nimwite mtoa hoja, Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri, naye aweze kuhitimisha hoja hii. Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi.

Naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo: Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Muswada huu. Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kambi ya Upinzani, kwa maoni na ushauri wao pia. Ninaahidi kwamba, Serikali itayafanyia kazi maelekezo na mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha ya Uchumi na yale yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani. Naomba sasa nianze kujibu hoja moja baada ya nyingine, kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kujibu hoja ambayo imetolewa na Wabunge, ambayo inahusu kuondoa ushuru wa kodi ya forodha kwa mafuta ghafi kwa asilimia kumi kutadumaza kilimo cha mbegu za mafuta nchini. Hoja hii ilitolewa na Mheshmiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Dr. Gama, Mheshimiwa Kaboyonga na Mheshimiwa Dr. Chegeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, Serikali ilikuwa makini katika kuitafakari hoja hii na kabla hatujafikia hoja hii, zilifanyika stadi mbili. Stadi ya kwanza ilifanywa na wenzetu CTI, kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda. Stadi ya pili ilifanywa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kilichobainika ni kwamba, uzalishaji wa mbegu za mafuta hapa nchini, hautoshi kukidhi mahitaji ya viwanda vya mafuta nchini. Uzalishaji wa ndani ulionekana kuchukua chini ya asilimia kumi. Kwa maana nyingine, asilimia zaidi ya 90 ya mafuta yalikuwa yanatoka nchi za nje na hasa Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe takwimu tu ili Waheshimiwa Wabunge wawe nazo katika kujiridhisha. Uwezo wa kusindika wa viwanda vya mafuta tulivyonavyo hapa Afrika Mashariki nzima, ilikuwa ni milioni *1.5 metric tones.* Huo ndio uwezo wa viwanda vyetu tulivyonavyo ndani. Katika milioni *1.5 metric tones*, viwanda vya Tanzania vilikuwa vina uwezo wa kusindika mafuta *510,000 metric tones*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie uwezo wa uzalishaji wa mbegu au upatikanaji wa mbegu. East Africa kwa ujumla, tulikuwa na uwezo wa kupata *120,000 metric tones*, viwanda vinaweza kuzalisha milioni 1.5, uwezo wa East Africa wa mbegu ni 120,000 na uwezo wa Tanzania wa kupata mbegu ndani ya nchi yetu ilikuwa ni *metric tones 65,000.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuwa, hapa tuna upungufu. Wenzetu Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda; na hasa Kenya na Uganda, ambao wana hivi viwanda vya mafuta, wanaitegemea Tanzania izalishe mbegu nyingi na wao wako tayari kununua mbegu za Tanzania ili watoe mafuta, lakini uwezo huo hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile nataka niseme kwamba, mbegu zinazozalishwa kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta hazitozwi VAT. Kwa hiyo, mbegu hizi zinazalishwa, zinapelekwa kwenye kiwanda.

Tumeamua kufanya nini katika suala hili licha ya kwamba hatuna uwezo wa kuzalisha mbegu kukidhi mahitaji ya viwanda vyetu? Serikali yenu ni sikivu, kwanza, tumesema wazalishaji wa mafuta wale wadogo wadogo, wakulima, ndugu zangu wa Singida na maeneo mengine mnaelewa; wazalishaji wa mbegu wanawauzia wale wanaokamua wenye viwanda vidogo vidogo. Wanakamua katika grade mbili, hawafikii ile ya tatu ambayo ndiyo hii iliyo nzuri inayouzwa. Tumesema wale wenye viwanda vidogo vidogo, watakapokamua yale mafuta na kuyauza kwenye viwanda vikubwa vikubwa kwa ajili ya ku-*refine* yale mafuta, tumewaondolea ushuru wa VAT wa asilimia 18; hawatalipa Kodi ya VAT.

Sasa hii ina maana kwamba, wenye viwanda hao wanao-*refine* mafuta, tunawa-*encourage* wanunue mafuta ya ndani, kwa sababu hayatakuwa na Kodi ya VAT ya asilimia 18. Kwa hiyo, badala ya kuingiza mafuta kutoka nje, tutapata nafasi nzuri na tija nzuri kununua mafuta ya ndani. Watakaponunua mafuta ya ndani, yule mdogo mdogo anayekamua na yeye baada ya wiki mbili ataona duuh! mafuta yangu yamemalizika, sina tena mafuta, atawashawishi wakulima wazalishe mbegu zaidi, tukishirikiana na Wabunge. Kwa hiyo, jukumu letu sisi Wabunge ni kuwahamasisha wakulima, wazalishe mbegu zaidi ili tuweze kukamua, halafu tuwauzie viwanda vikubwa vikubwa bila kuwa na Kodi ya VAT. Kwa mtazamo huo, tunadhani kwamba, Serikali itakuwa imefanya *justice*. Tutalinda wakulima wetu wa mbegu, halafu tutalinda vile viwanda vyetu vikubwa vikubwa, ambavyo vinaajiri watu zaidi ya 1,000. Tutalinda ajira zetu katika viwanda vikubwa vikubwa.

Kwa hiyo, kuanzia leo, jukumu letu sisi Wabunge ni kuwahamasisha wakulima wetu wazalishe mbegu nyingi zaidi, kwa ajili ya ndani na kwa ajili ya Soko la Kenya na Uganda. Soko liko wazi, wenzetu wameshatuhakikishia, wanasema sisi hatuna ardhi ya kulima hizo mbegu, Tanzania mnayo ardhi, limeni tununue. Kwa hiyo, kwa hoja hii, nadhani Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi tumefikia muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ilikuwa ni suala zima la kurejesha ushuru wa forodha kwa asilimia kumi wa *synthetic yarns.* Sasa hapa nataka nije na historia

kidogo ili tuweze kuwa pamoja katika suala hili. Kodi hii ni pamoja na wenzetu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunapokaa na wenzetu, tunaanza na Kamati ya Wataalamu *(Technical Committee)*. Tukitoka kwenye Kamati ya Wataalamu, tunakuja Makatibu Wakuu, kikao chao kutoka *The Sectoral Ministries* ambazo zina wajibu katika suala lile. Tukitoka hapo, tunakwenda kwenye Mkutano wa Mawaziri. Katika Kamati ya Wataalamu, hoja hii tumesema kwamba, irudishwe ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Kaboyonga, usipige makofi, bado sijamaliza. Tumesema irudishwe ifanyiwe kazi na baadae Makatibu Wakuu na Mawaziri, washauriwe ipasavyo *on the basis* ya *scientific analysis*. Wenzetu wamelifanyia kazi, waliyobaini ni mambo mengi sana, lakini naomba kwa sababu ya muda, niyataje machache. Kwanza, wamesema soko la nje wanalouza *materials* ndilo linalo-*determine* kukupa wewe *order* kwamba, wanataka *75% cotton* na *25% polyster*.

Wenzetu hawa tunapowawekea kodi, wanasema kwamba, soko lao la nje linakuwa vigumu ku-*compete* kwa sababu wao wanakuwa na gharama kubwa. Pili, wataalamu wametuambia kwamba, sasa hivi katika kuchanganya, mara nyingi wanachanganya wakitumia na hii *synthetic yarn*. Kwa maana hiyo, hatuwezi tukasema kwamba, tunataka kutengeneza ya kwetu ya *cotton* wakati soko linataka kuchanganya na *polyster*.

Sasa kwa sababu hii kodi ni ya Afrika Mashariki; ni kodi ambayo ni pamoja na wenzetu Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, tukasema kwamba, sisi Hazina ambao ndio wawakilishi katika masuala ya kodi kwa Watanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tutashauriana na wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili sisi Tanzania tuweze ku-*suspend* kodi hii. Mheshimiwa Kaboyonga, nilijua utapiga makofi. *(Makofi)*

*Common Market* inaanza mwaka kesho Januari. Kwa hiyo, hili suala tunaweza tukaenda nalo mpaka ikifika Januari litakuwa halina tena utata, kwa sababu suala zima la *Common Market* linasema huwezi ukawabagua wenzako. Ndiyo tabu yake; huwezi ukambagua mwenzako, ukalinda kiwanda chako. Tumekubaliana kuwa na soko la pamoja, ambalo linaanza mwaka 2010 Januari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama Waheshimiwa Wabunge watakumbuka, haya mambo ya *Common Market* yana umuhimu wake kwa ushirikiano na mustakabali wa nchi zetu zote tano. Kwa hiyo, tulichokiamua; Serikali yenu tulivu imeamua ku-*suspend* kodi hii mpaka hapo tutakapokuja nayo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo liliibuka ni la msamaha wa VAT kwenye chai na kahawa. Tumetakiwa kurejesha ili kunusuru viwanda na kuongeza uzalishaji wa mazao haya. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Kigoda, dada yangu Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Shellukindo na dada yangu Mheshimiwa Ruth Msafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze kama ifuatavyo: Serikali imeliangalia kwa kina suala hili la kodi kwa wakati huu. Nini tulichokiamua? Kabla sijasema hapo, nataka niseme tu kwamba, kama nilivyoeleza; Januari 2010 *Common Market* hatutaweza tena kuzuia chai na kahawa toka Kenya isiingie Tanzania. Kwa hiyo, hata wewe ukisema kodi hii unaiondoa sasa hivi, uko kwenye kipindi cha miezi sita tu mpaka Januari mwaka kesho hii kodi inarudi palepale; kwa sababu huwezi kubagua chai ya Kenya na Uganda kwa chai yako. Kwa hiyo, kwa upande wetu, tumesema vilevile kwamba, kodi hii tunai-*suspend* ili kuweza kuangalia mpaka mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe msamaha kwenye uzalishaji wa ndani wa mbegu ili ziweze kusaidia unafuu wa mafuta. Hapa nitaeleza kidogo tu kwamba, viwanda vidogovidogo vinavyozalisha mafuta, kama nilivyosema mwanzo, havina Kodi ya VAT kwa sababu mapato yao kwa mwaka lazima yawe milioni arobaini na kuendelea ili viweze kuwa *registerd* katika VAT. Kwa hiyo, iko hivyo na suala hili liliulizwa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Gama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa ni mapato yatokanayo na Visa, Balozi zitafidiwa vipi? Dada yangu, Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Lucy Owenya, walilizungumza hili. Nataka niseme tu kwamba, hapa tunazungumzia Visa za nchi tatu; tunazungumzia Marekani, *currently* ndio ambao wanalipa dola mia moja; *Ireland*, *currently* ndio wanaolipa dola mia moja na Pakstani, ndio wanaolipa dola mia mbili. Nchi nyingine zote zinalipa dola hamsini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokisema hapa, nchi hizi ili ku-*encourage* utalii tumepunguza viwango vya Visa na hasa Marekani. Watalii wengi wanatoka Marekani wanakuja Tanzania, tunahisi kwamba, tukipunguza Visa kutoka dola mia moja mpaka dola hamsini, tuta-*encourage* utalii, kwa maana hiyo, Balozi zetu zitakusanaya mapato zaidi, kwa sababu Watalii wengi watakuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tunasema kila Balozi tayari ina kasma yake na fedha zake katika Bajeti. Atakapokuja Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ataeleza; kama Balozi itakuwa na upungufu wa fedha, basi ni wajibu wetu Hazina kuwapelekea, kwa sababu bajeti yao itakuwa imepitishwa na Bunge hili. Visa ni chanzo pekee ambacho kinawasaidia Mabalozi wetu kuweza ku-*run activities* zao huko waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Godfrey Zambi, alitaka tufute VAT kwenye meli kutoka nje. Kama mtakumbuka, tumesema kwamba, tunafuta VAT kwa meli za ndani. Sasa yeye kasema tuzifutie VAT na meli zilizoko nje. Nataka nimueleze kwamba, ushauri wake ni mzuri, tumeupokea na tutaufanyia kazi. Kuufanyia kazi ikiwa ni pamoja na ku-*study* wenzetu Kenya wanafanya nini katika hizi meli za nje. Kwa hiyo, pengine mwaka kesho tukija hapa, tunaweza kuja na ushauri mzuri zaidi katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Pindi Chana, ambaye ametaka Sheria ya Ushahidi ifanyiwe marekebisho ili kukidhi mahitaji ya *electronic documents*. Nataka nimwambie mdogo wangu kwamba, tayari Sheria ya Ushahidi imekwishafanyiwa marekebisho kupitia Sheria Namba Mbili ya

Mwaka 2007 ili kuruhusu *elecrtonic documents* zikubalike kama ushahidi mahakamani. Kwa hiyo, sheria hii tayari imekwishafanyiwa marekebisho na itaweza kuruhusu hizo *electronic documents* kutolewa kama ushahidi mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imetolewa kutoka kwa Mheshimiwa Mgana Msindai ni suala zima la Wizara ya Fedha, isaidie uanzishwaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Nataka nimwambie kaka yangu Mheshimiwa Msindai kwamba, Serikali imeupokea ushauri na Wizara yangu itakaa pamoja na Wizara ya Kilimo na Wahusika wote ili tuweze kuona hatua za kuchukua, ikiwezekana haraka sana. Tutaangalia Bodi hizi ambazo wananchi wanazihitaji kama zina faida, tukiona zina faida basi tutazianzisha haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho ni ile ambayo imeulizwa au imechangiwa na Mheshimiwa Lubeleje kuhusu kuziachia Serikali za Mitaa vyanzo zaidi vya mapato. Hoja hii itachukua muda kidogo. Mheshimiwa Lubeleje, alikuwa ana *point* hapa, anasema hivi sasa Serikali za Mitaa zinategemea zaidi Ruzuku. Nimesoma hoja zake zote; zinategemea ruzuku kutoka Serikali Kuu, lakini kwa bahati nzuri akaeleza kwamba, hawafanyi kazi za kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu umewaacha huku wategemee ruzuku, *of course*, ndio *nature* ya mwanadamu; kama kuna *free lunch* kwa nini afanye kazi? Mimi nataka niseme kwamba, hapa pana ajenda kidogo mbili, tatu. Nataka nizungumzie kwa Mheshimiwa Lubeleje na Watanzania wote wanisikie na Halmashauri zote zinisikie na Wabunge tusaidiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ni kwamba, vile vyanzo vilivyomo katika Halmashauri havikusanywi ipasavyo. Suala hili tumelizungumzia mwaka jana tukasema, kwa kushirikiana na TRA, tutajitahidi kutoa mafunzo ili kuzisaidia Halmashauri zetu ziweze kukusanya kutokana na vyanzo vile vilivyoko ndani ya Halmashauri. Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi; mtakumbuka kwamba, tumeipa kazi TRA kuanza na Mkoa wa Dar es Salaam, Ilala, Temeke na Kinondoni. Katika Kodi ya Majengo, nadhani Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atakubaliana nami kwamba, sasa hivi *collection* ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tulikubali kwamba, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atakapotoa kwenye gazeti kwamba, sasa tuingize na Halmashauri za Mikoa mingine; Sisi TRA tutafanya kazi na Halmashauri hizo katika ku-*improve* mapato. Tumwombe tu Mheshimiwa Waziri, aangalie makusanyo ya Dar es Salaam kupitia Ilala, Temeke na Kinondoni, basi aturuhusu ili tuweze kuongeza Halmashauri nyingine tuweze kufanya kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika hili, nataka niseme kwamba, Serikali imesema kupitia Bunge lako Tukufu na itaendelea kusema, tunataka kudhibiti mianya. Tutaendelea kudhibiti mianya, kwa sababu mapato inawezekana yanapatikana, lakini kwa sababu kuna mchwa anakula mapato yetu, sisi wengine tutakuwa hatuyaoni hayo mapato.

Kwa hiyo, hili tumesema tutadhibiti mapato na ndio maana sasa tumeanzisha utamaduni wa kuweka mikono yetu katika Halmashauri. Hii itatusaidia sana kuongeza mapato katika vianzio vyetu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu katika hili, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu sisi ni Madiwani katika Halmashauri zetu, tusaidiane basi katika hili. Mimi ninaamini katika Halmashauri zetu tunazosimamia, Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kudurusu na kukokotoa mapato na tuka-*question* mapato yale.

Kwa hiyo, tusaidiane katika ku-*prove* eneo lile. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Lubeleje, Watanzania wote na Waheshimiwa Wajumbe wote walioko katika Halmashauri kuwa, Serikali itahakikisha kwamba, ina- *improve* mapato ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi*)

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa hiyo, sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009
### *(The Finance Bill 2009)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchango wangu nilishauri kwamba, katika ibara hii ya nne, ibara mpya ya 10(A), kuna neno limetumika pale ambalo halikukamilika; *quasi judicial* panakosekana *hyphen* pale na kuna vifungu vingine nitajaribu kusema hivyo isipokuwa kama imeonekana kwamba si sawa wakati tunachangia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwani inabadili maana; kuna neno lililokosekana?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI - MHE. JEREMIA S. SUMARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 5

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya tano inayosomwa hapa ni ile ambayo iko *part three;* siyo?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema hivi; kile kiambatanisho cha *schedule of amendments* kitakachokuwa kinasoma aina mbalimbali za bidhaa zitakazotozwa au kutokutozwa kodi, ile sehemu inayotaja *crude oil,* naomba Mheshimiwa Waziri nimshauri watafute neno lingine litakalotumika badala ya *crude oil.*

Hii ni kwa sababu utafiti wote na mimi juzi nilikuwa Malaysia; Malaysia hawazalishi *crude oil*, Indonesia hawazalishi *crude oil* wala Singapore hawazalishi *crude oil.* Mafuta waliyonayo ni *semi-refined*. Ndio maana nataka tuelewe kwa nini litumike neno ambalo kule yanakotoka halipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, lakini hicho kifungu kidogo cha tano hakina *schedule of amendment.*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu una kiambatanisho kinachoonesha kodi mbalimbali ambazo zitatozwa na ili zitozwe, lazima kifungu kitajwe ni cha aina gani. Ndicho ninachozungumzia mimi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Mzindakaya, sijakuelewa kwa sababu tuko kifungu cha tano. Kifungu hicho cha tano, hakiendani na *schedule of amendment,* kiko kama kilivyo. Sasa labda ungekaa unisikilize.

Ningetaka nijue, una neno lolote ambalo linasumbua kwenye kifungu kile cha tano, tutakapofika hapo unaposema, basi utatoa ushauri unaotaka kuutoa. *Specific* kwenye kifungu cha tano una neno?

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wako, mbele ya safari.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mwenyekiti hali kadhalika, ibara ya sita mpya, kuna neno pale linakosekana ile *hyphen* kwenye *quasi judicial body.*

**MWENYEKITI:** Tumeiona, Mheshimiwa Waziri; nadhani hatuna neno?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna neno.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 9(b), naona kama kuna makosa; kwa sababu ukianza pale juu inasema: "*For the purpose of subsection (2), "dutiable value" means in relation to:"* Ukienda (b) yanaanza maneno yale yale *in relation to.* Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri yale maneno *in relation to* kwenye *Bill* pale yako *redundant.*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 13, ibara ya 139 (A); ina neno vilevile ambalo linakosa kile kiunganishio pale *quasi judicial body*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi nafikiri sasa tukubalianae kwa ibara hiyo na maeneo yote sasa ambayo yana tatizo hili, tukubali kwamba tunayarekebisha yote kwa pamoja; tunaafikiana?

**WABUNGE:** Ndiyo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni hiyo hiyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali itueleze kwamba, baada ya *concession* ambazo zimefanywa kuhusiana na haya mafuta ya mbegu kutoka ushuru wa asilimia kumi kwenda sifuri; ambao umeitikia mchango wa Waheshimiwa Wabunge, hasa kwenye Ahadi ya Serikali; maana tunapitisha sheria sasa. Tulitegemea kuona kwenye eneo hili kuhusiana na Kodi ya Ongezeko la Thamani, ambalo Serikali imesema hawa wakulima wadogo hawatalipa VAT ya asilimia kumi na nane.

Sasa hatuwezi tukasema hili limekubalika bila kuingizwa katika marekebisho haya. Napenda Serikali ituhakikishie; tunafanya nini katika hatua hii na lugha hiyo iko wapi ili twende pamoja? *(Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli anachosema Mheshimiwa Andrew Chenge kwamba, kwa hali ya kawaida, tungekwisha tengeneza *schedule of amendment*, ambayo ingeonesha dhahiri mabadiliko ambayo Mheshimiwa

Waziri wa Fedha na Uchumi ameridhia. Kutokana na mwenendo wa muda, imekuwa vigumu kuchapisha *schedule of amendment* tangu hoja za Wabunge zilipokwisha kutolewa leo asubuhi, halafu Serikali kwenda kujadiliana na kukubaliana na kuja kutoa msimamo hapa.

Kwa hiyo, tunaomba kwamba, aliyoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa sababu yatanaswa kwenye *Hansard*, basi marekebisho hayo yaunganishwe kwenye Muswada wenyewe utakapokwenda kuchapishwa. Endapo Bunge litaamua, basi baada ya machapisho hayo, linaweza kupitishwa kwenye Kamati ili kuhakikisha kilichosemwa hapa na Waziri wa Fedha na Uchumi, kimekuwa *captured* kwenye *schedule of amendment* na kwenye Muswada na kwa hiyo kusiwe na hitilafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana, lakini niseme kwamba, kitu alichokizungumza Mheshimiwa Chenge pia kina mantiki katika utendaji bora wa kazi na shughuli za Bunge. Sasa ningeomba tukubaliane, pamoja na Kamati kupelekewa lakini Bunge ndilo linalopitisha na si Kamati kwa mujibu wa Kanuni na kwa mujibu wa Sheria

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri sasa aseme, mabadiliko hayo yachukuliwe kwenye *Hansard* na yapitishwe na Bunge na Kamati sasa itakwenda kufuatilia kama yatakuwa yameandikwa kama Bunge lilivyopitisha. Kwa hiyo, ningeomba uyaseme mabadiliko yale tuliyoyapendekeza na yanayokubalika katika kifungu hiki ili *Hansard* iweze kuyanukuu na Kamati ya Bunge itathibitisha kama yapo hivyo kuliko kuiachia Kamati na Sheria inasema Bunge ndio litapitisha.

Mheshimiwa Waziri, naomba ufanye hilo ili tuweze kukipitisha kifungu hiki, pamoja na hayo mabadiliko yaliyochelewa kuingizwa kwenye *schedule of amendment.*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. La kwanza ni kufuta aya ya kifungu cha ishirini na saba, ambayo nafikiri bado hatujaifikia.

**MWENYEKITI:** Hicho cha ishirini na saba kiache, tutakapofika mtatupa taarifa hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakupa taarifa kadiri tunavyoendelea kwenye vifungu.

**MWENYEKITI:** Sawa, kama mtakuja kuisema kwenye kifungu cha ishirini na saba.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa sawa.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tupate maelewano kwamba, kwa sababu kifungu hiki kinahusika na *Value Added Tax*, kwenye chai na kahawa, naamini tumeelezwa kwamba, hiyo itasitishwa na vilevile itazingatiwa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninathibitisha kwamba, ndiyo itaahirishwa kwenye chai na kahawa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati huo sasa tukisubiri Meza ya Wanasheria wetu itusaidie kufikia kifungu hicho namba ishirini na saba, tuendelee sasa kupitisha hivi vilivyotangulia mbele.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuona kwamba, sasa tunataka kufanya mambo kienyeji. Jambo hili halijawa tayari, kwa kutumia Kanuni zetu za Bunge, inabidi lirudishwe kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, likiiva ndio lije tena hapa. *(Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga, ungetoa hoja na kama hoja yako ingeungwa mkono, ningelihoji Bunge kurudisha Muswada huu sasa kwenye Kamati ya Bunge. Sasa wewe umesimama kutoa ushauri bila kutoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, ninachoweza kufanya, nitakiahirisha kifungu hiki kwa kutoa muda wa dakika kama tatu, Mheshimiwa Waziri afanye *consultation* na Timu ya Wanasheria halafu aje kutupa majibu. Tunaendelea na ishirini na mbili, tunatoa muda wa dakika tano tu Waheshimiwa Wabunge. Kama ingetolewa hoja, tungeahirisha tukaendelea kufanya utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Job Ndugai.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni utaratibu uliozoeleka hapa Bungeni kwamba, kwa hatua kama hii, Kamati na Mheshimiwa Waziri wanakuwa wameelewana. Ningependa kutoa hoja kwamba, jambo hili lirudishwe kwenye Kamati, kwa muda wa nusu saa wanaweza kuwa wamemaliza na tukaendelea kumalizia vifungu vilivyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitarudi kuvaa joho halafu nitawahoji ili muiamue tuingie hatua inayofuata. Kwa hiyo, narudi kwanza kuvaa joho ili niwahoji.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Kama tulivyoona, tumepata utata wa kuendelea kupitisha Muswada huu katika kifungu hicho kidogo cha ishirini na moja. Kwa kuwa Serikali haikupata nafasi ya kuleta Jedwali la Marekebisho na hivyo kutupelekea kufikia katika kifungu hicho bila kuwa na Jedwali hilo; na Mheshimiwa Job Ndugai, ametoa hoja Bunge liahirishwe mpaka Kamati na Wizara waweze kuafikiana katika kifungu hicho.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Job Ndugai, ametoa hoja Bunge liahirishwe kwa muda wa nusu saa; na sasa hivi ni saa kumi na mbili kasoro dakika tano, kwa hiyo, nusu saa ananiambia tutakutana tena hapa saa kumi na mbili. Ngoja niendelee kutoa maelekezo, kwa sababu kila ninachowahoji lazima muelewe nawahoji nini; kwa mujibu wa Mheshimiwa Job Ndugai, Bunge liahirishwe kwa muda wa nusu saa, ina maana tuahirishe Bunge. Hoja hiyo itahusu kuahirisha Bunge mpaka saa kumi na mbili na nusu, halafu turudi tena ndani kwa ajili ya kumalizia kazi iliyokuwa imebakia.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na mbili na nusu, baada ya kupata taarifa ya Kamati na Wizara katika kuafikiana kwenye suala hili na hasa kwa utayari wa *schedule of amendment.*

*(Saa 11.55 jioni Bunge lilifungwa mpaka saa 12.30 jioni)*
*(Saa 12.30 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Wahehsimiwa Wabunge, tulikubaliana kurejea saa kumi na mbili na nusu na sasa tumerejea tena kumalizia shughuli yetu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli hizi, tuliwapa Kamati kwa mujibu wa Kanuni zetu, wakamalizie kuondoa utata katika kifungu tulichokuwa tumeishia na tulitumia kanuni zetu za Bunge. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ili aweze kutoa taarifa ya shughuli ya Kamati iliyofanyika.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA (MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa

Kanuni za Bunge, Kamati ya Fedha na Uchumi, inatoa taarifa kuwa, imekubaliana na Serikali kuhusu marekebisho katika Muswada huu, kuhusiana na eneo la mafuta ghafi, pamoja na kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Chai na Kahawa. Marekebisho hayo, yatawasilishwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, yatagusa ibara ya 27 ya Muswada uliopo mbele yetu na tunaoujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, tunakushukuru sana kwa taarifa hiyo, kwa niaba ya Kamati yako.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009
***(The Finance Bill, 2009)***

Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

**MHE. JEREMIAH S. SUMARI (NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisome marekebisho ya ziada ya kifungu cha 27 cha Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2009, unaohusu kifungu cha 27; na kwa sababu hatujapata muda wa kukichapisha, ninaomba nikisome kama kitakavyoonekana kwenye sheria yenyewe na ninaomba *Hansard* pia wakinase. Ninasoma kama ifuatavyo:-

*Enclose 27 by;*
*(a) Deleting paragraph (a);*
*(b) Renumbering paragraphs (b),(c),(d),(e) and (f);*
*(c) Adding a new paragraph after paragraph (f) as renumbered (g) "by adding a new item 30 as follows: "Supply of crude edible oil. The supply of crude edible oil by a local processor to a local edible oil processing plant."*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 28(a) ambayo inasema, *deleting item 8 and substituting for them the following*. Sasa katika hii ambayo inakuwa *substituted,* mstari wa nne kuna maneno yanasomeka; "*The Customs Laws*, kuna maneno yanasomeka *PR service* sijaona kwenye *schedule* ya marekebisho; yale maneno hayana maana pale na bahati nzuri niliwasiliana na wanasheria humu ndani wakasema yameingizwa pale kimakosa.

**MHE. JEREMIAH S. SUMARI (NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaafiki haya tutayatoa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 29

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, Kanuni namba ngapi?

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni Namba 68(7). Leo asubuhi, iliwasilishwa Taarifa ya Mwaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 37(4) inayosema; baada ya Hati kuwasilishwa Bungeni, Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge, anaweza kutoa hoja kwamba Bunge liijadili Hati hiyo. Kwa kuwa muda haujatajwa *specifically* na bado Hati hii imewasilishwa leo; na kwa kuwa baada ya kutoka nje kwenye *pigeon hole* tuliziona; nakusudia kutoa hoja kwamba ijadiliwe.

Ninataka mwongozo wako kwamba; je, muda wa kutosha upo kwa sababu hamjataja *time* au lah!?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa na ndiyo maana ulikaa kabla hata sijawaruhusu, kwa sababu ulitaka kuwahisha shughuli kabla ya wakati wake. Kwa busara za Kiti, ninaomba tumalize hoja iliyopo mbele yetu halafu nitakupa mwongozo wa hicho unachokisema.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika. Kama nilivyochangia, hatuna *schedule of amendment* na bahati nzuri, Mawaziri wamesikia wamefanya mabadiliko, lakini kuna jambo ambalo ninataka mwongozo wako. Sheria hii imezungumzia *crude edible oil*, lakini kwa taarifa yangu mimi na bahati nzuri kaka yangu Mheshimiwa Dr. Mzindakaya amenisaidia, inayokuja ni *semi-refined*; je, viwanda hivi badala ya kuleta *crude* wakaleta *semi-refined* washtakiwe?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, miongozo yote itapatiwa majibu baada ya kupitisha Muswada wenyewe; hebu tumalizie hatua tuliyoifikia kwanza, kwa sababu tukianza kusikiliza miongozo, hatutamaliza kazi ambayo iko mbele yetu.

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE (NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2009 *(The Finance Act, 2009)*, kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Naomba kutoa hoja kwamba, Taarifa hiyo ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatua hii sasa inabakia kwa Mheshimiwa Rais, kushughulika na Muswada huu na hatimaye uwe sheria na uweze kutumika katika nchi yetu.

Niendelee kuwaomba wenzetu wa Serikali, kupitia Mawaziri husika na Baraza zima la Mawaziri, litusaidie haya tuliyoyapitisha katika Bunge letu, yaweze kufanyiwa kazi vizuri kwa Mwaka wa Fedha huu wa 2009/2010 na tutakutana tena kwenye Bajeti ijayo, kuona yapi yamefanikiwa na yapi hayajafanikiwa.

Waheshimiwa Wabunge, hatua hiyo tumemaliza na nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri. Vilevile nichukue nafasi hii, kuwapongeza

tena Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine, Bunge hili leo limetumia muda wake vizuri kuhakikisha linafanya kazi yake ipasavyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamaliza, ninayo matangazo kadhaa hapa Mezani, lakini pia ninayo miongozo miwili ambayo Waheshimiwa Wabunge wameniomba.

Waheshimiwa Wabunge, nikianza kwa suala la Mheshimiwa Dokta Zainabu Gama, Sheria tumeshaipitisha, suala linalofuata ni la kiutawala ndani ya Wizara. Kwa hiyo, ninafikiri sasa tuwaachie Wizara, kanuni zitakazotungwa na usimamizi ndiyo utakaoleta sasa mwelekeo wa utekelezaji wa sheria yenyewe, hatuwezi kurudi tena kujadili sheria ambayo tumeshaipitisha. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Dokta Gama, mjadala huo sasa umefungwa na kwa mujibu wa Kanuni mjadala wa sheria hii umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, nikirudi kwa Mheshimiwa Mnyaa ni kweli Kanuni Namba 37 inasema, Hati inaweza kuwasilishwa Bungeni wakati wa Vikao vya Bunge na Waziri, Mwanasheria Mkuu, Kamati ya Bunge ama Mbunge yeyote. Namba mbili ya Kanuni hiyo inasema, nakala za matoleo yote ya gazeti, pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri na kugawiwa kwa Wabunge. Namba tatu inasema kwamba, Hati zote zitawasilishwa Bungeni bila kutolewa hoja yoyote kwa ajili hiyo.

Namba nne inasema kwamba, baada ya Hati kuwasilishwa Bungeni, Waziri ama Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge yeyote, anaweza kutoa hoja kwamba, Bunge liijadili Hati hiyo, baada ya kuwasilishwa Mezani.

Waheshimiwa Wabunge, Hati imewasilishwa leo asubuhi, maamuzi yangu; neno baada halinisaidii kujua ni baada ya Hati kuwasilishwa ama ni siku nzima toka Hati imewasilishwa. Kwa mantiki hiyo, nitamwomba Mwanasheria wa Bunge atusaidie, akimsaidia pia Mheshimiwa Mnyaa kutoa maana ya baada na baada ya hapo Jumatatu tutalitolea maamuzi kama Mheshimiwa Mnyaa yupo sahihi ama kanuni yetu inasema vinginevyo.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ni maamuzi yangu katika miongozo niliyopewa na naomba niendelee na matangazo. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shellukindo, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, wakutane kesho tarehe 20 Juni katika Ukumbi Namba 219 uliopo katika Jengo la Utawala, ghorofa ya pili, kuanzia saa tano kwa ajili ya kikao.

Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, anaomba Wajumbe wake wakutane kuanzia kesho tarehe 20 - 21 Juni 2009, saa tatu asubuhi katika Ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala; kutafanyika vikao vya Kamati, kuchambua na kujadili Taarifa za Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009.

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo; Waheshimiwa Wabunge wenye Halmashauri hizo, mnaweza kuhudhuria; Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati hiyo ninaomba mhudhurie kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, tumepokea ratiba ya mbio za Mwenge wa Uhuru kwa nchi nzima. Nimeombwa niwatangazie kwamba, ratiba hizo zimewekwa kwenye visanduku vyetu vya barua, kwa hiyo, tukipita pale tutakuta ratiba ya mbio za mwenge katika Majimbo yetu zimeshatolewa tayari kwa ajili yetu.

Waheshimiwa Wabunge, tumepokea fomu za kujiandikisha watakaoshiriki mbio za *Olympic* kesho. Nimeombwa niwatangazie wote wanaopenda kushiriki, wajiorodheshe leo kwenye Jengo la Utawala; fomu za kujiandikisha na ratiba za shughuli zote kwenye mbio hizo zitapatikana sehemu ya mapokezi, utawala ama ndani ya ukumbi kabla hatujatoka. Waheshimiwa Wabunge wote, tunaombwa sana tushiriki na wale wote wanaotaka kushiriki mbio hizo kesho wafanye hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yaliyokuwa Mezani na ninaomba niseme, ninawashukuru sana kwa ushirikiano; siku imekuwa ndefu lakini tumeimaliza vizuri. Baada ya kusema hayo, ninaomba niwatakie kila la kheri kwa *week end* hii na sasa naahirisha shughuli za Bunge za leo mpaka Siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi ndani ya ukumbi huu.

*(Saa 12.47 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 22 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)